MARY NJERI NDUNG'U

UNIVERSITY OF NAIROBI
EAST AFRICANA COLLECTION

M.A

CHUO KIKUU CHA NAIROBI

2009

# "MADA NA FOKASI KATIKA KISWAHILI SANIFU: MTAZAMO WA MUUNDO WA TAARIFA"

Na

MARY NJERI NDUNG'U

Tasnifu hii imetolewa ili kutosheleza baadhi ya mahitaji ya Master of Arts, Idara ya Isimu na Lugha

CHUO KIKUU CHA NAIROBI

2009

University of NAIROBI Library
0472450 6

# UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na kwa maoni yangu haijawahi kutolewa kwa mahitaji ya shahada yoyote katika Chuo Kikuu kingine chochote.

**MARY NJERI NDUNG'U**

19/10/2009

Tasnifu hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yetu tukiwa wasimamizi walioteuliwa na Chuo Kikuu cha Nairobi.

**BW. BASILIO GICHOBI MUNGANIA**

21.10.2009

**DKT. JOHN HAMU HABWE**

21/10/2009

# TABARUKU

Kazi hii naitabarukia wazazi wangu Bw. Joseph Ndung'u na Bi. Janet Wambui Ndung'u. Mmenifaa kwa mengi na kunihimiza katika yote. Aidha kwa wapwa zangu wote katika uchanga wao, Mungu awajalie maishani.

# SHUKRANI

Kufanikiwa kwa kazi hii kumechukua juhudi na kujitolea kwa watu mbalimbali. Sio rahisi kuwataja wote walionifaa kwa hali na mali mbali nitawataja baadhi yao.

Nawashukuru sana wasimamizi wangu Bw. Basilio Gichobi Mungania na Dkt. John Hamu Habwe kwa kuniongoza na kunipa ushauri bila uchovu katika utafiti huu hadi mwisho. Ushauri wenu na mwongozo dhabiti zimeniwezesha katika kufanikisha kazi hii.

Nawashukuru pia wahadhiri wote katika Idara ya Isimu na Lugha, Chuo Kikuu cha Nairobi, hususan wale walionifunza. Hawa ni pamoja na Dkt. John Habwe, Bw. Basilio Mungania, Dkt. Mwenda Mbatia, Prof. Kithaka wa Mberia, Prof. M. Abdulaziz, Dkt. Kineene wa Mutiso, Dkt. Ayub Mukhwana, Dkt. Zaja Omboga, Dkt. Tom Olali na Dkt. Burugeya. Namshukuru pia Bi. Priscah Jerono ambaye alitembea nami mwanzoni mwa utafiti huu.

Natoa shukrani zangu kwa wanafunzi wenzangu Gitonga, Linah, Nyaga, Josephine, Mukabane na Margaret. Tumelisukuma gurudumu hili pamoja hadi mwisho. Lucy Wairima na Catherene Munga, nawashukuru kwa dhati ya moyo wangu, milima na mabonde yote tumeyapitia pasi na kupiga moyo konde.

Aidha nawashukuru wazazi wangu wapendwa Bw. Joseph Ndung'u na Bi Janet Wambui Ndung'u. Mlinipa msingi imara katika malezi na pia elimu. Nawashukuru kwa hisani yenu isiyo kifani na maombi yenu kila mara. Asanteni sana.

Pia shukrani zangu ziwaendee ndugu zangu ambao wamenivumilia kwa mengi waliponihitaji nikiwa maktabani. Pokeeni shukrani zangu; Waweru, Lucy, Fr. Kim, Ciku, John, Bati, Michael, Nyambura, Kamau, Njoki, Wangui, Kiragu na Mangi. Shukrani zangu pia ziwaendee shemeji na wifi zangu.

Ningependa kuwashukuru wapwa zangu wote katika umri wao mchanga. Mungu awajalie kufanikiwa maishani.

Shukrani tele ziwaendee marafiki zangu wote hasa Bi Asumpta Mulila na Bw. Timothy Arege ambao wamenifaa kwa ushauri na kunihimiza kila wakati kuwa nitashinda. Shukrani.

Kadhalika shukrani kwa Chuo Kikuu cha Nairobi kwa kunipa fursa ya kuendeleza masomo yangu.

Zaidi ya yote, shukrani zote ni kwa **Mwenyezi Mungu** aliyeniwezesha katika yote. **Amina.**

# IKISIRI

Utafiti huu umeshughulikia mada na fokasi katika Kiswahili Sanifu. Tumechunguza na kuchanganua tungo ambazo hutambulisha mada na fokasi huku tukitolea maelezo na ufafanuzi wa kina. Malengo ya utafiti huu ni kuchunguza ikiwa kuna uhusiano kati ya mada na fokasi. Pia tumechunguza utambulishaji wa mada na fokasi huku tukitathmini ikiwa mada na fokasi huweza kutambulishwa kwenye kirai, kishazi au kileksika. Mwisho tumetathmini kufanikiwa kwa Mtazamo wa Muundo wa Taarifa katika utambulishaji wa mada na fokasi katika Kiswahili Sanifu.

Nadharia ambayo imetuongoza katika utafiti huu ni Mtazamo wa Muundo wa Taarifa iliyoasisiwa na Wanaisimu wa Shule ya Prague, ikaendelezwa na Halliday (1967) na baadaye kukuzwa zaidi na Lambrecht (1994). Muundo wa taarifa husimbwa katika sentensi katika utambulishaji wa mada na fokasi ili kubainisha ni sehemu gani ya sentensi inayobeba taarifa mpya na ni sehemu gani inayobeba taarifa inayojulikana.

Katika uchanganuzi wa data, tumeteua dâta kutoka riwaya ya *Kuli* ya Adam Shafi (1979) ambayo tumetumia kama data ya kimsingi. Aidha tumepata data zaidi kutoka makala mbalimbali zilizochapishwa. Zaidi ya hayo tumezalisha data ili kukidhi mahitaji yetu katika uchanganuzi wa tungo ambazo hutambulisha mada na fokasi katika Kiswahili Sanifu.

Sura ya kwanza ni utangulizi wa utafiti huu. Imejumlisha utangulizi, mada ya utafiti, madhumuni ya utafiti, nadharia tete, sababu za kuchagua mada hii, upeo na mipaka, uhalalishaji, msingi wa kinadharia, yaliyoandikwa kuhusu mada ya utafiti na mbinu za utafiti.

Sura ya pili imeshughulikia maswala ya kimsingi yanayohusiana na mada, fokasi na msingi wa kinadharia wa Muundo wa Taarifa. Katika sura ya tatu, tumeshughulikia na kuchanganua tungo ambazo hutambulisha mada. Tumepata kuwa mada katika sentensi huhitaji kuakisiwa kama vile katika kuitanguliza katika sentensi, kuihamisha kushoto miongoni mwa njia zingine.

Sura ya nne imejikita katika uchanganuzi wa data katika tungo ambazo hutambulisha fokasi katika Kiswahili Sanifu. Tumechunguza aina za fokasi kama vile fokasi kwenye kiarifu, fokasi kwenye KN na fokasi katika sentensi miongoni mwa aina zingine za fokasi.

Katika sura ya tano, tumeangalia jinsi mada na fokasi huhusiana katika muktadha wa utambuzi, uchochezi, na ulinganuzi. Tumepata kuwa mpangilio wa maneno katika sentensi huwa na mchango mkubwa katika utambulishaji wa mada na fokasi katika Kiswahili Sanifu ambao huwa huru kwa kiasi.

Sura ya sita inabeba hitimisho na mapendekezo ya utafiti huu. Katika hitimisho tumetoa matokeo ya utafiti yanayohusiana na utambulishaji wa mada na fokasi katika Kiswahili

Sanifu. Mapendekezo ambayo tumetoa yatachochea tafiti zaidi katika uwanja huu. Tumependekeza kuwa tafiti zaidi zifanywe katika uchanganuzi wa data wa kimofosintaksia katika utambulishaji wa mada na fokasi katika Kiswahili Sanifu. Pia tafiti zaidi ambazo zitaongozwa na nadharia tofauti au utafiti katika usimbaji wa muundo wa taarifa kwenye tungo changamani za kimofosintaksia au za kiarudhi

# YALIYOMO

**Yaliyomo** **Ukurasa**

## SURA YA KWANZA

Ungamo ........................................ i
Tabaruku ........................................ ii
Shukrani ........................................ iii
Ikisiri ........................................ v
Yaliyomo ........................................ viii
Tafsiri za dhana muhimu ........................................ xi

**1.0. Utangulizi ........................................ 1**
1.1 Utangulizi ........................................ 1
1.2 Mada ya Utafiti ........................................ 3
1.3. Madhumuni ya Utafiti ........................................ 7
1.4 Nadharia Tete ........................................ 8
1.5 Sababu za Kuchagua Mada hii ........................................ 8
1.6 Upeo na mipaka ........................................ 10
1.7 Uhalalishaji ........................................ 10
1.8 Msingi wa Kinadharia ........................................ 11
1.8.1 Mtazamo wa Muundo wa Taarifa ........................................ 11
1.8.2 Umuhimu wa Mtazamo wa Muundo wa Taarifa katika Sarufi ........................................ 17
1.9. Yaliyoandikwa kuhusu mada ya utafiti ........................................ 18
1.10 Mbinu za Utafiti ........................................ 24
1.10.1 Ukusanyaji Data ........................................ 24
1.10.2 Uchanganuzi wa Data ........................................ 25

## SURA YA PILI


**2.0 Mada, Fokasi, Muundo wa Taarifa, Umbo la Kisintaksia, Muundo wa Sentensi na Uainishaji wa Hadhi ya Taarifa.... 26**

2.1 Utangulizi........................................................................ 26

2.2 Mada................................................................................ 26

2.2.1 Mada ya sentensi na mada ya diskosi ........................... 28

2.3 Fokasi .............................................................................. 29

2.3.1 Uamilifu wa fokasi linganuzi......................................... 30

2.4 Mada, fokasi na mpangilio wa maneno............................ 30

2.5 Vipashio vya taarifa.......................................................... 32

2.6 Makundi ya Toni na Mkazo.............................................. 34

2.7 Muundo wa Taarifa na Umbo la Kisintaksia.................... 36

2.8 Muundo wa Taarifa na Muundo wa Sentensi.................... 38

2.9 Uainishaji wa Hadhi ya Taarifa......................................... 41

2.10 Hitimisho........................................................................ 42


## SURA YA TATU


**3.0 Tungo Zenye Kutambulisha Mada.............................. 44**

3.1 Utangulizi........................................................................ 44

3.2 Kutanguliza mada katika sentensi..................................... 44

3.3 Kuhamisha mada kushoto................................................. 49

3.4 Kuhamisha mada kulia...................................................... 53

3.5 Kuhamisha yambwa tendwa na yambwa tendewa............ 60

3.6 Hitimisho.......................................................................... 64


## SURA YA NNE


**4.0 Tungo Zenye Kutambulisha Fokasi............................ 66**

4.1 Utangulizi........................................................................ 66

4.2 Aina za fokasi.......................................................................66

4.2.1 Fokasi kwenye kiarifu................................................66

4.2.2 Fokasi katika sentensi................................................69

4.2.3 Fokasi kwenye Kirai nomino......................................72

4.2.4 Fokasi Finyu..............................................................75

4.3 Fokasi katika ukanushaji..............................................................77

4.4 Fokasi katika tungo za maswali ya majibu ya ndiyo/la.................81

4.5 Fokasi katika maswali ya majibu yanayohitaji maelezo................83

4.6 Kuhamisha fokasi kushoto..............................................................86

4.7 Hitimisho.......................................................................................88

## SURA YA TANO

**5.0 Uhusiano Kati ya Mada na Fokasi.............................. 90**

5.1 Utangulizi......................................................................... 90

5.2 Utambuzi, Uchochezi na vigezo vya mada-fokasi..................... 91

5.3 Ulinganuzi.......................................................................... 95

5.3.1 Fokasi linganuzi.......................................................... 95

5.3.2 Mada Linganuzi........................................................... 99

5.4 Hitimisho............................................................................ 101

## SURA YA SITA

**6.0 Hitimisho na Mapendekezo................................... 103**

6.1 Utangulizi........................................................................... 103

6.2 Hitimisho............................................................................ 103

6.3 Mapendekezo...................................................................... 110

**MAREJELEO .................................................................... 111**

# TAFSIRI ZA DHANA MUHIMU

| | |
|---|---|
| Arifu yakinishi | affirmative declarative |
| Dai la kipragmatiki | pragmatic assertion |
| Diskosi/usemi | discourse |
| Faridipeke | particle |
| Fokasi | focus |
| Fokasi linganuzi | contrastive focus |
| Fokasi isiyotarajiwa | contingency focus |
| Fokasi sahihishi/rekebishi | corrective focus |
| Fokasi ya kutambulisha upya | reactivating focus |
| Kanuni ya Utengano wa Urejeleo na Uamilifu | Principle of Separation of Reference and Role |
| Katafora | cataphora |
| KH (kirai husishi) | prepositional phrase |
| KN (Kirai Nomino) | argument |
| KN (kirai nomino) | noun phrase |
| KT (kirai tenzi) | verb phrase |
| Kuhamisha kushoto | clefting |
| Kuhamisha mada kulia | right dislocation |
| Kuhamisha mada kushoto | left dislocation |
| Kuhamisha yambwa | dative shifting |
| Kusimba | encode |
| Kutanguliza mada katika sentensi | Y-movement |

| | |
|---|---|
| Kutanguliza mwanzoni mwa sentensi | fronting |
| Leksimu | lexeme |
| Mada | topic |
| Mada linganuzi | contrastive topic |
| Mada ya diskosi | discourse topic |
| Mada ya sentensi | sentential topic |
| Mpangilio funge wa maneno | fixed word order |
| Mpangilio huru wa maneno | free word order |
| Mrejeosabiki | anaphora |
| Muundo wa taarifa | Information Structure |
| Nguvu ya Mawasiliano | Communication Dynamism |
| T (kitenzi) | verb |
| Taarifa | information |
| Taarifa inayojulikana | given information |
| Taarifa mpya | new information |
| Taarifa iliyomo | information content |
| Uchochezi | activation |
| Uchukulio wa kipragmatiki | pragmatic presupposition |
| Umaanisho | implicature |
| Utambuzi | identifiability |
| Utambulishaji mada | topicalization |
| vielezi vumishi | adverbial modifiers |
| Welekeo | probability |

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI

## 1.0 Utangulizi

Kwa mujibu wa Mgullu (1999:12), lugha ya Kiswahili ni miongoni mwa lugha za Kibantu zinazozungumzwa katika maeneo ya Afrika Mashariki na ya Kati. Ni miongoni mwa lugha za Kibantu ambazo ni ambishi. Ni lugha ambayo hutumia viambishi mbalimbali ili kuwakilisha dhana mbalimbali. Mahusiano ya kisarufi hudhihirishwa na viambishi mbalimbali vya mwanzo au fuatilizi kwenye mzizi wa kitenzi. Kila kiambishi huwa na uamilifu wa kisarufi. Kitenzi cha Kiswahili huambishwa viambishi vinavyoandamana na mzizi wa kitenzi na huwa na athari kwenye kategoria za maneno katika sentensi. Kitenzi cha Kiswahili huathiriana na nomino katika sentensi. Kiima huwakilishwa katika kitenzi na kiambishi kitangulizi. Kwa mfano:

1. **a**. Mtoto **a**limlilia mamake.

   **b**. Chakula **ki**liiva kabla ya wageni kuwasili.

   **c**. Nguo **zi**lifuliwa **zi**katakata.

Athari kati ya kategoria za maneno katika tungo husaidia katika utambuzi wa mada na fokasi katika kiwango cha kirai na kishazi. Hili hutokana na jinsi maneno hupangwa katika virai na vishazi mbalimbali.

Kategoria za maneno kama vile nomino na vielezi huathiriwa na kitenzi huku viambishi vikiathiri yambwa tendwa na tendewa, kauli, hali n.k. Kwa mfano:

**2. Maria a-li-m-nunu-li-a Juma kitabu jana.**

Vile vile lugha ya Kiswahili huwa na mpangilio wa maneno ulio huru kwa kiasi hivi kwamba kategoria za maneno huweza kupangwa kwa kutanguliza na kumalizia kwa kategoria yoyote bila kupotosha maana iliyokusudiwa mwanzoni. Kwa mfano sentensi inayofuata huweza kuandikwa kwa kufuata mipangilio ifuatavyo:

**3. Juma ameijengea nyumba paa.**

**a. Paa, Juma ameijengea nyumba.**

**b. Ameijengea nyumba paa Juma**

**c. Nyumba paa Juma ameijengea. n.k**

Mpangilio wa maneno husaidia na huchangia kwa kiwango kikubwa katika utambulishaji wa mada na fokasi katika Kiswahili Sanifu.

Mbali na mpangilio wa maneno, kiimbo ni dhana nyingine ambayo huchangia katika utambulishaji wa mada na fokasi. Kiimbo huhusu kupanda na kushuka kwa sauti wakati wa kutamka maneno, virai au vishazi katika sentensi. Kiimbo hutumika katika kutofautisha dhamira ya kauli kama vile: *anakula, anakula! au anakula?* Katika mazungumzo kiimbo hutumika kutambulisha vipashio vya kisarufi kwa kuonyesha mipaka ya sentensi, vishazi au maneno kama vile: *Kama kule nyuma, mbele kulikuwa pia kumefungwa.* Udhihirishaji wa mipaka katika viambajengo vya usemi hutumiwa katika utambulishaji wa mada na fokasi.

Tasnifu hii imelenga kuonyesha jinsi mada na fokasi hutambulishwa katika sentensi za Kiswahili Sanifu. Utafiti huu umeongozwa na mtazamo wa Muundo wa Taarifa ambao

huchangia pakubwa katika utambulishaji wa taarifa iwe ni taarifa inayojulikana au taarifa mpya katika sentensi na katika diskosi.

Mada na fokasi ni dhana ambazo hutumika kurejelea vitambulishi vya taarifa katika uwekaji mkazo ambao huweza kutumika ili kuzipa sehemu za sentensi, mofu, maneno, virai au vishazi msikiko na msisitizo. Jukumu la msikiko na msisitizo ni kutambulisha taarifa upya. Kazi chache zimefanywa katika sarufi ya Kiswahili kuhusiana na mada na fokasi. Wataalamu ambao wameshughulikia mada na fokasi katika Kiswahili ni kama vile Maw (1976), Augustine (2004) na Vitale (1981). Kazi zaidi zimefanywa katika lugha tofauti kama vile Chichewa, Sesotho, Kiingereza, Kichina, Kijapani, n.k.

Utafiti umelenga kuongezea mchango wa watafiti kama Maw (1976), Augustine (2004) na Vitale (1981) tukizingatia wazo kuwa ikiwa tafiti zingine zimefanywa katika lugha nyingine kuhusiana na fokasi na mada, inawezekana kuchunguza suala la mada na fokasi katika lugha ya Kiswahili. Kazi hii ni jaribio la kudhihirisha jinsi mada na fokasi husimbwa katika Kiswahili Sanifu.

## 1.2 Mada ya Utafiti

Zipo tafiti nyingi zilizofanywa kuhusu lugha ya Kiswahili. Kazi nyingi zimelenga vipengele vingine vya kisarufi na fasihi ya Kiswahili Sanifu. Baadhi ya tafiti hizi zimeshughulikia fonolojia, mofolojia, sintaksia na semantiki. Hata hivyo, kuna kazi chache mno za Kiswahili ambazo zimejikita katika mada na fokasi. Ashton (1947) ameshughulikia kiimbo katika aina mbalimbali za sentensi za Kiswahili huku akiegemea

zaidi katika sifa za kiarudhi ambazo hutumika kutambulisha mada na fokasi. Vitale (1981) ameelezea kuhusu mipangilio maalum ya maneno ambayo hutambulisha fokasi au msisitizo. Augustine (2004) ameshughulikia muundo wa taarifa katika Kiswahili akiongozwa na mtazamo wa Lambrecht (1994) huku akitumia tungo za maswali na zenye kuhamisha mada au fokasi kushoto ili kutambua elementi za mada na fokasi. Miongoni mwa kazi ambazo zimefanywa katika lugha zingine ni kama vile za Karnerva (1990), Milanie (2007), Bresnan na Mchombo (1987), na wengineo.

Mada yetu ya utafiti, tofauti na tafiti tulizotaja hapo juu, imejumlisha uchanganuzi wa jinsi fokasi na mada hutambulishwa katika Kiswahili Sanifu. Pia imechunguza zaidi ikiwa mada na fokasi huweza kusimbwa kama kiima, kitenzi, yambwa au kama kipashio kingine katika Kiswahili.

Utafiti huu, kama tutakavyotaja, umetumia mtazamo wa Muundo wa Taarifa. Nadharia hii imetusaidia kutambua ni sehemu gani ya sentensi ambayo ni mada na ipi ni fokasi. Pia umetuongoza katika kutambua uhusiano uliopo kati ya mada na fokasi. Mtazamo wa Muundo wa Taarifa ni hali ya kusimba umuhimu wa uhusiano wa viambajengo vya kishazi, hasa nomino, na hutambuliwa kama uteuzi kati ya mpangilio wa vibadala vya kisintaksia. Athari ya mawasiliano ya muundo wa taarifa ni kuangaza vipengele fulani vya ujumbe wa kishazi na kukosa kuangaza vingine. Katika utafiti huu tumechunguza jinsi uchukulio na ujumlishaji huchangia katika utambulishaji wa taarifa inayojulikana pamoja na taarifa mpya.

Kama tulivyotaja hapo awali, tafiti kuhusu kutambulisha mada na fokasi zimefanywa katika lugha zingine lakini sio katika lugha ya Kiswahili Sanifu. Kazi hii ni jaribio la kutambua jinsi mada na fokasi husimbwa katika sentensi za Kiswahili Sanifu. Mada na fokasi ni vitambulishi vya taarifa inayojulikana au taarifa mpya katika usemi na ambavyo huzipa sehemu za sentensi: maneno, virai au vishazi msikiko/umaarufu. Jukumu muhimu la msikiko/umaarufu ni kutambulisha ujumbe mpya. Kwa mfano katika fokasi, tunaweza kutambulisha kiima kama ifuatavyo:

**4. a. <u>Kaole</u> alivunja dirisha.**

**b. Kuna mtu aliyevunja dirisha.**

**c. Ni Kaole.**

Katika **(4b)** ujumbe ambao umetolewa ni kuwa kuna mtu aliyevunja dirisha. Katika **(4c)** tunapata ujumbe mpya wa kuwa mtu aliyevunja dirisha ni *Kaole*.

Kwa hivyo inalekea kuwa fokasi huweza ikatambulishwa kwenye kiima katika Kiswahili Sanifu. Tumechunguza kama ruwaza hii inajitokeza katika viambajengo vingine katika sentensi ya Kiswahili Sanifu.

Kutokana na mfano tulioutoa hapo juu kuhusu fokasi, tumeweza kuchanganua zaidi tungo katika Kiswahili Sanifu ili kujibu swali la ikiwa kuna uhusiano kati ya mada na fokasi.

Kuna mada ya sentensi na mada ya diskosi. Tunaweza kubainisha tofauti kwa kutumia utungo ufuatao:

**5. Musa alikuwa amekodi nyumba nzuri na ya kifahari. Hakuwa tayari kuihama lakini hangeweza kuilipia kodi, unaona. Na jinsi ilivyokuwa na ua la kupendeza upande wa nyuma.**

Kutokana na mfano huu, tunapata kuwa mada ya diskosi inajitokeza katika sentensi ya kwanza: *Ni nyumba ya Musa*. Katika sentensi ya pili, mada mpya inatambulishwa kama mada ya sentensi kwa kutumia kiwakilishi **Ha-** katika kitenzi *hakuwa* (katika ukanushaji) lakini mada ya diskosi bado ni *nyumba ya Musa* na ndiyo sababu sentensi ya tatu inalingana vizuri na zile za mwanzo bila kutolewa maelezo. Katika diskosi kwa kawaida, baada ya kutanguliza taarifa inayojulikana, taarifa iliyotolewa hutambulishwa kwa kutumia mrejeosabiki katika sentensi zinazofuata.

Kwa upande mwingine, mada ya usemi hupewa uhai na muktadha wa mazingira ikiwemo mrejeosabiki na viwakilishi kwa kutumia leksimu zinazohusiana, leksimu zinazorudiwarudiwa, zote ambazo huleta mshikamano katika usemi unaozifanya ziwe zaidi ya mkusanyiko wa sentensi zinazohusiana. Mada ni sehemu ya kauli ambayo inazungumziwa, ambayo huwakilishwa na kiarifu. Mara tu mada inapotolewa, inakuwa ujumbe unaojulikana, yaani mambo ambayo tayari yamesemwa na kueleweka. Kwa mfano tunaweza kutambulisha mada ifuatavyo:

6. a. **Mtoto** mdogo alidungwa sindano na daktari.

   b. **Daktari** alimdunga mtoto mdogo sindano.

   c. **Mtoto mdogo,** daktari alimdunga sindano.

Mada pia hurejelewa kama dhamira huku kiarifu ambacho hutoa ujumbe juu ya mada kikirejelea kiima.

Lugha nyingi hutambulisha mada kupitia njia zifuatazo:

i. Kwa kuitambulisha kama kiima.

ii. Kwa kutumia kauli tendewa ili kugeuza yambwa kuwa kiima.

iii. Kwa kuhamisha mada mwanzoni mwa sentensi.

Utafiti huu umelenga kuchunguza kama hali hizi na nyingine nyingi huweza kutumika katika Kiswahili Sanifu ili kutambulisha mada na fokasi. Na katika uchanganuzi wetu tumeongozwa na nadharia ya Muundo wa Taarifa ili kuchunguza vitambulishi vya mada na fokasi.

## 1.3. Madhumuni ya Utafiti

Madhumuni ya utafiti huu ni:

i. Kuchunguza ikiwa kuna uhusiano kati ya mada na fokasi katika Kiswahili Sanifu.

ii. Kuchunguza utambulishaji wa mada na fokasi katika Kiswahili Sanifu.

iii. Kutathmini ikiwa mada na fokasi huweza kutambulishwa katika Kiswahili Sanifu kama kiima, kiarifu, yambwa, kijalizo, kirai, na kishazi, na

iv. Kutathmini kufanikiwa kwa Muundo wa Taarifa katika utambulishaji wa mada na fokasi katika Kiswahili Sanifu.

## 1.4 Nadharia Tete

Utafiti huu umeongozwa na nadharia tete zifuatazo:

i. Kuna uhusiano kati ya mada na fokasi katika sentensi za Kiswahili Sanifu.

ii. Kuna uwezekano wa kutambulisha mada na fokasi katika sentensi za Kiswahili Sanifu.

iii. Mada na fokasi huweza kutambulishwa kwenye vipashio vyote vya sentensi za Kiswahili Sanifu kama kiima, kiarifu, yambwa, kijalizo, kirai na kishazi, na

iv. Nadharia ya Muundo wa Taarifa inakidhi mahitaji yote katika uchunguzi wa kutambulisha mada na fokasi katika sentensi za Kiswahili Sanifu.

## 1.5 Sababu za Kuchagua Mada Hii

Tumechagua mada hii kwa sababu ni eneo la isimu ya Kiswahili ambalo halijafanyiwa utafiti kwa kina. Utambulishaji wa mada na fokasi ni eneo ambalo hutatiza sana katika jinsi ya kutofautisha ni ipi mada na ipi fokasi katika sentensi za Kiswahili. Nadharia ya Muundo wa Taarifa itafaa katika uchanganuzi huu. Mtazamo wa Muundo wa Taarifa ni hali ya kusimba umuhimu wa uhusiano wa viambajengo vya kishazi, hasa nomino, na hutambuliwa kama uteuzi kati ya mpangilio wa vibadala vya kisintaksia.

Tafiti zimefanywa na maelezo kutolewa kuhusu mada na fokasi katika lugha nyingine ambazo si za asili ya Kibantu na ambazo si ambishi. Kwa sababu hiyo, mapendekezo yaliyotolewa huenda yakakosa kutosheleza au kufanikisha matokeo katika lugha ya Kiswahili, na ndiyo sababu utafiti huu unakuwa wa kutegemewa katika utambulishaji wa

mada na fokasi katika Kiswahili Sanifu. Aidha utafiti huu utajikita katika uchanganuzi wa mada na fokasi katika riwaya ya Kiswahili hususan riwaya ya *Kuli* ya Adam Shafi. Pia tumetumia tungo kutoka Kiswahi Sanifu ambazo tumezalisha sisi wenyewe kutokana na uelewa wetu wa Kiswahili ili kufanikisha utafiti huu.

Utafiti huu una umuhimu katika mawasiliano kwa kuwa utachangia katika utambuzi wa taarifa mpya na taarifa inayojulikana katika muktadha maalum. Inakuwa ni muhimu katika mawasiliano kati ya msemaji na msikilizaji kwa kuwa msemaji hutumia uchukulio na ujumlishaji katika kuhusisha kinachosemwa wakati fulani na muktadha. Pia utafiti huu utachangia pakubwa kitaaluma kwani utatoa mwangaza kuhusu jinsi mada na fokasi hutambulishwa katika Kiswahili huku ukitoa changamoto zitakazochochea tafiti zaidi. Vilevile, utafiti huu utachangia katika ujifunzaji wa lugha katika somo la Kiswahili Sanifu.

Hali kadhalika, utafiti huu utakuwa mwongozo kwa wale watakaoazimia kufanya utafiti katika uwanja huu. Aidha utafiti huu utatoa mchango katika uratibishaji wa mipango ya mawasiliano hasa katika uandishi wa insha, ripoti, makala za semina, taarifa, kumbukumbu, hotuba, n.k. Huu ni uwanja ambao kwa kutumia muundo wa taarifa, mawasiliano hurahisishwa kwani wasikilizaji hutambua kwa urahisi kuhusu taarifa mpya na taarifa inayojulikana.

Matumizi ya aina mbalimbali za sentensi na tungo za Kiswahili za kauli mbalimbali zikiwemo tungo za mazungumzo miongoni mwa tungo zingine zimetumika katika

uchanganuzi huu. Kwa kuzitumia tumepata kategoria mbalimbali za maneno, virai na vishazi ambavyo vimetumika katika utambulishaji wa mada na fokasi.

## 1.6 Upeo na Mipaka

Utafiti huu umejikita katika lugha ya Kiswahili Sanifu. Tumetumia miundo mbalimbali ya sentensi za Kiswahili ili kutambua utokeaji wa mada na fokasi. Tumeteua maneno, virai na vishazi vya Kiswahili. Hali kadhalika, tumetathmini vipashio mbali mbali vya sentensi ili kubainisha jinsi mada na fokasi hutambulishwa kwavyo. Hatimaye, tumechunguza uhusiano na tofauti iliyopo kati ya mada na fokasi katika Kiswahili sanifu. Mtazamo wa Muundo wa Taarifa umetumika katika utafiti huu. Utafiti huu umeangazia mada na fokasi katika mkabala wa kiusemi na katika uchanganuzi wa data tumejikita katika kuchanganua senstensi na mazungumzo katika riwaya ya *Kuli*. Hii ni riwaya ya Kiswahili ambayo haijatumika katika uchanganuzi wa data ya aina hii. Mbali na kutumia data kutoka riwaya ya *Kuli*, tumezalisha sentensi kutoka Kiswahili Sanifu ambazo tumetumia katika uchanganuzi wetu ili kufanikisha utafiti wetu zaidi.

## 1.7 Uhalalishaji

Mada na fokasi ni mada ambazo hazijashughulikiwa na wengi hasa katika Kiswahili Sanifu. Kazi nyingi zilizofanywa katika sintaksia zimejikita katika uchanganuzi wa masuala ya kisarufi na kanuni zinazoiongoza sarufi ya Kiswahili. Katika utafiti huu tumetumia riwaya ya *Kuli* na sentensi ambazo tumezalisha kutoka Kiswahili Sanifu ili kutoa mchango wa kutambulisha mada na fokasi katika muktadha wa kiusemi. Riwaya ya *Kuli* haijafanyiwa utafiti wowote katika kiwango cha mada na fokasi na ndiyo sababu

tumeiteua kama msingi wa data yetu. Tumetumia miundo mbalimbali ya sentensi na miktadha ya mazungumzo kutoka kwenye riwaya hii na sentensi zingine ambazo tumezalisha wenyewe kutoka Kiswahili Sanifu ili zitumike katika uchanganuzi wa data.

Vipengele vya mada na fokasi vimechunguzwa ili kuonyesha jinsi muundo wa taarifa unavyojidhihirisha katika diskosi na katika uwasilishaji wa kazi ya riwaya. Tumechunguza ustadi wa mwandishi katika kuhamisha mada na fokasi katika utunzi wake. Nadharia ya muundo wa taarifa imetumika katika utafiti huu ili kubainisha uhusiano na tofauti iliyopo kati ya mada na fokasi.

## 1.8 Msingi wa Kinadharia

### 1.8.1 Mtazamo wa Muundo wa Taarifa

Crystal (1980:234) anaeleza kuwa *Taarifa* ni dhana inayotumiwa na wanaisimu kwa jumla kama istilahi ya taaluma ya takwimu. Katika matumizi yake ya kawaida, dhana hii hutumika na wanaisimu kadhaa kama msingi wa kuelezea muundo wa taarifa. Inadaiwa kuwa usemi au matamshi huweza kutazamwa kama jambo linalobeba muundo wa taarifa, huku ukisimba habari muhimu za elementi katika ujumbe ulio na vipashio vya taarifa vinavyoweza kutambulishwa.

Kipashio cha toni au viambajengo vinavyobeba wazo kamili huwakilisha kipashio cha taarifa, na mkazo hutambulisha fokasi ya taarifa. Sentensi nyingi huweza kuwa vipashio pweke vya taarifa, kwa mfano:

**7. a. Chakula kilicho tayari kipelekwe *sebuleni.***

Kwa kubadilisha mkazo kulingana na mtazamo huu, tutabadilisha idadi ya vipashio vya taarifa na kuwa:

**b. *Chakula* kilicho tayari / kipelekwe** *sebuleni*.

Katika **(7a)** kipashio cha taarifa ni kimoja na msisitizo upo kwenye kiambajengo cha mwisho, *sebuleni*, tofauti na **(7b)** ambapo msisitizo upo kwenye viambajengo viwili, *chakula* na *sebuleni*, na kuifanya kauli hii kuwa na vipashio viwili vya taarifa ambavyo vinabeba taarifa muhimu.

Hata kama kipashio kimoja cha toni kitabakia, kubadilisha hali ya toni huathiri muundo wa taarifa kama vile:

**c. *Chakula* kilicho tayari kipelekwe sebuleni (na sio chai).**

Tofauti na ilivyo katika usemi, maandishi huwa hayadhihirishi kipashio cha toni na maneno ambayo huwekewa mada na fokasi hupigiwa mstari chini. Kwa kutumia mtazamo wa muundo wa taarifa kipashio cha taarifa hutambulishwa, iwe ni taarifa mpya au taarifa inayojulikana.

Foley (1996:200-209) anaeleza kuwa muundo wa taarifa ni hali ya kusimba umuhimu wa uhusiano wa viambajengo vya kishazi, hasa viwakilishi, na hutambuliwa katika mpangilio wa vibadala vya kisintaksia. Muundo wa taarifa wa kishazi mahsusi hubainishwa na sentensi kuu au usemi ambao ni sehemu yake (ya muktadha). Umuhimu wa kuwasiliana katika muundo wa taarifa ni kuangaza vipengele fulani vya ujumbe katika kishazi na kukosa kuangaza vingine. Umuhimu wa kusimba muundo wa taarifa huwa tofauti katika lugha mbalimbali za ulimwengu. Anaeleza kuwa kuna njia

mbalimbali zinazotumika katika kusimba muundo wa taarifa katika sentensi zikiwemo mada, fokasi, mpangilio wa maneno na matumizi ya mofimu mahsusi ambazo husimba uamilifu wa muundo wa taarifa wa kiwakilishi ambacho huwakilishwa katika kitenzi kwa kutumia viambishi.

Brown na Yule (1983:153) wanaeleza kuwa utafiti wa kina kuhusu Muundo wa Taarifa katika tungo uliasisiwa na wanataaluma wa Shule ya Prague kabla ya Vita Vikuu vya Pili vya Dunia. Walishughulikia Nguvu ya Mawasiliano ya elementi zinazounda sentensi katika mfumo wa 'mtazamo wa uamilifu' wa sentensi. Kazi nyingi zilizokuzwa za wafuasi wa Prague ziliwekwa wazi na wanataaluma wa kimagharibi kwa mara ya kwanza. Halliday (1967) alitoa ufafanuzi wa kukuza vipengele vya kazi za wafuasi wa Prague ambavyo vilikuwa na uhusiano wa moja kwa moja na welekeo kwenye miundo ya matini. Halliday alitumia mtazamo wa Prague wa taarifa zinazojumlisha kategoria zifuatazo:

i. Taarifa mpya ambayo mzungumzaji anaamini kuwa haijulikani na msikilizaji.

ii. Taarifa inayojulikana ambayo msemaji anaamini kuwa inajulikana na msikilizaji (ama kuwa taarifa hiyo iko kwenye muktadha au kuwa tayari imetajwa katika diskosi).

Halliday aliunga mkono wafuasi wa Prague kwa kusema kuwa uamilifu wa mkazo katika lugha ni kutambulisha ni taarifa ipi msemaji anachukulia kuwa mpya na ni taarifa ipi anachukulia kuwa inajulikana. Katika utafiti wake kuhusu muundo wa taarifa, Halliday alishughulikia mpangilio wa taarifa katika lugha ya Kiingereza na kuhusisha mpangilio

huo na utambuzi wa kifonolojia hasa kwenye kiimbo. Hivi karibuni, wasomi wengi wametoa ufafanuzi zaidi kuhusiana na mjadala wa taarifa inayojulikana na taarifa mpya katika hatua ya miundo ya kisintaksia ambayo huchukuliwa kudhihirisha kategoria hizi za taarifa.

Lambrecht (1994:6) anaeleza kuwa muundo wa taarifa huhusu uchanganuzi wa seti nne za kategoria ambazo hujisimamia lakini huhusiana, nazo ni:

i. Taarifa ya kauli ikijumlisha uchukulio wa kipragmatiki na dai la kipragmatiki. Haya huhusisha machukulio ya msemaji kuhusu hali ya ufahamu ya msikilizaji na utambuzi wake wakati wa matamshi.

ii. Utambuzi na uchochezi ambavyo huhusu machukulio ya msemaji kuhusu hali ya taswira ya virejelewa vya lugha katika uelewa wa msikilizaji wakati wa matamshi na mabadiliko thabiti ambayo taswira hizi hupitia wakati wa mazungumzo.

iii. Mada inayohusu mahusiano ya kipragmatiki yaliyopo kati ya virejelewa vya usemi na kauli katika muktadha wa diskosi iliyopo.

iv. Fokasi ambayo ni elementi katika kauli ya kipragmatiki pale ambapo mada hutofautiana na uchukulio na ambayo huyafanya matamshi ya sentensi kuwa arifu.

Kila mojawapo ya kategoria hizi huelekea kuhusiana moja kwa moja na sifa za kimuundo katika sentensi.

Lambrecht (1994:6) anaeleza kuwa muundo wa taarifa huhusu matamshi yanayohusu hali chukulizi za utambuzi za wasemaji na wasikilizaji. Muundo wa taarifa ni kile kiambajengo cha sarufi ambacho kauli kama taswira za utambuzi huwekwa pamoja na miundo ya maneno katika sarufi kwa mujibu wa hali za utambuzi za washiriki wanaotumia na kufasiri miundo hii kama vipashio fulani vya diskosi.

Muundo wa taarifa wa sentensi ni dhihirisho rasmi la muundo wa kipragmatiki katika diskosi. Kategoria muhimu katika diskosi ni:

i. Uchukulio na dai.

ii. Utambuzi na uchochezi. na

iii. Mada na fokasi.

UNIVERSITY OF NAIROBI
EAST AFRICANA COLLECTION

Muundo wa taarifa kwa kawaida hujidhihirisha katika:

i. Hali za kiarudhi kama vile mkazo.

ii. Vitambulishi maalum vya kisarufi kama vile kiima. kiarifu. kijalizo. na yambwa.

iii. Maumbo ya kisarufi (hasa viambajengo vya viwakilishi).

iv. Nafasi na mpangilio wa viambajengo vya sentensi.

v. Maumbo ya tungo changamani za kisarufi.

vi. Teuzi fulani kati ya vipashio vya kileksika vinavyohusiana.

Muundo wa taarifa huingilia kati katika hatua zote za kutoa maana katika mfumo wa sarufi. Huwa umejikita kwenye ulinganuzi wa seti za sentensi zenye ulinganuzi wa kisemantiki lakini kwa kawaida katika sentensi zenye tofauti za kipragmatiki kama vile:

i. Kauli tendwa dhidi ya kauli tendewa

ii. Sentensi zenye kufuata kanuni za kisarufi dhidi ya zenye mada.

iii. Sentensi zenye kufuata kanuni za kisarufi dhidi ya zenye kuhamisha mada au fokasi kushoto.

iv. Sentensi zenye kuweka mkazo kwenye kiima dhidi ya zenye mkazo kwenye kiarifu, n.k.

Van Valin na La Polla (1997:199) wakimnukuu Lambrecht (1994) wanaeleza kuhusu muundo wa taarifa kama mahusiano ya kipragmatiki kati ya virejelewa vya sentensi. Muundo wa taarifa hudhihirisha jinsi lugha tofauti zinavyotumia sintaksia, mofolojia na mkazo ili kusimba miundo tofauti ya fokasi: fokasi kwenye kiarifu, fokasi kwenye sentensi na fokasi finyu. Mtazamo wa Lambrecht ni wa kutumia tungo za sentensi na kuhamisha kushoto ili kubainisha elementi za mada na fokasi. Mada zilizotambulishwa huweza kutangulizwa mwanzoni mwa sentensi, kuwekewa kidatu na sauti nzito, mtuo, viwakilishi vyenye mkazo, na msisitizo wa vitenzi vishirikishi, na kadhalika. Tungo zinazotambulisha fokasi huwa ni pamoja na kuhamisha kushoto, matumizi ya mkazo, msisitizo wa vitenzi vishirikishi, na maneno mengine ambayo hupewa fokasi.

Lyons (1968) anatoa wazo kuwa muundo wa taarifa unahusu jumla ya taarifa inayobebwa na kipashio cha kiisimu katika muktadha fulani, na hili huamuliwa na idadi ya utokeaji wake katika muktadha. Taarifa inayobebwa na kipashio fulani hufafanuliwa kama uamilifu wa welekeo wake, kwa mfano, ikiwa vipashio viwili au zaidi vina welekeo

sambamba katika muktadha fulani, basi huwa vinabeba yaliyomo kwenye taarifa katika muktadha huo.

Brown na Yule (1983:155) wanaeleza kuwa mtazamo wa muundo wa taarifa hulenga vipashio vidogo vya muundo wa usemi, vipashio vidogo katika kiwango cha kirai au kishazi. Wanazingatia jinsi taarifa inavyowekwa pamoja kwenye miundo midogo na hasa nyenzo ambazo wazungumzaji na waandishi wanatumia katika kuwaelekezea hadhira lengwa hadhi ya taarifa ambayo inatambulishwa kwenye usemi/diskosi.

## 1.8.2. Umuhimu wa Mtazamo wa Muundo wa Taarifa Katika Sarufi

Lambrecht (1994) anaeleza kuwa wanaisimu wengi walioshughulikia muundo wa taarifa na hadhi yake katika mfumo kamili wa sarufi huufafanua kama wenye hatua tatu. Lambrecht amewanukuu wanaisimu hawa wa Shule ya Prague; Mathesus, Firbas, Benes na Vachek katika kazi ya Danes (1966), wanaobainisha hatua hizi tatu;

i. Hatua ya muundo wa kisarufi katika sentensi,

ii. Hatua ya muundo wa kisemantiki katika sentensi, na

iii. Hatua ya mpangilio wa matamshi katika sentensi.

Kulingana na Danes, Halliday na Dik, mawanda ya kawaida ya muundo wa taarifa (mtazamo wa sentensi amilifu, maudhui/dhamira, uamilifu wa kipragmatiki) huwa ni sentensi au kishazi. Kwa mfano, muundo wa taarifa huelekezwa kwenye sarufi ya sentensi fulani. Unahusu mpangilio wa maneno katika sentensi na mpangilio wa sentensi katika diskosi. Muundo wa taarifa hutoa msisitizo kuhusu mwingiliano wa sentensi na

miktadha yake. Swali la kimsingi ni kuwa, kwa nini kuwepo miundo tofauti tofauti ya sentensi? Miundo hii ya sentensi ndiyo hutuongoza katika utambuaji wa ni sehemu gani ya sentensi ambayo inabeba taarifa mpya au ni gani inayobeba taarifa inayojulikana. Uchanganuzi wa mahusiano kati ya sentensi na diskosi kwa kawaida huwa wa kiuamilifu zaidi ya ulivyo wa kawaida.

## 1.9. Yaliyoandikwa Kuhusu Mada ya Utafiti

Aissen (1992) ameshughulikia mada na fokasi katika Mayan. Anaeleza kuwa lugha nyingi za Mayan kimsingi hutanguliza kiarifu lakini virai mbalimbali hutokea kabla ya kiarifu wakati vinapowekewa mada na fokasi. Kazi yake imejikita katika msingi wa kinadharia ulioasisiwa na Chomsky (1986) wa Uchanganuzi Miundo Virai ili kuchanganua mada na fokasi katika lugha tatu za Mayan. Amejikita katika virai vya kiimbo na ithibati ya kisintaksia inaunga mkono tofauti za miundo virai zinazoanzishwa na misingi ya kiarudhi. Utafiti wake umekuwa motisha kwetu katika kuchunguza utambulishaji wa mada na fokasi katika Kiswahili Sanifu huku tukijikita kwenye sintaksia yake na kujikita katika uchanganuzi kiusemi.

Muller-Gotama (1996) amechunguza mada na fokasi katika Sundanese. Amejikita katika uchanganuzi wa jinsi taarifa hushughulikiwa kisarufi katika Sundanese. Ametumia data kutoka makala mbalimbali na pia kuzalisha mifano yake mwenyewe. Ameonyesha kuwa Sundanese hutumia faridipeke: *mah*, *teh* na *tea* katika kutambulisha taarifa mpya, taarifa inayojulikana na taarifa inayotumiwa upya, mtawalia. Kutokana na utafiti wake tutapata vigezo vya kimsingi kama vile virai, virai na tungo amilifu ambavyo tutatumia katika

uchanganuzi wa data katika Kiswahili Sanifu. Pia tutapata dhana muhimu zinazorejelewa katika muundo wa taarifa na ambazo hutumika katika utambulishaji wa mada na fokasi katika Kiswahili Sanifu.

Sornicola (1996), ameandika kuhusu mada, fokasi na mpangilio wa maneno. Ameshughulikia asili ya mpangilio wa maneno katika lugha ambao huwa thabiti/funge katika lugha zingine kama Kiingereza na huru kwa kiasi katika lugha zingine kama Kiswahili. Ametoa fafanuzi kuhusu dhana za mada na fokasi, maelezo kuhusu miundo inayohusiana na mada na kuchangia katika kuelezea mikakati ya kisintaksia inayoweka fokasi katika nafasi isiyotambuliwa. Utafiti huu utatuongoza katika uchanganuzi wa data kwa kuwa utambulishaji wa mada na fokasi katika Kiswahili Sanifu hutegemea kwa kiasi kikubwa mpangilio wa maneno katika sentensi.

Givon (2001) ameshughulikia tungo zenye fokasi linganuzi na pia tungo zenye kutambulisha mada huku akitumia mifano ya sentensi kutoka lugha mbalimbali. Anaeleza kuwa fokasi linganuzi huingiliana na mawanda mengine ya kisarufi na mbinu za ulinganuzi huingiliana na mada. Kutokana na kazi yake, tutapata vigezo muhimu vya kutumia katika uchanganuzi wa data katika utambulishaji wa mada na fokasi katika Kiswahili Sanifu.

Cruttenden (1986) ameelezea kuhusu taarifa inayojulikana na taarifa mpya katika sentensi mbalimbali na pia ameshughulikia fokasi linganuzi. Maelezo yake yatachangia sana katika utafiti huu.

Hofmann (1993) ameandika kuhusu vitambulishi vya balagha kama vile vibainishi, vitambulishi vya mada na vitambulishi vya fokasi. Kiswahili ni lugha ambayo haitumii vibainishi lakini vitambulishi vya mada na fokasi vitachangia katika utafiti wetu.

Saeed (1997) ameelezea kuhusu dhana za mada na fokasi na jinsi zinavyotumika katika utambulishaji wa taarifa mpya na taarifa inayojulikana. Maelezo yake kuhusu dhana za mada na fokasi yatatuongoza katika utafiti huu.

Carlos (2008) ameandika kuhusu aina za fokasi katika lugha ya Kiingereza na akaeleza kuwa sababu ya kutumia kidatu cha kiini toni katika ufafanuzi wa muundo wa taarifa katika lugha ni kutokana na vikwazo vya kimuundo. Pia anaeleza kuwa hakuna ulinganuzi wowote wa kisemantiki kati ya taarifa mpya na taarifa inayojulikana, kuwa lugha hufafanua aina mbalimbali za maana ya fokasi kama vile fokasi ya kutambulisha upya, fokasi isiyotarajiwa na fokasi sahihishi. Japo kazi yake ina mchango mkubwa, haijazingatia lugha ya Kiswhili Sanifu ambayo ndiyo msingi wa utafiti huu.

Cobuild (1990) ameshughulikia muundo wa taarifa akijikita katika nafasi ya elementi za muundo wa kishazi ambao kwa kawaida hufuata kiima, kitenzi, kiarifu, yambwa, kijalizo na chagizo. Kiima hutangulia na ndicho huzungumziwa katika sentensi. Mchango wake hata kama umejikita katika Kiingereza utatupa vigezo vya kutumia katika utambulishaji wa mada na fokasi katika Kiswahili Sanifu.

Kanerva (1990) ametoa mchango wake katika utafiti kuhusu fokasi kwenye virai vya kifonolojia ambavyo ni vidogo na hutokea katika sintaksia katika lugha ya Chichewa. Utafiti wake umejikita zaidi katika hatua mbili; kirai cha kiimbo na kirai cha kifonolojia. Amependekeza kuwa kazi zaidi katika lugha zingine zinaweza kufanywa ili kutambua athari ya fokasi kwenye maumbo katika mawanda ya kiarudhi na uwezekano wa hatua ya mfumo wa kiarudhi unaotokea kati ya kirai cha kifonolojia na kirai cha kiimbo. Kazi yake imejikita katika fonolojia tofauti na kazi yetu ambayo imejikita kwenye sintaksia. Hata hivyo ina mchango katika utafiti huu kwa kuwa itachangia kwa kutuangazia mambo muhimu yanayohusiana na virai katika sintaksia.

Utafiti wake pia unaeleza kuwa vigezo muhimu vya mabadiliko na mageuzo huwa kwenye umbo la nje: miundo ya nje iliyofasiriwa kifonolojia, ya kimofolojia na ya vishazi. Amejikita katika miundo ya nje kwa kuwa ndiyo ambayo hutambulikana katika maandishi. Kazi yake itatoa mchango katika utafiti huu kwa kuwa hata kama inatofautiana na Kiswahili kwenye ukubalifu wa kiarifu unaopatikana katika viulizi, zote ni lugha za Kibantu. Pia itatuongoza katika uchanganuzi wa data ili kutambulisha jinsi mada na fokasi hutegemea mpangilio wa maneno.

Mchombo (1980) alichunguza mada, kiwakilishi na upatanifu katika Chichewa. Anaeleza kuwa Chichewa huwa na ukubalifu wa kisarufi na kiima, na ukubalifu wa mrejeosabiki na kiarifu na lugha zingine za Kibantu huonyesha migawanyo tofauti ya ukubalifu huu. Katika uchanganuzi wake, anaeleza kuwa lugha nyingi za Kibantu hutofautiana na Chichewa katika kuweka mada ikitangulia mwanzoni kama kiima katika kishazi. Viulizi

haviwezi kuwa mada na hivyo katika maswali yasiyohamisha kushoto, swali kuhusu kiima huwezekana wakati kiima kinapopakana au kinapofuatana na kirai tenzi. Kazi yake itatoa mchango katika utafiti huu kwa kuwa, mbali na tofauti zilizopo, ni lugha ya Kibantu. Aidha, tutatumia matokeo yake ili kutathmini ikiwa viulizi huweza kutambulisha mada katika Kiswahili Sanifu.

Maw (1976) alishughulikia fokasi na mofolojia ya kitenzi cha Kiswahili. Alieleza kuwa dhana kama vile mtazamo wa sentensi amilifu, fokasi, mada-kina, mada-kiarifu, taarifa inayojulikana na taarifa mpya ni dhana ambazo kwa kiasi au kwa wingi zimekubalika kama nyenzo muhimu katika ufafanuzi wa lugha mahususi au sehemu ya lugha. Kwa kuwa alijikita katika lugha ya Kiswahili, tutatumia mchango wake katika kujaza pengo la uchanganuzi wa mada na fokasi katika Kiswahili Sanifu.

Augustine (2004) katika utafiti wake kuhusu mada na fokasi katika Kiswahili alitoa ufafanuzi wa muundo wa taarifa katika Kiswahili akiongozwa na mtazamo wa Lambrecht. Alitumia tungo za maswali na za kuhamisha kushoto ili kutambua elementi za mada na fokasi. Alipendekeza kuwa mada zisizotambulishwa huweza kutambuliwa kwa kuzitanguliza mwanzoni mwa sentensi kwa kutumia kidatu cha juu, mipumuo, viwakilishi vyenye mkazo, na matumizi ya kitenzi kishirikishi ***ndi-***. Tungo zinazotambulisha fokasi ni pamoja na zenye kuhamisha kushoto, zenye kutumia kiimbo maluum, zenye kutumia kitenzi kishirikishi ***ndi-*** na maneno mengine yenye kutoa fokasi. Kazi yake ingawa itachangia katika utafiti huu, imetoa tu kiasi cha miundo inayotumika katika kutambulisha mada na fokasi katika Kiswahili. Utafiti wetu utajaza pengo la kazi

yake kwa kujikita katika muktadha wa diskosi tutakapotumia miundo mbalimbali ya sentensi.

Ashton (1947) ameshughulikia kiimbo katika aina mbalimbali za sentensi za Kiswahili Sanifu. Ameegemea zaidi katika sifa za kiarudhi kama vile msisitizo na mkazo ambazo hutumika katika kutambulisha mada na fokasi. Amejikita tu kwenye mfumo wa kimsingi wa kiimbo katika Kiswahili Sanifu. Kazi yake itakuwa na mchango mkubwa sana katika utafiti wetu kwa kuwa dhana za kiarudhi kama vile mkazo na msisitizo vitatumika. Dhana hizi zitafaa sana hasa katika uchanganuzi wa data ya dayolojia ili kutambulisha ni kiambajengo gani katika sentensi ni mada na kipi ni fokasi.

Vitale (1981) ameelezea kuhusu mpangilio maalum wa maneno ambao hutambulisha fokasi au msisitizo katika Kiswahili Sanifu. Kazi yake ilishughulikia sintaksia na vipengele vingine ambavyo huwa na uhusiano na mofolojia ya Kiswahili Sanifu. Pia ameshughulikia mpangilio wa maneno ambao katika Kiswahili Sanifu huwa huru kwa kiasi kutokana na sifa za kiarudhi kama vile msisitizo na pia ubainifu wa aina ya taarifa (mpya au inayojulikana) inayobebwa katika kishazi. Kutokana na kazi yake tutakuwa na msingi wa kuchanganulia data yetu huku tukiegemea kwenye mpangilio wa maneno ili kubainisha ni kwa jinsi gani taarifa mpya na taarifa inayojulikana husimbwa katika maneno, virai au vishazi vya Kiswahili Sanifu.

Kazi ambazo tumetaja zitachangia pakubwa katika kufanikisha utafiti huu kwa kuwa zitakuwa msingi wa kazi yetu. Vilevile zitaturahisishia kazi katika kuelewa dhana muhimu zinazohusiana na mada na fokasi na katika utambuzi wa msingi wa kinadharia.

## 1.10 Mbinu za utafiti

### 1.10.1 Ukusanyaji Data

Kimsingi utafiti huu umekuwa wa maktabani. Tumedurusu vitabu na kazi zingine ambazo zimeandikwa kuhusiana na mada hii. Tumesoma vitabu mbalimbali kuhusiana na dhana na kaida za mada na fokasi. Kwa njia hii, tumeweza kupata mwelekeo na msingi imara wa kinadharia ambao umetuwezesha kuchanganua kazi hii.

Pia, tumekisoma kitabu cha riwaya ya Kiswahili hususan *Kuli* cha Adam Shafi. Riwaya hii imetusaidia katika kutoa baadhi ya mifano ili kuonyesha utambulishaji wa mada na fokasi katika Kiswahili Sanifu. Data zaidi imetolewa kutoka makala mbalimbali za Kiswahili na nyingine zaidi tumeizalisha ili kukidhi mahitaji yetu katika uchanganuzi wa data. Kutokana na data hii tumefanya uchanganuzi ili kubainisha ikiwa mada na fokasi hutambulishwa katika Kiswahili Sanifu.

Aidha, tumetumia mtandao ili kupata data zaidi kutoka kwenye majarida yaliyoandikwa kuhusiana na mada ya utafiti na msingi wa kinadharia ambayo yamechangia katika utafiti wetu. Kadhalika tumezungumza na wataalamu miongoni mwao wakiwa wahadhiri katika Chuo Kikuu cha Nairobi na vyuo vingine, ambao wametupa ushauri na maarifa zaidi kuhusu jinsi ya kulikabili tatizo letu la utafiti.

### 1.10.2 Uchanganuzi wa Data

Tumechagua miundo mbalimbali ya sentensi za Kiswahili kwa kutumia sampuli lengwa ili kupata data inayofaa na itakayokidhi mahitaji yetu katika uchanganuzi wa data. Tumechanganua miundo mbalimbali ya sentensi na kuonyesha kwa kutolea maelezo utambulishaji wa fokasi na mada katika sentensi za Kiswahili Sanifu. Tumechanganua data kwa kuchukua mafungu mbalimbali ya matini husika kama vile mazungumzo au dayalojia na pia kauli zinazojisimamia. Tumetoa maelezo kamili kuhusiana na jinsi mada na fokasi huweza kutambulishwa katika tungo huku tukijikita kwenye mtazamo wa muundo wa taarifa. Kutokana na data yetu, tumeweza kubainisha vipashio mbalimbali vya taarifa na kutofautisha ni kipashio kipi kinachobeba taarifa mpya na ni kipi kinachobeba taarifa inayojulikana. Hatujatumia takwimu zozote katika utafiti huu.

# SURA YA PILI

# MADA, FOKASI, MUUNDO WA TAARIFA, UMBO LA KISINTAKSIA, MUUNDO WA SENTENSI NA UAINISHAJI WA HADHI YA TAARIFA

## 2.1 Utangulizi

Katika sura hii tutashughulikia maswala ya kimsingi yenye uhusiano na mada, fokasi na msingi wa kinadharia wa muundo wa taarifa. Utata ambao hutokana na uelewa wa nadharia ya muundo wa taarifa hutokana na uwazi kuwa uchanganuzi wa kisarufi hapa hushughulikia mahusiano kati ya umbo la kiisimu na hali za utambuzi za wasemaji na wazungumzaji na kuwa wanaisimu wanaoshughulikia muundo wa taarifa inawabidi kwa pamoja kushughulikia vipengele vya kawaida na vya mawasiliano vya lugha. Katika sura hii tutajikita katika hali ya muktadha wa diskosi ambapo vipengele vya taarifa yenye uchukulio na dai hutolewa kupitia njia za kisintaksia, kisemantiki na kipragmatiki. Mifano mbalimbali itatolewa kutoka kwenye makala mbalimbali ili kufafanua maswala husika.

## 2.2 Mada

Crystal (1980:468) anafafanua dhana ya mada kama istilahi inayotumika katika semantiki na lugha kama sehemu ya sifa jozi badala ya muundo wa sentensi, kama ilivyo katika muundo wa sarufi mapokeo wa kiima-kiarifu. Mada ya sentensi ni ukamilifu kuhusu kile

kinachozungumziwa, nayo maelezo zaidi yanayotolewa kuhusu ukamilifu huo ndicho kiarifu. Umuhimu wa tofauti hii ni kuwa unawezesha utoaji wa taarifa ya jumla kuhusu mahusiano kati ya sentensi ambazo tofauti kati ya kiima-kiarifu hukosa kueleweka. Mada katika kiwango cha sentensi hulingana na kiima cha sentensi kama vile:

**8. Mgeni** ***anabisha mlangoni.***

*Mgeni* ni kiima cha kauli hii na hivyo basi huchukuliwa kuwa ndicho kiambajengo kinachotambulisha mada. Kauli hii si lazima iwe kama vile:

**9. Ndiye yule mgeni aliyebisha mlango.**

Na hata kama ni kiima sio lazima kitangulie mwanzoni mwa sentensi na huweza kutolewa kwa kubadilisha mpangilio wa maneno kama vile:

**10. Maria ni jina langu**

Katika kauli hii, kiima kimehamishwa na kutokea mwishoni mwa kauli huku bado kikitumiwa kutambulisha mada ya sentensi hiyo. Hali kama hii hurejelewa kama kiima cha kisaikolojia.

Lugha zingine hutanguliza mada ya sentensi kwa kutumia vishirikishi (kama Kijapani, Kisamoa, n.k.). Ukinzani kati ya mada/ kiarifu hata hivyo huwa vigumu kuthibitisha, tukizingatia athari za kiimbo na katika sentensi nyingi, uchanganuzi huwa vigumu, kama vile katika sentensi agizi na za maswali. Utambulishaji wa mada hudhihirika wakati kiambajengo kinapohamishwa kushoto na kuchukua nafasi ya kwanza katika sentensi na kuwa na uamilifu wa mada.

Halliday (1967) anaeleza kuwa katika isimu mada au dhamira ni ile sehemu ya kauli inayoarifiwa katika usemi (kiarifu). Inapoelezwa, mada inakuwa ujumbe unaojulikana au mambo ambayo tayari yamesemwa na kueleweka, kama vile:

**11. a. <u>Mbwa</u> alimuuma mtoto mdogo.**

**b. <u>Mtoto mdogo</u> mbwa alimuuma.**

**c. <u>Mtoto mdogo,</u> alimuuma mbwa.**

## 2.2.1 Mada ya Sentensi na Mada ya Diskosi

Tofauti huweza kutolewa kati ya mada ya sentensi na mada ya diskosi. Hocket (1958) katika Brown na Yule (1983:70-71) anaeleza kuwa tofauti inaweza kutolewa kati ya mada ya kiarifu katika sentensi hivi kwamba msemaji hutangaza mada na kisha kuielezea katika lugha zingine. Mada kwa kawaida huwa pia ni kiima, na kiarifu hukamilisha kiima. Mada ya sentensi hulingana na kiima kinachotoa habari kuhusu kiarifu, kama vile:

| | |
|---|---|
| **12. <u>Kazi</u>** | **<u>haijambo kidogo.</u>** |
| **Kiima** | **kiarifu** |

Dhana ya mada kama inavyotumiwa katika ufafanuzi wa muundo wa sentensi ni dhana inayotambulisha kiambajengo mahususi cha sentensi. Mada ya sentensi kwa kawaida hubebwa na msemaji wala sio na sentensi. Kuhusu mada ya diskosi, Keennan na Schieffenlin (1976), wanatofautisha mada ya sentensi na mada ya diskosi kwa kusema kuwa mada ya diskosi sio kishazi nomino, lakini kauli ambayo kwayo madai fulani hutolewa au hushawishiwa. Wanaelekea kubadilisha dhana ya kishazi nomino kimoja sahili na kuelezea mada kama dhana ya kishazi au sentensi moja sahili. Wanachokisema katika utafiti wao ni kuwa lazima pawe kauli moja (kishazi au sentensi sahili) katika kila

kifungu cha diskosi ya mazungumzo kinachosimamia mada ya diskosi ya kifungu kizima. Hata hivyo, mada ya diskosi kwa kawaida hutegemea mada ya sentensi kwa kuwa sentensi au vishazi vingi kwa pamoja ndivyo huleta muktadha wa kiusemi.

## 2.3 Fokasi

Crystal (1980:183) anafafanua dhana hii kama inavyotumiwa na wanaisimu wengi katika ulinganuzi wa sentensi na ambao hutofautisha kati ya taarifa inayodhaniwa na wasemaji na ile ambayo ni kiini (au fokasi) cha msingi wa mazungumzo yao. Fokasi kulingana na mtazamo huu ni kinyume cha uchukulio, kama vile.

**13. Ni <u>Maria</u> aliyempiga mtoto.**

**Maria** ndiye fokasi na kwa kutumia umbo la kiimbo, fokasi itatambulikana kwa urahisi. Kwa kuzingatia uchukulio, swali ambalo litatoa jibu la sentensi hii litakuwa. '**Nani alimpiga mtoto?** badala ya, **Maria alifanya nini?**

Halliday (1967:199-244) anafasiri fokasi kama dhana inayotumika katika nadharia ya isimu na ambayo inajishughulisha na jinsi taarifa katika kishazi kimoja huhusiana na taarifa iliyoitangulia. Kihistoria, fokasi imekuwa na mitazamo miwili: wa kiuzalishaji na wa kiuamilifu. Mtazamo wa kiuzalishaji hutumiwa kueleza maneno au maelezo ambayo huwa na sifa za kiarudhi au za kisintaksia kwa kijumla kwa sababu hutoa taarifa mpya. Mtazamo wa kiuamilifu hutumiwa kuelezea maneno au maelezo yanayoasisi muambatano katika matini au mazungumzo.

### 2.3.1 Uamilifu wa Fokasi Linganuzi

Fokasi linganuzi hubeba ukadirio, matarajio na ulinganuzi wa vipengele mbalimbali vya sentensi. Vishazi tenzi huweza kubeba vipande vya taarifa kila kimoja kikiwa na kiwango tofauti cha ukadirio. Vipande vingine hudhaniwa kuwa vinatambulikana na msikilizaji kama vitajwa bainifu au kama taarifa yenye uchukulio. Vipande vingine huwa havitambuliki kama vitajwa visobainifu au kama taarifa inayodaiwa. Lakini ukadirio wa taarifa huwa haubadilishani na ubainifu au uchukulio bali hutegemea muktadha wa mazungumzo ambao taarifa hupitishwa katika muktadha unaofaa. Vipande vya taarifa inayotambulikana huweza kutokadiriwa na kuwa linganuzi na kipande cha taarifa mpya huweza kukadiriwa na kuwa linganuzi. Kipande cha taarifa mpya huweza kukadiriwa na kuwa bila ulinganuzi kama vile:

**14. a.Ali aliniazima baisikeli.**

**b. <u>Ali</u> ndiye aliyeniazima baisikeli (si Hassani).**

**c. <u>Ni baisikeli</u> ambayo niliazimwa na Ali (sio gari).**

Kiima bainifu au ambacho si bainifu katika **(14a)** huweza kuwekewa fokasi linganuzi kama ilivyo katika (**14b)** na (**14c**). Ubainifu au kutotambulikana sio masiala bainifu ya kuweka vipengele vya taarifa chini ya fokasi linganuzi (Chafe 1976) na kuwa katika **(14c)** neno *'baisikeli'* liko katika mawanda ya uchukulio.

## 2.4 Mada, Fokasi na Mpangilio wa Maneno

Mpangilio wa maneno umekuwa ukihusishwa na sarufi na mtindo. Katika sarufi, mpangilio wa maneno ni chombo cha kusimba mahusiano ya kisarufi, matokeo yakiwa

mpangilio wa maneno wa kimsingi katika lugha. Mpangilio wa maneno kama jambo la kipragmatiki. hujumlisha ulinganuzi kutokana na ruwaza ambazo ni za sifa za kipragmatiki kama vile uhamishaji na utambulishaji wa mada na fokasi.

Dhana hizi mbili za mada na fokasi hushughulikia mambo yanayohusiana na sintaksia. semantiki na pragmatiki huku fonolojia ikishirikishwa. Mada hurejelea taarifa ambayo inapatikana katika muktadha wa kiisimu au muktadha wa kihali. Fokasi hurejelea taarifa ambayo haijatolewa au ambayo imetolewa kwa uchache sana katika muktadha wa kiisimu au wa kihali. Dhana hizi ni linganuzi kwa kuwa taarifa inayojulikana ndiyo mada na ile taarifa mpya ndiyo fokasi. kama vile:

| | | |
|---|---|---|
| **15. a. Ni mvulana anayempakata paka** | **Inayojulikana:** | **X anampakata paka** |
| | **Mpya :** | **X ni <u>mvulana.</u>** |
| **b. Ni paka anayepakatwa na mvulana.** | **Inayojulikana:** | **Mvulana anampakata X.** |
| | **Mpya :** | **X ni <u>paka</u>** |

Mada ni sehemu ya sentensi ambayo hubeba hadhi ya chini kabisa ya uwezo wa mawasiliano. nayo fokasi au kina ni sehemu ambayo hubeba hadhi ya juu kabisa ya uwezo wa mawasiliano. Mada ni taarifa yenye uchukulio nayo fokasi ni taarifa ambayo haina uchukulio. Mada humaanisha kile kinachozungumziwa nayo fokasi ni kile kinachosemwa kuhusu kile kinachozungumziwa. Tunapata kuwa katika mpangilio wa maneno sio lazima mada itangulie mwanzoni mwa sentensi kama vile:

**16. a. <u>Maria</u> alikuwa na hasira sana jana.**

**b. Jana <u>Maria</u> alikuwa na hasira sana.**

Katika **(16a)** Maria ndiye mada ya sentensi na neno hili linatokea mwanzoni mwa sentensi tofauti na ilivyo katika **(16b)** ambapo neno *jana* ni kielezi cha wakati na wala sio mada ilhali linatokea mwanzoni mwa kauli. Katika sentensi ambazo hazijatambulishwa, nafasi ya fokasi huja mwishoni, lakini huwa sio kawaida kwa sababu fokasi, tofauti na mada, hailingani na kiambajengo kimoja, lakini maumbo ya viambajengo. Kwa mfano katika **(16a)** hapo juu, kirai tenzi **alikuwa na hasira sana jana** ni fokasi ya sentensi hiyo.

Hadhi ya ukubalifu kati ya kanuni za muundo na kanuni za mpangilio za uteuzi wa fokasi huwa tofauti kutoka lugha moja hadi nyingine. Hili hutokana na sifa za uainishaji zinazoathiri sarufi kwa kiasi tofauti. Tukirejelea tathmini za uhusiano kati ya mpangilio wa maneno na fokasi, tunaweza kuhitimisha kuwa uhusiano huu umeathiriwa na sifa za uainishaji wa lugha. Ikiwa fokasi hulingana na uarifu, hali ambayo hutambuliwa katika hatua ya umbo la kirai tenzi, hakuna nafasi ya fokasi ambayo ni bia na fokasi huweza kuhama itokeze kama kiima, kiarifu, yambwa au kijalizo kama tulivyotaja hapo awali. Kama tulivyotaja awali, fokasi hurejelea taarifa ambayo haijatolewa kamwe katika diskosi au ambayo imetolewa kwa uchache mno katika muktadha wa kiisimu au kihali.

## 2.5 Vipashio vya Taarifa

Halliday (1967:199-244) anaeleza kuwa msemaji huwa na nia ya kusimba yanayobebwa na kishazi (kipashio cha kimsingi katika mfumo wa sarufi) kwa njia nyingi, kile anachokirejelea kama maudhui inayodhaniwa ya kishazi ambayo huweza kulinganishwa na kile wataalamu wengine hukiita maudhui ya kauli ya sentensi sahili. Maudhui ya kishazi hupangwa na msemaji ili kupata muundo wa kishazi wa kisintaksia, ambapo

msemaji huchagua kati ya dhamira alizo nazo. Katika lugha ya mazungumzo, yaliyomo katika kishazi hupangwa kwenye vipashio vya taarifa moja au zaidi ambavyo hutambulika na wa kifonolojia katika kiimbo.

Kulingana na Halliday (1967), msemaji hana budi kuweka usemi wake katika vipande vya vipashio vya taarifa. Inambidi kuwasilisha ujumbe wake kwenye mfululizo mmoja na hivyo kuwa na uhuru wa kuamua ni jinsi gani atakavyoipanga taarifa yake. Msemaji yuko huru kuamua ni wapi kila kipashio cha taarifa kinaanzia na kumalizikia na jinsi kinavyopangwa katika sentensi. Hivyo basi, msemaji akimwambia msikilizaji, **'Yohana ameenda shambani na Maria'**, msemaji anaweza kupanga taarifa hii na kuwa kipande kimoja kama vile:

**17. a. Yohana ameenda shambani na Maria.**

*au* kama vipande viwili:

**b. Yohana – ameenda shambani na Maria.**

*au* kama vipande vitatu:

**c. Yohana – ameenda shambani - na Maria.**

Mpangilio wa viambajengo vya sentensi unaobebwa na kipashio cha taarifa huhusiana na jinsi ambavyo taarifa inayojulikana na taarifa mpya inavyosambazwa katika kipashio kizima. Halliday anaeleza kuwa kwa kawaida msemaji atapanga taarifa inayojulikana kabla ya taarifa mpya. Mpangilio huu wa muundo wa taarifa usiotambulishwa huchukuliwa kuwa taarifa inayojulikana na taarifa mpya. Vipashio vya taarifa ambavyo hutangulia katika usemi kwa kawaida hubeba tu taarifa mpya.

## 2.6 Makundi ya Toni na Mkazo

Vipashio vya taarifa hutambuliwa moja kwa moja kwenye usemi kama makundi ya toni au kama makundi yenye kubeba taarifa kamili. Msemaji husambaza kiasi cha taarifa anayotaka kueleza kwa kutumia vipashio vya kifonolojia vilivyotangulizwa. Makundi ya toni hutambuliwa kifonolojia kuwa yanabeba silabi toni moja tu. Katika sentensi, makundi toni hubeba taarifa kamili ambayo inahusiana. Silabi toni hupewa sifa ya kuwa kipashio cha juu cha mkazo. Makundi ya toni ambayo hutolewa kwenye lugha ya mazungumzo huwa yanalingana na utamkaji wa maneno katika lugha hiyo. Kulingana na mtazamo wa Halliday, kila hatua huanza kwa/na silabi kaze na hubeba idadi ya silabi isiyowekewa msisitizo inayofuata. Kawaida silabi ya kwanza katika kundi la toni huwa imelegezwa. Kwa mfano:

**18.** // ^ **Hili / haliWEZEkani//**

Silabi toni huwa na uamilifu wa kutoa fokasi katika taarifa mpya. Katika hali ambazo hazijatambulishwa, silabi toni hutoa fokasi katika kipashio cha mwisho au cha kati cha kileksika ambacho kwa kawaida ni cha kiambajengo kinachobeba taarifa mpya. Tazama mwanzo wa usimulizi wa hadithi:

**19. a.** //**Zamani za kale katika/ KIJIJI/ chetu,//**

**b. // paliishi/ WAKAZI/ wachache sana, labda watatu.//**

**c. //Mmoja alikuwa ni /MHUBIRI/ aliyeishi upande wa pili unaoelekeana na JUA.//**

**d. //Wa pili alikuwa ni/ KICHAA/ aliyeishi upande huo//**

**e. //katika /KIBANDA/ kilichofanana na kindungu cha kuwingia ndege.//**

**f. //Watu walisema /kuwa alikuwa/ MGANGA/ kabla ya kubatizwa kichaa ........//** **(Wamitila 2002:1)**

Kutokana na mfano uliopo hapo juu msimulizi anaweka hadithi yake katika vipande vya vipashio vya taarifa ambavyo hutambuliwa kama makundi ya toni. Katika makundi hayo, kipashio cha kileksika kimeonyeshwa kwa kutumia herufi kubwa na hutambulishwa kama fokasi ya taarifa mpya. Katika mfano **(19f)** tunaona kuwa **Kichaa** anarejelewa kwa kutumia kiwakilishi **a-** katika **alikuwa** kwa sababu neno hili limetajwa katika taarifa iliyotanguliwa na hivyo kuchukuliwa kama taarifa inayojulikana na mzungumzaji.

Hadhi ya taarifa haitathmini tu kama kitu ambacho tayari kimetajwa au bado hakijatajwa katika diskosi kwa kuwa mara nyingi na kwa usahihi haya hutegemea uchukulio wa msemaji lakini sio mazingira ya matini au hali. Kile ambacho tunasema ni kuwa taarifa mpya huwa ni kirejelewa cha mwisho kulingana na uchukulio wa msemaji na kuwa ndicho taarifa mpya. Halliday anaeleza kuwa kuna uhusiano wa karibu kati ya utambuzi na kipashio cha kifonolojia katika kundi toni na cha kisintaksia katika kirai: katika hali ya kutambulishwa, kipashio cha taarifa kitatokea kwenye kirai, lakini msemaji ana uhuru wa kuifanya ilingane na kiambajengo chochote ambacho kimedhihirishwa katika muundo wa taarifa.

## 2.7 Muundo wa Taarifa na Umbo la Kisintaksia

Huu ni muundo wa taarifa kwa kuzingatia umbo la kisintaksia. Vibainishi hutumika kutanguliza taarifa mpya, kwa mfano ifuatayo ni miundo tofauti ya taarifa ya kisintaksia ambayo hurejelea vitu vinavyojulikana. Taarifa inayojulikana imepigiwa mistari chini:

**20. a. Jana usiku nyumba ya shangazi ilichomwa moto.**
**Majirani walijaribu kuuzima moto huo lakini hawakufaulu.**

**b. Maria alitoa maji kutoka kwenye kikapu.**
**Maji hayo yalikuwa moto.**

**c. Maria alitoa vitu kutoka kwenye kikapu.**
**Maji yalikuwa moto.**

**d. Jana, Halima aliuza Toyota yake.**
**Leo, Ali amelinunua gari hilo.**

**e. Nilinunua vitabu wiki jana.**
**Napenda kusoma riwaya sana.**

**f. Rehema alinunua nyumba nzee.**
**Paa lake lilikuwa linavuja.**

**g. Vito viliwekwa wapi?**
**Viliibiwa na mteja.**

**h. Niliwaona vijana wawili pale.**
**Mmoja alimkumbatia mwingine.**

**i. (katika drama, muigizaji anatoa kamba ajinyonge)**
**Hakika, huwa hajinyongi.**

**j. Hassani hufanya kazi Nairobi.**
**Ali vilevile.**

**k. Tazama!**
**Inaanguka!**

Tunapata kuwa maumbo ya kisintaksi ambayo hujadiliwa yakihusishwa na taarifa inayojulikana hujumlisha: vipashio vya kileksika ambavyo hutajwa kwa mara ya pili

kama katika **(20a)** na **(20b)**, vipashio vya kileksika ambavyo huwakilishwa na vikoa vya maana vya kileksika vilivyotanguliwa kutajwa kama katika **(20c)**, **(20d)**, **(20e)** na **(20f)**, viwakilishi vya mrejeosabiki vinavyofuata au huwa sehemu ya umbo la kileksika katika sentensi kama katika **(20a)**, **(20g)** na **(20h)**, viwakilishi vya kurejelea muktadha wa mahali kitajwa hupatikana kama katika **(20i)** na **(20k)**, na viwakilishi vya utendaji kama katika **(20i)** na **(20j)**.

Kutokana na mifano **(20a)** – **(20k)** tunapata mifano ya vitu ambavyo hurejelewa kama taarifa inayojulikana, viwakilishi na virai nomino bainifu. Katika fasihi, maumbo haya huchukuliwa kama yenye uhuru wa kubadilika na kila umbo huwa na umuhimu likilinganishwa na lingine katika muktadha mmoja kama vile:

**21.** **<u>Vi</u>liibiwa na mteja** huweza kubadilishwa na kutumika kama <u>vito</u> **viliibiwa na mteja.**

Ni dhahiri kuwa maelezo yanayotumika katika kutambulisha upya kirejelewa kile kile hubeba taarifa zaidi kuliko kurudia neno lile lile. Tunapata kuwa mazungumzo ya kujirudiarudia huchosha na kwa kawaida wazungumzaji huwa hawajirudiirudii katika mazungumzo yao. Hebu tutazame mifano ifuatayo:

**22. a. Mwalimu alifika leo darasani huku amebeba mkoba mkubwa.**

**Ndani mlikuwa na ensaiklopidia.**

**b. Mwalimu alifika leo darasani huku amebeba mkoba mkubwa.**

**Ndani ya mkoba mkubwa mlikuwa na ensaiklopidia.**

**c. Mwalimu alifika leo darasani huku amebeba mkoba mkubwa.**

**Mkoba mkubwa uliobebwa na mwalimu leo alipoingia darasani ulikuwa na ensaiklopidia ndani.**

Mchanganuzi wa diskosi ana jukumu la kutambua ni wapi taarifa inayojulikana inaporudiwa tena na ni wapi na lini taarifa mpya inapotolewa upya. Viwakilishi huwa havitumiki kama maelezo ya kutambulisha kitu kilichohamishwa bali huwa maelezo ya kutambulisha vitu vinavyojulikana. Katika data ni muhimu kutambua ni maelezo gani yanayotanguliza kitu kipya katika diskosi na ni maelezo gani yanayotumika kutanguliza mambo ambayo yanajulikana au yametajwa katika diskosi.

## 2.8 Muundo wa Taarifa na Muundo wa Sentensi

Tunaweza tukabainisha tofauti iliyopo kati ya taarifa mpya na taarifa inayojulikana kama ifuatavyo kulingana na mtazamo wa Hornby (1972):

| **Sentensi** | **Taarifa mpya na taarifa inayojulikana** |
|---|---|
| **23. a.** Ni mvulana anayempakata paka | Inayojulikana: X anampakata paka |
| | Mpya : X ni **mvulana.** |
| **b.** Ni paka anayepakatwa na mvulana. | Inayojulikana: Mvulana anampakata X. |
| | Mpya : X ni **paka** |
| **c.** Anayempakata paka ni mvulana. | Inayojulikana: X anampakata paka |
| | Mpya : X ni **mvulana.** |

**d.** Anachopakata mvulana ni paka. Inayojulikana : Mvulana anapakata X.

Mpya : X ni **paka.**

**e.** Mvulana anampakata paka. Inayojulikana: X anampakata paka.

Mpya : X ni **mvulana.**

Halliday (1967) anaeleza kuwa sentensi huangaza taarifa inayojulikana na taarifa mpya kwa kuweka mkazo au msisitizo katika maneno mahsusi. Neno lenye mkazo au kirai kinachobeba mkazo kwa kawaida hubeba taarifa mpya. Halliday anasisitiza kuwa mzungumzaji ndiye huangaza hadhi ya taarifa. Kulingana na mifano tuliyotoa hapo juu, kuna maswala kadhaa yanayoibuka. Kwanza, sio dhahiri ikiwa taarifa mpya na taarifa inayojulikana hubainishwa na umbo la sentensi au na athari ya uwekaji msisitizo kwenye viambajengo tofauti vya sentensi au kutokana na uhusiano wa mifumo hii miwili. Pili, Halliday anachukulia kuwa sentensi huangaza taarifa mpya na taarifa inayojulikana. Pia anasisitiza kuwa wazungumzaji ndio huangaza hadhi ya taarifa. Tatu, Hornby (1972) na Clark na Clark (1977:93) wanaonelea kuwepo kwa fokasi moja ya taarifa kwa kila sentensi. Kulingana na Halliday, kila kishazi kinatarajiwa kubeba fokasi moja ya taarifa kama ifuatavyo:

**24. a. //siwezi yakhe// sijawahi kunywa maisha yangu//**

**b. //mwenye kutafuta elimu//sharti akeshe usiku//**

Nne, dhana ya taarifa inayojulikana haitumiwi kama dhana changanuzi kuelezea hadhi ya virejelewa vya maelezo katika hadhi ya virejelewa kama uchukulio ulioelezwa na vishazi katika sentensi.

Taarifa hupataje hadhi ili ichukuliwe kuwa ni taarifa inayojulikana? Halliday anaeleza kuwa taarifa inayojulikana huwa ni taarifa inayochukuliwa na msemaji kama ile inayoweza kupatikana upya kwa kutumia mrejeosabiki au muktadha nayo taarifa mpya huchukuliwa kama kiini lakini sio kumaanisha kuwa haijatangulizwa lakini tukizingatia kuwa msemaji anaiwasilisha kama ambayo haiwezi kupatikana upya katika diskosi iliyotangulia. Dahl (1976:37) anaeleza kuwa dhana za taarifa inayojulikana na taarifa mpya hutumika kuelezea mambo ya kijumla katika lugha kama vile kiimbo, mkazo na mpangilio wa maneno na pia matumizi ya mbinu za mrejeosabiki.

Chafe (1976:30) anasema kuwa tukisema kuwa jambo fulani ni taarifa inayojulikana ni kusema kuwa ni ile ambayo msikilizaji anatarajiwa kuwa anaijua tayari. Chafe anasisitiza kuwa hadhi ya taarifa inayojulikana inastahili kuwekewa mipaka katika ufahamu ambao msemaji anachukulia kuwa uko kwenye hisia za msikilizaji wakati wa mazungumzo au usemi. Anaendeleza dhana ya mambo muhimu akilini na ambayo hupewa kipaumbele na msikilizaji ili kuonyesha umuhimu wake. Anadai kuwa hali ya taarifa inayojulikana ni hadhi isiyodumu kwa sababu taarifa mpya inapoingizwa katika diskosi ile inayojulikana hutoweka, kama vile:

**25. Rashid: Lo! Nani wale?**
**Kijana: Wako wapi?**
**Rashid: Wale watu waliojipaka rangi nyeusi.**
**Kijana: Hawakupaka rangi wale.**

Ingekuwa rahisi kwa Rashid kuuliza kuhusu vijana fulani waliokuwa wamejipaka rangi nyeusi. Lakini maneno '*nani wale*' yanachukuliwa kama taarifa mpya kwa kuwa ni jambo ambalo halikuwa akilini mwa msikilizaji wakati wa usemi. Taarifa inayojulikana

inatarajiwa kutambulikana huku taarifa mpya ikiwa haijulikani. Wasikilizaji wanastahili kuamini kuwa taarifa inayojulikana hubeba taarifa ambayo wanaweza kujitambulisha kwayo. Wanaelewa kuwa ni taarifa ambayo mzungumzaji anaamini kuwa wote wanakubali na kuwa mzungumzaji anadai kuiamini.

## 2.9 Uainishaji wa Hadhi ya Taarifa

Prince (1981:235) anapendekeza kuwa msemaji anaweza kutanguliza mambo mapya katika diskosi kwa njia mbili. Mambo mapya kabisa ambayo huchukuliwa kuwa hayajulikani kwa njia yoyote na mzungumzaji na yatatangulizwa katika diskosi kwa kutumia maelezo yasiyo bainifu kama vile:

**26. 'Najum, kijana wa Kiarabu hirimu yake Bwana Msa, bila ya kungojea kuambiwa.....'** **(Abdulla M.S 1968)**

Katika kauli hii. tunapata kuwa kuna mambo mapya kabisa ambayo yanatangulizwa katika diskosi. yaani maelezo kumhusu Najum.

Aina ya pili ni mambo ambayo hayajatumika na ambayo yanachukuliwa na msemaji kuwa yanajulikana na mpokezi katika ufahamu wa awali. lakini sio katika hisia zake wakati wa mazungumzo. kama vile:

**27. Rashid: Lo! Nani wale?**
**Kijana: Wako wapi?**
**Rashid: Wale watu waliojipaka rangi nyeusi.**
**Kijana: Hawakupaka rangi wale.**

Kijana alikuwa anawafahamu watu wale waliokuwa wamejipaka rangi kulingana na Rashid, lakini katika hisia zake wakati wa mazungumzo hakuwa akiwafikiria na ndiyo sababu anamuuliza Rashid, ***'wako wapi?'***

Aina ya tatu ni mambo yanayoamsha hisia: hisia za kihali kama matumizi ya viwakilishi ***mimi*** na ***wewe***, na hisia za kimatini ambazo ni mambo ambayo tayari yametangulizwa katika diskosi na ambayo yanarejelewa kwa mara ya pili au zaidi. Mambo yanayoamsha hisia ndiyo Halliday na Chafe wanachukulia kama taarifa inayojulikana kama vile:

**28. Mimi nataka unieleze vipi ulijua kuwa yeye Ali Makame ndiye aliyeingia ndani akafungua sanduku akaiba fedha na kisanduku cha dhahabu za yule bibi? (Abdalla M.S 1968)**

Kifungu hiki kinatuelekeza kuwa mambo ambayo yanazungumziwa katika usemi huu ni mambo ambayo tayari yanaeleweka na wote, msemaji na msikilizaji.

## 2.10 Hitimisho

Katika sura hii, tumeangazia maswala mbalimbali yanayohusiana na mada, fokasi na msingi wa kinadharia wa muundo wa taarifa. Maswala haya na vigezo vilivyozungumziwa hapa vitachangia katika uchanganuzi wa data katika utambulishaji wa mada na fokasi katika Kiswahili Sanifu. Aidha mtazamo wa muundo wa taarifa utatumiwa katika kutambulisha taarifa mpya na taarifa inayojulikana katika vipengele mbalimbali vya sentensi katika muktadha wa diskosi.

Katika sura ya tatu, tutachunguza na kuchanganua sentensi ambazo hutumika katika utambulishaji wa fokasi katika Kiswahili Sanifu.

# SURA YA TATU

# TUNGO ZENYE KUTAMBULISHA MADA

## 3.1 Utangulizi

Katika sura ya pili tumejadili masuala ya kimsingi yanayotumika katika uchanganuzi wa data na ambayo yanahusu utambulishaji wa mada na fokasi. Tumetoa ufafanuzi wa jinsi muundo wa taarifa hutumiwa katika utambulishaji wa taarifa mpya na taarifa inayojulikana. Katika sura hii, tutashughulikia tungo zenye kutambulisha mada katika Kiswahili Sanifu. Mada katika sentensi huhitaji kuakisiwa kama vile katika kutangulizwa katika sentensi, kuihamisha kushoto, n.k. Tungo zenye kusimba mada ambazo zitashughulikiwa hapa zitajikita katika mpangilio wa maneno katika muktadha wa kipragamtiki.

## 3.2 Kutanguliza Mada Katika Sentensi

Tungo zenye kutanguliza mada katika sentensi huangaliwa kipragmatiki kama zenye kwenda kinyume na mpangilio wa maneno. Mbinu hii huwa na mipaka yake katika viwakilishi vya KN katika kishazi. Ni mbinu inayohusu kutanguliza mada linganuzi, ikiwa haijatokea katika nafasi ya kwanza katika kishazi. Mada linganuzi inapochukua nafasi ya kwanza katika kishazi, huwa inatiliwa mkazo ili kuitambulisha. Mada hutangulizwa katika sentensi wakati kirejelewa kimoja kinapolinganishwa na kirejelewa kingine na ambavyo viko katika kundi moja kisemantiki. Kwa mfano:

**29. "Nenda <u>kwao</u>" (<u>wewe</u> <u>nenda</u> <u>kwao</u>)**

**W T E**

**"<u>Kwao</u> <u>siwezi</u> <u>kwenda</u> maanake sina mazowea hayo"**

**E Ts T** **(Shafi 1979:116)**

Neno ambalo linawakilisha mada katika mfano wa **(29)** huweza kuhamishwa na kutangulizwa katika sentensi katika muktadha wa mazungumzo. **Kwao** katika sentensi ya pili ni kiambajengo ambacho kimehamishwa mwanzoni mwa sentensi kudhihirisha kuwa kinabeba mada ya tamko hilo. Hapa tunapata ulinganuzi wa mada kwa kuhamisha mada mwanzoni mwa sentensi na kategoria ya sentensi inayohamishwa ni kielezi cha mahali. Kama vile:

**30. '<u>Wewe</u> <u>nenda</u> <u>kwao</u>"**

**W T E**

**"<u>Kwao</u> <u>siwezi</u> <u>kwenda</u> ........"**

**E Ts T** **(Shafi 1979:116)**

Kutokana na mazungumzo haya ambayo yalifanyika kati ya Rashidi na Salum, tunapata kuwa Rashidi alikuwa anatamani sana kumtembelea Amina, msichana rafiki yake, lakini hakujua afanye nini. Kutokana na tatizo hilo, Salum, rafiki yake anamwambia aende *kwao* yaani kwa akina Amina. Kielezi *kwao* ndicho mada ya kauli hii ambacho kimetangulizwa mwanzoni mwa sentensi na kudhihirisha kuwa ni taarifa ambayo tayari inajulikana. Ikiwa Rashidi alitaka kumuona sana Amina hangempata mahali pengine isipokuwa kwao.

Kategoria nyingine ya sentensi ambayo inaweza ikatangulizwa mwanzoni mwa sentensi ni kiarifu, kwa mfano:

**31. "Rashidi kawa mtundu sana siku hizi" Bi Mashavu alianza mazungumzo, "<u>Nd'o mwanamume</u>, lazima awe mtundu." Majaliwa alisema**

**(Shafi 1979:5)**

Maneno '*mtundu siku hizi*' yanalinganishwa na '*Nd'o mwanamume*' katika maneno ya Majaliwa. Katika jibu lake Majaliwa ametanguliza mada mwanzoni mwa sentensi ili kuthibitisha kuwa habari inayojulikana inabebwa na maneno yanayolingana na kiarifu katika sentensi kwanza na ambayo yanamrejelea mwanao Rashidi ambaye ameanza kuwa mtundu kulingana na mkewe, Bi Mashavu.

Hali kadhalika tunaweza kuwa na ulinganuzi wa yambwa tendwa kama katika mfano ufuatao:

**32. Nilimwona Ali pale.**
**<u>Maria</u> sikumwona.**

*Ali* ni kiambajengo ambacho kinabeba uamilifu wa yambwa tendwa. Kwa kufuata ulinganuzi wa mada, tunatanguliza mada katika kauli ya pili kwa kutumia kiambajengo *Maria* ambacho kinahamishwa kushoto kulingana na mpangilio wa maneno ambao ni huru kwa kiasi katika Kiswahili Sanifu.

Katika kauli ya kwanza *Ali* ndiye anayetangulizwa kama mada ya sentensi ile, lakini kwa kuwa tunatanguliza mada katika sentensi kwa kutumia mada linganuzi jina la *Maria* linatumika kuonyesha ulinganuzi wa majina haya ambayo yako katika kundi moja

kisemantiki. Ni muhimu kukumbuka kwamba katika kauli ya kwanza tunapomtaja *Ali*, jina la *Maria* liko katika uchukulio wa msikilizaji na ndiyo sababu pale linapotajwa katika kauli ya pili halichukuliwi kama taarifa mpya bali kama taarifa inayojulikana.

Pia tunaweza tukawa na ulinganuzi wa yambwa tendewa kama vile:

**33. Tulimnunulia Maria nyumba.**
**<u>Amina</u> hatukumnunulia kitu.**

Yambwa tendewa katika mfano wa **(33)** ni *nyumba* aliyonunuliwa Maria ambayo inapewa ulinganuzi na Amina ambaye hakununuliwa kitu. Hii ndiyo sababu *Amina* anatangulizwa mwanzoni mwa sentensi kama mada linganuzi.

Tukizingatia mifano ya kauli ambazo huwa na mada ikiwa katika nafasi tangulizi katika kishazi, kama tulivyosema hapo awali, mada huwa inapewa mkazo ikiwa katika nafasi iliyotokeza mwanzoni. Kwa mfano:

**34. a. Kamau alitia bidii sana masomoni.**
**b.<u>Wanjiru</u> hakuthubutu.**

Katika sentensi ya **(34a)**, *Kamau* ndiye kiambajengo kinachobeba mada ya sentensi hiyo. Kwa kuwa kimetokea mwanzoni mwa sentensi kama kiima ambacho huchukuliwa kuwa mada, ili kuitambulisha mada, inabidi kirejelewa hiki kipewe msisitizo au mkazo.

Givon (2001:263) anaeleza kuwa sifa moja ya vishazi vinavyotanguliza mada ni kuwa vishazi hivi huwa ni vya namna moja. Kwa hivyo, huwa vina ulinganuzi na uhamishaji

kushoto pale ambapo kiambajengo kinachotangulizwa hutengwa kutoka kwenye kishazi kizima kwa kutumia vipumuo kama vile koma. Kwa mfano:

**35. <u>Na leo</u>, baada ya siku nyingi, Rashidi alimwona tena yule mpishi anashughulika kuwagawia chakula. (Shafi 1979:51)**

Kauli ya kwanza katika kishazi hiki '*Na leo*' imehamishwa na mwandishi au imetangulizwa katika kishazi na imetenganishwa na kishazi kizima kwa kutumia kipumuo au koma ili kumaanisha kuwa neno *leo* lina ulinganuzi na maneno yanayofuata katika sehemu ya kishazi. '*baada ya siku nyingi.*' Maneno yaliyotumiwa na mwandishi katika kauli hii ni kuwa yanaturudisha nyuma katika diskosi hadi wakati Rashidi alipokuwa akitafuta kazi. Yule mpishi anayetajwa pale alimpa Rashidi kazi ya kuosha visinia na malipo aliyoyapata ni chakula cha mchana. Kwa hivyo, mwandishi anaturudisha nyuma hadi wakati huo siku nyingi zilizokuwa zimepita. Kwa kuwa mpishi na Rashidi hawakushirikiana kwa muda mrefu haikuwa rahisi kwa mpishi yule kumkumbuka Rashidi.

Kutokana na mifano tuliyoitoa, tunapata kuwa mada huweza kutangulizwa mwanzoni mwa kishazi kama taarifa inayojulikana kwa kutumia ulinganuzi kati ya maneno ambayo huwa katika kundi moja kisemantiki. Mada inaweza kutambulishwa kama kiima au kiarifu cha sentensi.

## 3.3 Kuhamisha Mada Kushoto

Kuhamisha mada kushoto ni mbinu inayotumiwa kutambulisha virejelewa vya mada hususan vile bainifu na vya mrejeosabiki ambavyo vimeachwa nje ya diskosi kwa muda. Mbinu hii hutumika wakati mwandishi au msemaji anakusudia kurejesha upya kirejelewa katika diskosi. Virejelewa ambavyo vinahamishwa kushoto, huwa ni vile ambavyo vimetumika katika diskosi na panakuwa na haja ya kuvitumia upya katika diskosi. (Givon, 2001:265).

Kutokana na riwaya ya *Kuli* tunapata mfano ufuatao wa kuhamisha mada kushoto:

**36. King'ora kimelia. Ni saa moja na nusu asubuhi. Watu wamekasirika na mamia yao wameuzonga mlango wa chuma unaowazuia wasiingie ndani ya bandari ya mji wa Unguja.**

**Kelele, matusi na malalamiko; vijana, watu wazima na hata watoto, wote wakiwa wamevaa nguo chafu zilizoraruka, nyingine zikiwa zimepoteza rangi yake ya awali kwa kupakua na kwa kutiwa viraka vya rangi mbalimbali.**

**Nyuma ya mlango wa chuma amesimama Mhindi mmoja na ..............**

**(Shafi, 1979:9)**

Katika aya ya kwanza tunapata kirejelewa *mlango wa chuma* kimewasilishwa katika diskosi kwa mara ya kwanza, kitaweza kubeba uamilifu wake iii kitolewe au kiweze kutumika kama kiarifu katika diskosi inayofuata. *Mlango wa chuma* ni kirejelewa

kilichotumika katika aya ya kwanza kuonyesha kuwa watu waliokuwa wakitafuta kazi bandarini walizuiliwa nyuma ya mlango huo wa chuma ili wasiingie bila kibali. Katika aya inayofuata, kirejelewa hiki hakijatajwa kamwe kwa kuwa aya hiyo inatuelezea mambo tofauti na yale yanayohusu mlango huo wa chuma. Aya ya pili inahusu hali ya watu, wazee, vijana na watoto waliofika bandarini kutafuta kazi.

Katika aya ya tatu kirejelewa, *mlango wa chuma*, kimerudishwa katika diskosi ili kutoa ufafanuzi zaidi na umuhimu wake katika diskosi. Sababu ni kuwa mlango wa chuma ndiyo mada ya usemi huu na kuwa mwandishi anairudisha katika diskosi ili kuendeleza matumizi yake. Mlango wa chuma ulikuwa kizuizi kilichotumiwa na Mhindi kuchuja waliokuwa na nguvu ili waingie bandarini kufanya kazi. Katika aya ya tatu kirejelewa kimetangulizwa mwanzoni mwa sentensi kama taarifa ambayo inajulikana tayari. Kirai 'Nyuma ya *mlango wa chuma'* ni mfano wa kuhamisha mada kushoto ili kuitumia upya katika diskosi.

UNIVERSITY OF NAIROBI
EAST AFRICANA COLLECTION

Lambrecht (1994:181) anaeleza kuwa kuinua uwakilishaji wa kirejelewa kutoka hali ya kutotumika hadi hali ya kutumika katika utambuzi wa msikilizaji humfanya msemaji kusimba kirejelewa hicho kama kauli ya mada iliyopendelewa. Tukirejelea mfano ulio hapo juu, mada iliyohamishwa kushoto (*nyuma ya mlango wa chuma*) inainua kirejelewa (*mlango wa chuma*) kutoka hali ya kutotumika na kukipa hadhi ya kutumika upya na hivyo kuanzisha mada mpya ambayo katika utambuzi inaweza ikapatikana upya.

Inatokea kuwa, virejelewa ambavyo tayari vimetumika katika usemi husimbwa katika umbo la kileksika la kirai nomino kuliko kwenye viwakilishi, kwa mfano wakati ambapo inabidi kuepukana na utata unaotokana na kuwepo kwa virejelewa viwili au zaidi ambavyo vinatumika kwa wakati mmoja, kama vile:

**37. Leo asubuhi niliwaona Ali na Hassani.**

**Yeye ni mgonjwa sana.**

Katika mfano huu tunapata kuwa si dhahiri ni kipi kati ya virejelewa *Ali* au *Hassani* kinawakilishwa na kiwakilishi *yeye*. Ingefaa zaidi, katika muktadha huo, kurejelea yule ambaye ni mgonjwa kwa kutumia nomino *Ali* au *Hassani*.

Hali kadhalika, tungo zenye kuhamisha mada kushoto hutumika kutambulisha jinsi msisitizo huhamishwa kutoka kwa kirejelewa kimoja hadi kwenye virejelewa viwili au zaidi. Hii ndiyo sababu tunapata utokeaji wa viwakilishi vya KN ambavyo vimehamishwa, kama vile:

**38. "Kwani wewe rafiki yangu jina lako nani?"**

**"Mie! Mie naitwa Saburi."** **(Shafi 1979:12-13)**

Kiwakilishi *mie* kimerudiwa mara mbili katika KN ambacho kinawakilisha kuhamishwa kwa mada kushoto. Maneno au viwakilishi vya Virai Nomino kwa kawaida huwa na uamilifu na ulinganuzi ambao hurejelewa kama Virai Nomino vya mada linganuzi. Tunaweza tukalinganisha mifano zaidi:

**39. a. Nilinunua nguo jana. <u>Inapendeza</u> sana**

**b. Nilinunua nguo na kiti jana. <u>Inapendeza</u> sana, lakini kilikuwa <u>kimevunjika.</u>**

Kiwakilishi kinachorejelea nguo katika sentensi **(39a)** na **(39b)** kimetumika kwa njia moja, kuwa kinarejelea *nguo*, lakini katika sentensi ya pili kimewekewa msisitizo zaidi. Kuna ulinganuzi kati ya viwakilishi vya virejelewa vya *nguo* na *kiti.*

Kiswahili ni lugha ambayo ni bainishi, (Whiteley, 1968:101), na vitenzi vyake hubeba viambishi vinavyowakilisha kiima. Kwa hivyo, viambishi ambavyo vinawakilisha virejelewa huwa vimeambatishwa kwenye kitenzi, kama vile, *i-na-pend-e-z-a*. Hata hivyo vivumishi visisitizi hutumika ili kidhihirisha uhamishaji wa mada kushoto. Kwa mfano:

**40. Nyumba yenyewe ilikuwa ya kupanga ingawa ilikuwa si nyumba ya kuitwa nyumba. Lilikuwa banda tu .......... (Shafi 1979:16)**

Katika usemi huu, mada imehamishwa kushoto kwa kutumia kivumishi *yenyewe* ambacho kinatambuliwa kwa kuwekewa mkazo au msisitizo.

Givon (2001:267) anaeleza kuwa katika lugha, KN ambacho kimehamishwa kushoto hutambulishwa kama yambwa kuliko kama kiima. Kwa mfano:

**41. "Mbona nasikia parkacha parkacha huko! Nani tena huyo?" Bi Mashavu aliuliza kutoka jikoni.**

**"Mie Rashidi" (Shafi 1979:42)**

Kiwakilishi *mie* kinachotumiwa katika usemi huu na Rashidi kujirejelea, kinaweza kutambulishwa kuwa ni uhusika wa yambwa kuliko kuwa kiima kwa kuwa mwandishi angechagua kutumia:

**"Ni mimi Rashidi"** au

**"Ndiye mimi Rashidi"**

Katika mazungumzo ya kawaida huwa tùnapata watu wakisema:

**42. Swali: Umesikia kutoka kwa Kamau?**

**Jibu: Kamau, yeye ni mgonjwa sana siku hizi.**

Katika mazungumzo haya, tunapata kuwa kiarifu au yambwa inahamishwa kushoto kama taarifa ambayo tayari inajulikana kumrejelea yule anayeuliziwa katika swali hilo. Taarifa inayojulikana ndiyo pia mada iliyohamishwa kushoto katika sentensi ya pili.

## 3.4 Kuhamisha Mada Kulia

Lambrecht (1994:199) anatoa maelezo kuhusu madai ya wanaisimu wengi kuhusu nafasi ya mada katika sentensi. Wanaisimu hawa hasa wa Shule ya Prague wamedai kuwa kuna kanuni bia au mwelekeo imara kati ya lugha unaoshikilia kuwa mada hutokea kama kiambajengo cha kwanza katika sentensi. Mada kulingana na sarufi mapokeo hulinganishwa na kiima kama vile:

**43. Watoto wameenda shule.**

**Kiima kiarifu**

Kwa kuwa kiima hutangulia mwanzoni mwa sentensi, basi huwa kinachukuliwa kuwa kinatambulisha mada ya sentensi hiyo. Kwa hivyo tunaweza tukasema kuwa mada ya kauli hii ni *Watoto*.

Kuhamisha mada kulia ni hali isiyo ya kawaida katika lugha hasa katika Kiswahili Sanifu. Lakini tunapata katika hali zisizo rasmi au katika muktadha wa mazungumzo mada huweza kuhamishwa kulia. Uhamishaji huu hukiuka mwelekeo wa sarufi mapokeo wa kuwa mada hutokea mwanzoni mwa sentensi huku ikichukua nafasi ya kiima. Kama tulivyotaja hapo awali kuhusu uhamishaji wa mada kushoto, msemaji huwa na uhuru wa kuhamisha mada kulia ili kuinua utokeaji wa kirejelewa ambacho hakijatajwa katika mazungumzo yake na angetaka kukileta katika utambuzi wa msikilizaji na hapo basi kukisimba kama mada iliyopendelewa. Kuhamisha mada kulia katika sentensi husaidia katika kubeba taarifa ya kauli hiyo inayohusu kirejelewa cha mada. Kwa mfano:

**44. "He! Hata hupumziki kidogo, mara kufika nyumbani na kutoka tena?" Amina aliuliza akiwa na wasiwasi.**

**"Nina miadi na <u>mtu</u>, kuna mambo muhimu tunataka kuzungumza." Rashidi alijibu ..........** **(Shafi 1979:146)**

Kutokana na mazungumzo hayo kati ya Amina na Rashidi, haijitokezi dhahiri ni mtu wa aina gani atakayekutana naye Rashidi. Neno hili *mtu* limetumika kama kiwakilishi cha jina la Faraji ambalo tunalipata baadaye katika diskosi. Faraji ndiye yule anayerejelewa na Rashidi katika mazungumzo yake na Amina. Mwandishi ametumia mbinu ya

kuhamisha mada kulia katika hali ya kumpatia msomaji taharuki ya kutaka kujua huyu mtu ndiye nani ili aendelee kusoma riwaya akiwa na matarajio fulani.

Jukumu la kisemantiki la kirejelewa *mtu* kama kiambajengo cha KN katika usemi huu huonyeshwa kwa kutumia kiwakilishi ambacho hurejelea kiambajengo cha kileksika ambacho kimehamishwa kulia. (Lambrecht. 1994:203). Tofauti na matumizi ya kiwakilishi kurejelea kirejelewa kilichohamishwa kulia. tunapata kutokana na mfano wetu hapo juu kuwa kirejelewa huweza kuwakilishwa na nomino ya jumla kama vile *mtu* kama ilivyotumika katika usemi. Nomino hii ya jumla inatumika kurejelea nomino maalum. **Faraji** ambaye ndiye mada iliyohamishwa kulia.

Kwa kawaida. tungo ambazo huhamisha mada kulia hutumika kwenye virejelewa ambavyo tayari vimetajwa au havijatajwa sana. lakini haiwezi ikatumika katika uamilifu wa ulinganuzi kama ilivyo katika kuhamisha mada kushoto au kutanguliza mada. Kwa mfano *Rashidi*. kabla ya harusi yake kwa Amina. walikuwa na matatizo kazini jambo ambalo lilisababisha kukutana faraghani yeye na wafanyakazi wenzake. Aliyekuwa kiongozi wao katika shughuli hizo alikuwa ni Faraji ambaye kila wakati aliandamana na Rashidi mikutanoni. Rashidi haoni haja ya kumjulisha Amina kuhusu mikutano yao na hii ndiyo sababu anamwambia kuwa anatoka kidogo kumuona mtu wakazungumze mambo muhimu. Baadaye katika diskosi. Faraji anatajwa wakizungumza na Rashidi kazini siku iliyofuata usiku wa mkutano na Amina pia anapata kumjua na kumfahamu Faraji.

Ni dhahiri kuwa virejelewa ambavyo havijatajwa kamwe katika diskosi haviwezi kutumika katika kuhamisha mada kulia au. kushoto. Lazima virejelewa hivi viwe vimetajwa mahali mara moja au zaidi katika diskosi iliyotangulia. Kulingana na mtázamo wa muundo wa taarifa (Brown and Yule, 1983:153), taarifa inayojulikana na ambayo ndiyo mada ya kauli huwa inarejelea ile sehemu ya kauli inayoarifiwa katika usemi. Mada inapoelezwa inakuwa ujumbe unaojulikana au mambo ambayo tayari yanasemwa na kueleweka. Kwa mujibu wa Brown na Yule, kirejelewa ambacho kinahamishwa kulia, lazima kiwe kimetajwa hapo awali katika diskosi.

Kama tulivyotaja hapo awali, tungo zenye kuhamisha mada kulia huweka KN, ambacho hubeba mada mwishoni mwa kishazi na ambacho hubeba taarifa kuhusu kirejelewa cha mada. Tungo kama hizi katika fasihi hurejelewa kama mpangilio wa maneno uliogeuzwa au usiofuata kanuni za kisarufi za lugha fulani. Kwa mfano:

**45. *Yeye* ni kijana mzuri sana, <u>kaka yake</u> ambaye ..........**

Kulingana na kauli hii kiwakilishi *yeye* kinatangulizwa kabla ya kauli inayobeba mada ya *kaka yake* ambayo inachukua nafasi inayofuata katika sentensi. KN kilichohamishwa kulia hakibebi msisitizo kama kiwakilishi chake. Katika muktadha wa matamshi, kiwakilishi *yeye* kitapewa msikiko zaidi kuliko KN *kaka yake*. Hali kadhalika tunapata kuwa KN kilichohamishwa kinabeba upekee wa kipragmatiki kwa kuwa wakati kirejelewa cha kauli ya KN hicho kinapotajwa katika umbo lake la kileksika, tunapata kuwa tayari kimerejelewa kwa kutumia umbo la kiwakilishi katika kishazi. Kiwakilishi hicho ndicho hutumika katika kufafanua kirejelewa hicho.

Lambrecht (1994:203), akipinga madai ya Vennemann (1974), Hyman (1975), Givon (1976), Horis (1976) na Bailard (1981), anaeleza kuwa ni muhimu kutambua kuwa kiambajengo kilichohamishwa katika tungo ambazo huhamisha mada kulia sio hali inayoelezea utokeaji wa kirejelewa kisicho na umuhimu. Anaeleza kuwa kuhamisha mada kulia ni utungo ambao hufuata kaida za kisarufi na ambao humruhusu msemaji kufuata Kanuni ya Utengano wa Urejeleo na Uamilifu katika hali ya usemi mahsusi. Kwa mfano

**46. "Basi nakupa fununu ya kwamba safari hii mambo mazuri kweli kweli, lazima watatutambua wale," Faraji alimpa moyo Rashidi.**

**"Kweli?" Rashidi aliuliza kwa hamu zaidi.** **(Shafi 1979:147)**

Katika mfano huu kiwakilishi *wale* kimehamishwa mwishoni mwa kishazi. Kama kishazi hiki kingefuata kanuni ya muundo wa maneno katika sentensi za Kiswahili tungepata:

**Wale lazima watatutambua leo.**

*Wale* katika usemi huu ni kiwakilishi cha KN kinachorejelea kundi fulani la watu ambao walikuwa wasimamizi kule bandarini na ambalo lilikuwa linawanyanyasa wafanyakazi.

Kanuni ya Utengano wa Urejeleo na Uamilifu ni kanuni ya kisarufi ambayo inaeleza kuwa kiwakilishi cha kileksika cha kirejelewa cha mada hutokea katika nafasi tofauti na ile inayochukuliwa na jukumu la kirejelewa. Tukifuata mfano tulioutoa hapo juu, tunapata tungo za kuhamisha kulia au kushoto hukifanya KN kinachorejelewa kutokea mahali tofauti na pale kinapostahili kutokea kulingana na kanuni ya muundo wa sentensi.

Muundo wa sentensi huvifanya Virai Nomino vyote vya kiarifu kutokea kama Virai Nominovya kisarufi katika kiwango cha muundo wa kishazi.

Msemaji ambaye hutumia tungo zenye kuhamisha mada kulia huwa anaelewa kuwa, pindi tu kiwakilishi cha mada hakitoshelezi uelewa wa msikilizaji kuhusu hali ya nani au nini kinachoelezwa na kauli, yeye huhamisha mada kushoto katika muundo wa KN ili kufanikisha lengo lake la kuwasilisha taarifa iliyo kamili. Katika hali ya kawaida ya ushirikiano kati ya msemajii na msikilizaji, matumizi ya kiwakilishi hukubalika tu pale ambapo kirejelewa chake kimetumika katika diskosi. Utungo wa kuhamisha mada kulia huweza kutumika kama ombi lililodokezwa na msemaji kwa msikilizaji, aiweke wazi taarifa inayobebwa na kauli hadi pale mada iliyohamishwa kulia inapotajwa. (Lambrecht: 1994). Kwa mfano:

**47. "Wafanyakazi wa bandarini <u>tu</u>mechoka kudhiliwa. Siku kadhaa <u>tu</u>medai madai kadha wa kadha bila kufanikiwa. Kampuni ya Smith Mackenzie imekwisha <u>tu</u>onyesha wazi kama hawana nia wala azima yoyote ya kuleta mabadiliko ya aina yoyote kwa manufaa ya wafanyakazi." (Shafi, 1979:153)**

Kulingana na usemi huu tunapata kuwa KN *wafanyakazi* kimetumika mwanzoni mwa kauli na katika sentensi zinazofuata, viwakilishi vinavyorejelea wafanyakazi ndivyo vimetumika vikiwa viambishi vitangulizi katika vitenzi. KN kinachorejelea wafanyakazi kimetumika tena mwishoni mwa usemi huu. Usemi huu ni sehemu ya barua kutoka kwa kiongozi wa wafanyakazi wa bandarini kwa wafanyakazi. Kiongozi wao ndiye msemaji

wao na anapitisha taarifa muhimu kwa wafanyakazi. Mwandishi anatumia mbinu ya kutumia viwakilishi badala ya nomino kurejelea wafanyakazi katika usemi wote na kukamilisha kwa kuwataja wafanyakazi mwishoni mwa usemi. Hii ni njia moja, kama tulivyotaja hapo awali kuwa, msemaji ana ruhusa kutoka kwa msikilizaji ya kutumia viwakilishi hadi mwishoni atakapoweka KN kinachobeba taarifa inayojulikana na ambayo ndiyo mada ya kauli nzima.

Hata hivyo, tungo zenye kuhamisha mada kulia huwa na athari kwenye muundo wa kishazi kisintaksia. Katika lugha nyingi ikiwemo Kiswahili Sanifu, kiambajengo cha kuhamisha mada kulia, moja kwa moja, hufuata kishazi kinachobeba kauli ya kiwakilishi cha mada. Hivi ni kumaanisha kuwa huwa kimetambulishwa kisintaksia kama sehemu ya kishazi kinachobeba kiwakilishi cha mrejeosabiki. Kwa mfano:

**48. Kule anakofanya kazi, Nairobi.**

Kulingana na Givon (2001), kuna sifa tatu ambazo hubainisha tungo zenye kuhamisha mada kulia, nazo ni: kiwakilishi cha mrejeosabiki, alama ya koma inayodhihirisha mwisho wa kauli yenye kuwekewa mkazo, na utambulisho wa uhusika ulio horomo. Kwa mfano:

**49. "……………… anaruka majini, <u>yeye</u> huogelea upesi sana, na ………….."**

Mfano huu unatuonyesha kuwa kiwakilishi *yeye* kimehamishwa kulia na kinawakilishwa na kiambishi *a-* katika <u>*anaruka*</u>. Pia *yeye* ni KN chenye uamilifu wa kiima kilichohamishwa kulia katika kishazi.

Tofauti na ilivyo katika lugha zingine, lugha za Kibantu hususan Kiswahili Sanifu huonyesha tofauti kidogo sana katika kuhamisha mada kulia hasa inapotokea baada ya kitenzi. Hii ni kwa sababu Kiswahili Sanifu ni lugha ambayo mpangilio wake wa maneno huwa uko huru kwa kiasi. Kwa hivyo, huenda kukatokea ukosefu wa uelewa kati ya tungo zilizohamisha mada kulia na zile ambazo mpangilio wa maneno umebadilishwa na KN kutokea mwishoni mwa kishazi au kauli. Kwa mfano katika sentensi hii:

**50. Rashidi aliwatazama kwa hasira askari wale na kwa uchungu aliwaambia, "Yana mwisho <u>haya</u>"** **(Shafi 199:198)**

Kulingana na mpangilio wa maneno unaochukuliwa kuwa wa kawaida, maneno ya Rashidi yangekuwa:

**"Haya yana mwisho"**

Lakini kwa kuwa kiwakilishi *haya* ambacho kimo mwishoni mwa kishazi kinarejelea matatizo yanayowakumba wafanyakazi bandarini, msemaji anachagua kutumia KN hicho mwishoni mwa sentensi kuonyesha jinsi mada ilivyohamishwa kulia huku ikiwakilishwa na kiambishi *ya* katika kiambajengo *yana*.

## 3.5. Kuhamisha Yambwa Tendwa na Yambwa Tendewa

Vitale (1981:44) anaeleza kuwa Kiswahili Sanifu huwa na aina za sentensi ambazo hubeba yambwa tendwa na yambwa tendewa. Tungo hizi huwa na virai nomino vitatu kama ifuatavyo:

**51. $KN^1$ ___________ $KN^2$ $KN^3$**

Kwa mfano katika sentensi:

52. **Maria alimpigia Juma simu jana.**

**KN¹ KN² KN³**

Yambwa tendwa huchukua **KN²** nayo yambwa tendewa huchukua **KN³**. Katika Kiswahili Sanifu mpangilio wa virai nomino vya yambwa huwa huru na yambwa yoyote huweza kutangulia, kwa mfano:

53. **a. Nilimpikia chakula Juma.**

**b. Nilimpikia Juma chakula.**

**c. Badri alimwandikia barua Ahmed.**

**d. Badri alimwandikia Ahmed barua.**

Kitenzi ambacho huwa kwenye sentensi zenye yambwa mbili huwa kinabeba viambishi vinavyowakilisha yambwa hizo. Kutokana na kitenzi ndipo tunapata mpangilio kamili wa yambwa, kuwa yambwa tendwa ndiyo hutangulia baada ya kitenzi ikifuatwa na yambwa tendewa. Pasi na kuangalia vitambulishi vya yambwa katika kitenzi, tunapata kuwa kipashio cha yambwa tendwa au yambwa tendewa huweza kuhamishwa ili kutambulisha mada katika kishazi au usemi. Kwa mfano:

54. **"Mtengenezeeni nafasi huyu mwenzenu," yule kijana aliwaambia wale waliokuwa wameketi katika mstari huo.** **(Shafi 1979:73)**

Kutokana na kauli hii tunapata kuwa mada kwenye yambwa tendwa au yambwa tendewa hutiliwa mkazo na jinsi uamilifu wa mbinu zinazotumiwa kusimba mada zilivyopangwa katika matini. Katika mfano huu, kishazi, '*mtengenezeeni nafasi huyu mwenzenu*'

kinabeba yambwa mbili: yambwa tendwa, *huyu mwenzenu* na yambwa tendewa, *nafasi*. Bila kufuata mpangilio wa maneno unaochukuliwa kuwa wa kawaida, kauli hii inaweza kuwa na miundo ya sentensi ifuatayo:

**55. a. Mtengenezeeni nafasi huyu mwenzenu.**

**b. Mtengenezeeni huyu mwenzenu nafasi.**

**c. Mtengenezeeni mwenzenu huyu nafasi. N.k**

Kulingana na mifano hii yambwa tendwa huweza kuhamishwa ikachukua nafasi ya yambwa tendewa na yambwa tendewa nafasi ya yambwa tendwa. Ikumbukwe kuwa mpangilio wa maneno huwa na nafasi muhimu katika kuipa hadhi yambwa tendwa kulingana na usifa bia kati ya lugha. (Givon,.2001:269). Kipashio ambacho hubeba taarifa muhimu hutangulizwa kabla ya kile kingine kati ya yambwa tendwa na yambwa tendewa. Ikiwa yambwa tendewa ndiyo inayobeba taarifa muhimu itatangulia baada ya kitenzi huku ikifuatwa na yambwa tendewa, na kinyume chake. Kwa hivyo mwandishi au msemaji ana uhuru wa kutanguliza au kuhamisha yambwa kutegemea umuhimu wa taarifa anayotaka kuwasilisha. Katika kauli hii, '*mtengenezeeni nafasi huyu mwenzenu*', mada ambayo inabebwa na kauli hii ni *nafasi* ambayo kiongozi wa kundi anawaomba wafanyakazi wengine wamtengenezee Rashidi. Kauli hiyo hiyo kama ingekuwa '*mtengenezeeni mwenzenu huyu nafasi*', basi viambajengo '*mwenzenu huyu*' ndivyo vingekuwa mada katika usemi huo.

Givon (2001:270) anaeleza kuwa mpangilio wa maneno ni kanuni inayobainisha kutanguliza yambwa tendwa ambayo hubeba mada yenye taarifa muhimu kabla ya

yambwa tendewa ambayo inabeba taarifa isiyo muhimu kwa wakati huo. Kirejelewa ambacho ni muhimu katika sentensi au kishazi ndicho ambacho hutangulia kama vile:

**56. a. Alikata mti kwa shoka.**

**b. Alitumia shoka kukatia mti.**

Katika (**56a**) kiambajengo *mti* ndicho kinachobeba mada ya kauli kama yambwa tendwa na ndiyo taarifa muhimu na hapo hutangulia yambwa tendwa. Katika (**56b**). *shoka* ndicho kiambajengo muhimu na kina uamilifu wa yambwa tendewa na pia ndicho mada ya usemi huo.

Kulingana na Vitale (1981:130). Kiswahili ni lugha ambayo inaweza kupanga yambwa kwa kutumia muundo huru hata kama ule unaokubalika ni wa yambwa tendewa - yambwa tendwa. Kwa kuwa kitenzi hubeba viambishi vinavyowakilisha yambwa. mpangilio wa maneno unapobadilishwa. virejelewa vya yambwa vinapohama huhama pamoja na uamilifu wake. iwe ni tendwa au tendewa. Kwa mfano:

**57. "Unaweza kuielezea mahakama vipi mshtakiwa alianzisha fujo hiyo?"**

**(Shafi 1979:193)**

Katika kitenzi **ku-i-elez-e-a**, kiambishi {–i-} kinawakilisha kiambajengo *mahakama*, nacho kiambishi kifuatilizi {–e-} kinawakilisha maelezo yatakayotolewa. Kwa kuwa mada au taarifa muhimu katika usemi inahusu *nani*. basi kiambajengo kinachotangulia ni mahakama, kama yambwa tendwa. Lakini kama mada ya kauli hii ingekuwa inahusu *nini*. basi kiambajengo ambacho kingetangulia kingetarajiwa kueleza jinsi mshtakiwa

alivyoanzisha fujo bila kuzingatia ni akina nani waliokuwa wakisikiliza, kwa mfano:

**58. "Unaweza kuieleza vipi mshtakiwa ..........**

Kwa muhtasari, tunaweza tukasema kuwa kulingana na virejelewa ambavyo vimetangulia katika diskosi kwa mujibu wa mfano ulio hapo juu, mambo ambayo yangeelezwa na Bwana William kuhusu yaliyotokea bandarini yalikuwa yasikizwe na mahakama. Hivyo basi, mahakama ndiyo mada ya usemi huu ambayo ina uamilifu wa yambwa tendwa.

## 3.6 Hitimisho

Katika sura hii, tumeshughulikia tungo ambazo hutumika katika kutambulisha mada katika Kiswahili Sanifu. Tumeshughulikia utambulishaji wa mada katika kiwango cha kirai na kishazi katika muktadha wa diskosi. Tumechanganua jinsi mada hutangulizwa katika tungo, kuhamishwa kushoto, kuhamishwa kulia na kuhamishwa kwa yambwa. Utambulishaji wa mada katika sentensi za Kiswahili zenye muktadha wa diskosi hutegemea sana mpangilio wa maneno ambao katika Kiswahili Sanifu huwa huru kwa kiasi.

Tatizo moja kwa mujibu wa Lambrecht (1994) linalohusu uainishaji wa mpangilio wa maneno ambao ni bia ni kuwa maelezo mengi hayazingatii tofauti za muundo wa taarifa kati ya lugha tofauti tofauti kama vile muundo wa taarifa kwenye viwakilishi dhidi ya usimbaji wa maneno, mada dhidi ya fokasi n.k kama inavyojitokeza katika uchanganuzi wetu.

Uchanganuzi wetu wa data umetubainishia kuwa kwa kufuata viwango tulivyotumia vya utambulishaji wa mada. na labda kwa kutumia viwango/vigezo vingine ambavyo hatujatumia. tunapata kuwa mada huweza kutambulishwa katika kiwango cha kirai na kishazi pamoja na kategoria za kileksika katika sentensi.

# SURA YA NNE

# TUNGO ZENYE KUTAMBULISHA FOKASI

## 4.1 Utangulizi

Katika sura ya tatu, tumejikita katika uchanganuzi wa tungo ambazo hutambulisha mada katika Kiswahili Sanifu. Tumebainisha kuwa mada huweza kutambulishwa kama neno, kirai au kishazi katika sentensi za Kiswahili Sanifu. Katika sura hii, tutashughulikia uchanganuzi wa tungo ambazo hutambulisha fokasi. Aidha, tutashughulikia aina za fokasi tukiegemea jinsi fokasi inavyotambuliswha katika kiarifu, kishazi, virai na katika neno.

Pia tutaangalia jinsi fokasi huhama katika ukanushaji wa kauli. Vilevile, tutachanganua maswali yanayohitaji majibu ya Ndiyo/La na pia maswali yanayohitaji maelezo katika majibu ili kutoa ufafanuzi wa utambulishaji wa fokasi katika tungo hizi. Hali kadhalika, tutashughulikia fokasi linganuzi na uhamisho wa fokasi kushoto.

## 4.2 Aina Za Fokasi

### 4.2.1 Fokasi Katika Kiarifu

Hii ni aina ya fokasi ambayo huwiana na aina tatu za majukumu ya mawasiliano: kutambulisha kirejelewa, kutoa ufafanuzi kuhusu mada na kutoyapa kipaumbele matukio au kuwasilisha kirejelewa kipya katika diskosi. Fokasi ambayo hutambulishwa katika

kiarifu huwa na jukumu la kutambulisha au kufafanua zaidi kuhusu kiima na huwa haipewi msisitizo katika kauli, (Van Valin na La Polla, 1997:206). Ni aina ya fokasi ambayo hutambulisha mada katika uchukulio wa kipragmatiki ambapo kirai-kiarifu hutoa ufafanuzi kuhusu mada. Kwa mfano:

**59. Swali: Gari lako limefanya nini?**

**Jibu: Gari langu / limeharibika.**

Katika swali letu hapo juu, uchukulio tunaoupata ni kuwa mada ya swali hili ni *gari lake msikilizaji*, na ni kutokana na uchukulio huu tunapopata jibu. Dai huwa ni utokeaji wa mahusiano kati ya mada na hali ya matukio ambayo yanarejelewa na kiarifu, na dai katika kauli hii ni *limeharibika*, (Lambrecht, 1994:226). Muundo wa taarifa tunaoupata katika mfano wa **(59)** huweza kuwasilishwa ifuatavyo:

| | |
|---|---|
| **Sentensi:** | **Gari langu limeharibika.** |
| **Uchukulio:** | **Gari la msemaji.** |
| **Dai:** | **X = limeharibika.** |
| **Fokasi:** | **limeharibika.** |
| **Mawanda ya fokasi:** | **Kitenzi pamoja na viambajengo vinavyokifuata. (ikiwa vipo)** |

Kama tulivyotaja hapo katika sura ya tatu, mada hutambulishwa au hulinganishwa na kiima katika sentensi, lakini hili hutegemea muundo wa sentensi na sio kila wakati ambapo kiima hutambulisha mada katika sentensi. Kiarifu kulingana na mtazamo huu hutambulisha fokasi, kama vile:

**60. Salum alimwambia Rashidi, "Leo Chaani kweupe."**

**"Kuna nini?" Rashidi aliuliza**

**"Kuna Beni mbili, taarabu na Maumbwa." Alijibu Salum. (Shafi, 1979:101)**

Kulingana na kauli hii, mada inarejelea mahali panapoitwa *Chaani* ambapo Salum angetaka wapatembelee akiwa pamoja na Rashidi. Katika swali la Rashidi, "*Kuna nini?*" mahali pale panawakilishwa na kiambishi cha mahali *ku*-katika kitenzi *kuna*. Kwa hivyo, mada inawakilishwa na kiambishi kitangulizi katika kitenzi. Katika jibu la Salum, anaanza kauli yake kwa kutumia kitenzi ambacho kinabeba kiambishi kinachowakilisha mada. Sehemu nyingine ya sentensi inayofuata ni kiarifu chake na ndicho ambacho ni fokasi ya sentensi hiyo. Viambajengo vyote, yaani kitenzi na vingine ambavyo vinatajwa baada yake, viko kwenye mawanda ya fokasi, kama vile:

**"Kuna Beni mbili, taarabu na Maumbwa."**

Muundo wa taarifa kutokana na diskosi hii ni kama ifuatavyo:

| | |
|---|---|
| **Sentensi:** | **Kuna beni mbili, taarabu na Maumbwa.** |
| **Uchukulio:** | **Chaani, mahali panapozungumziwa.** |
| **Dai:** | **X = kuna Beni mbili, taarabu na Maumbwa.** |
| **Fokasi:** | **Beni mbili, taarabu na Maumbwa.** |
| **Mawanda ya fokasi:** | **Kitenzi na viambajengo vinavyofuata.** |

Fokasi kwenye kiarifu huweza kukosa kupewa msisitizo au kukosa kutambulishwa hata kama inabeba taarifa mpya. Viarifu hata hivyo huweza kupewa msikiko hata kama vinatajwa kwa mara ya pili katika sentensi. (Lambrecht, 1994:227). Kiarifu hujumlishwa na kitenzi pamoja na viambajengo vingine ambavyo hufuata kitenzi. Kwa mfano:

61. **"He! Unasoma saa ngapi? Alfajiri unakwenda kazini na hurejei mpaka magharibi, sasa huko masomoni unakwenda saa ngapi?" Faki aliuliza kwa mastaajabu.** **(Shafi, 1979:76)**

Kutokana na usemi huu tunapata kuwa kitenzi *unakwenda* kinapewa msisitizo wa fokasi kwa kuwa kimerudiwa kwa mara ya pili katika KT. *unakwenda saa ngapi?* Ingawa kitenzi hiki kina uhusiano na KT *unakwenda kazini* katika sehemu ya kwanza ya sentensi hiyo, haingefaa kuweka msisitizo wa fokasi katika kiambajengo kingine kipya katika kauli hii kama vile *masomoni*, hata kama ndicho kinachobeba taarifa mpya na muhimu kwenye kauli.

Hali ya kupatia au kutopatia fokasi msisitizo au kutoitambulisha katika kauli hutegemea sana muktadha wa mazungumzo kati ya msemaji na msikilizaji.

### 4.2.2 Fokasi katika Sentensi

Lambrecht (1994:233) anaeleza kuwa fokasi katika sentensi huwa ni aina ya fokasi ambayo hutoa taarifa au huwasilisha taarifa kuhusu tukio fulani. Fokasi katika sentensi hujumlisha kiima na kiarifu lakini huwa si sehemu ya elementi zozote zinazotambulisha mada. Katika tungo za aina hii, sentensi nzima huwa kwenye mawanda ya fokasi, hivi kwamba sentensi haitambulishi mada. Sentensi hii haibebi uchukulio wowote wa kipragmatiki. Kwa mfano:

**62. Swali: Kulitokea nini?**
**Jibu: Gari langu limeharibika.**

Jibu linalotokana na swali hapo juu halibebi uchukulio kamwe na kuwa dai au fokasi hupatana huku mawanda ya fokasi yakiwa ni sentensi nzima, kama vile:

**Sentensi:** Gari langu limeharibika.

**Uchukulio:** ------------------

**Dai:** Gari la msemaji limeharibika.

**Fokasi:** Gari la msemaji limeharibika.

**Mawanda ya fokasi:** Sentensi.

Tungo ambazo sentensi hutambulisha fokasi huwa hazina uchukulio wa kipragmatiki isipokuwa tu kwenye sifa nyingine za kauli zenye kutambulisha fokasi kwenye kiarifu hicho na ambazo hazitokei katika othografia bali katika hali ya utambuzi. Kwa mfano:

63. **"Sasa cha mno nini tena?"**

**"Ah, mwenzetu mmoja ameumia sana leo kazini na sijui hali yake namna gani hivi sasa."** (Shafi 1979:7)

Kutokana na usemi huu, tutasema kuwa uchukulio ni kuwa kuna kitu ambacho kimetokea pale bandarini kati ya wafanyakazi. Hata hivyo, uchukulio wa aina hii umedokezwa tu kihali wala sio katika sarufi leksika. Katika sentensi ambapo fokasi hutambulishwa, kilicho wazi ni kuwa hakuna kiima ambacho ni mada au uchukulio unaorejelea hali iliyotokea. Kwa kuwa dai liko kwenye sentensi nzima, basi dai na fokasi zinalingana kwenye utungo. Kutokana na ukosefu wa uchukulio tunapata fasiri ya tukio hili kama ifuatavyo:

**Sentensi:** 'Ah, mwenzetu mmoja ameumia sana leo kazini na sijui hali yake namna gani hivi sasa'.

**Uchukulio:** ----------------------

**Dai:** Msemaji ana mwenzake aliyeumia sana.

**Fokasi:** Msemaji ana mwenzake aliyeumia sana.

**Mawanda ya fokasi:** Sentensi.

Mawanda ya fokasi huchukua elementi ambazo pia si fokasi kama vile katika kiambajengo *mwenzetu.* Kulingana na mfano huu, kiambishi *–tu* katika *mwenzetu* sio sehemu ya fokasi bali sehemu ya mada kwa kuwa kinamrejelea msemaji, Majaliwa, na wafanyakazi wenzake. Hali kadhalika, kauli, *'mwenzetu mmoja ameumia sana leo kazini na sijui hali yake namna gani hivi sasa'*, sio sehemu ambayo ni mada ya sentensi na hii ni sifa mojawapo inayobainisha tungo zenye fokasi katika kishazi.

Van Valin na La Polla (1997:207) wanaeleza kuwa kishazi au sentensi inayotambulisha fokasi hukosa uhusiano wa mada-kiarifu kati ya kirejelewa kinachosimbwa na kiima, na kauli inayofafanuliwa na sentensi, yaani tamko halitumiwi kufafanua kirejelewa. Ukosefu wa uchukulio kwenye kauli hufanya dai kuwa na uamilifu unaolingana na wa fokasi. Tungo ambazo hutambulisha fokasi kwenye sentensi kwa kawaida hutumika katika hali za uwasilishaji, katika kuwasilisha hali au tukio jipya au kirejelewa kipya au vyote viwili. Kwa mfano:

**64. a. Batu: [*Akiingia uwanjani*] Mtukufu Mtemi atafika hivi punde. Waiteni watu.**

**b. Hapo zamani za kale miongoni mwa Wajaluo paliishi shujaa (aliyesifika sana).**

**c. Alhamdulillah! Nyoka kaingia chumbani!**

Tungo ambazo hutambulisha fokasi katika sentensi huwa na sifa moja kuu ya kutambulisha kiima kama kiambajengo ambacho hakitambulishi mada. Mifano **(64a)**, **(64b)** na **(64c)** inadhihirisha hali hii. Kiambajengo hiki au kiima hakitambulishi mada iwe ni kwa njia ya arudhi, kimofolojia au kisintaksia. Kwa kuwa utambulishaji wa mada

katika kiima hubainisha kigezo cha muundo wa mada-kiarifu usiotambulishwa. sentensi **(64a)**, **(64b)** na **(64c)** huweza kupewa sifa zinazokosa muundo wa kutambulisha fokasi kwenye kiarifu. Kwa mfano msemaji anapotamka: *Alhamdulillah! Nyoka kaingia chumbani!* Usemi huu ni taarifa mpya ambayo inaingizwa katika diskosi kwa mara ya kwanza. Kwa hivyo, vishazi hivi vinatambulisha fokasi kwa ukamilifu kinyume na jinsi tunavyopata kiarifu peke yake kikiwa kitambulishi cha fokasi katika sentensi. Huenda msemaji au msikilizaji wa kauli hii hakutarajia kumuona nyoka akiingia chumbani. Msemaji anashangaa na kushtuka na hivyo basi kutamka maneno hayo kwa ghafla. Hizi ni aina za vishazi ambavyo havibebi uchukulio na kama tulivyotaja awali, dai na fokasi huwa na ulinganifu sawa.

### 4.2.3 Fokasi kwenye Kirai Nomino

Katika miundo ya aina hii ya sentensi, fokasi hutambulishwa kwenye KN cha kauli wazi ambacho hubeba uchukulio. Kwa mfano.

**65. "Nani tapeleka yeye hospitali?" Yule Mzungu aliuliza**
**"Gari ya kampuni si ipo?" Wote waliopo pale walisema kwa umoja wao.**
**(Shafi 1979:6)**

Kutokana na usemi huu, uchukulio unaotolewa kwenye jibu ni kuwa wafanyakazi wanaamini kuwa kuna njia fulani ambayo inaweza kutumika kumfikisha yule mfanyakazi aliyeumia hospitalini. Hii ndiyo sababu wafanyakazi wanatoa jibu la pamoja na kusema.

**"Gari ya kampuni si ipo?"**

Dai linalotokana na kauli hii ni kuwa njia ambayo wafanyakazi walitarajia itumike ni kuwa gari la kampuni lilikuwa pale kuwatumikia wote katika bandari. Mkazo unawekwa

kwenye KN. *gari la kampuni* kama fokasi ya kauli hii. Tunaweza kutolea usemi huu muhtasari ifuatavyo:

| | |
|---|---|
| **Sentensi:** | **Gari ya kampuni si ipo?** |
| **Uchukulio:** | **Kuna njia ambayo wafanyikazi waliamini kuwa ingetumika kumpeleka mfanyikazi aliyeumia hospitalini.** |
| **Dai:** | **X = gari ya kampuni** |
| **Fokasi:** | **Gari ya kampuni.** |
| **Mawanda ya fokasi:** | **KN** |

Mawanda ya fokasi katika usemi huu yako kwenye KN kuliko kuwa kwenye nomino pekee. Hii ni kwa sababu mawanda ya fokasi hujikita kwenye kategoria za virai na siyo kwenye kategoria za maneno yaliyojisimamia pekee. KN kinachosisitizwa na ambacho kinaelezwa si *gari* nyingine yoyote bali *gari ya kampuni.*

Kwa kurejelea kauli hii tena. *gari ya kampuni si ipo?. tunapata* kuwa. dhihirisho la kauli *X si ipo* sio tu kuwa ina uchukulio unaotarajiwa kuwa unajulikana na msikilizaji lakini kuwa imetambulishwa kama ambayo inatumika katika diskosi.

Lambrecht (1994:229). anaeleza kuwa usemi huchanganuliwa kwa kufuata mtazamo wa hali ya mawasiliano ambapo ulitamkwa. Kwa mfano. tukirejelea tena usemi wetu hapo juu. tunapata kuwa Mzungu na wafanyakazi wanaelewa kuwa sio tu kuwa ipo njia ya kumpeleka mfanyakazi aliyeumia hospitalini lakini huenda kukawa na uwezekano wa Mzungu na wafanyakazi kufikiria kuwa njia zingine zingepatikana za kumpeleka yeye hospitalini kama vile kwa kutumia baiskeli. kumbeba au njia nyingine yoyote. Dai

linalotokana na kauli hii ni kuwa, siyo tu utambulishaji wa *X* na njia itakayotumiwa na wafanyakazi kumpeleka mfanyakazi hospitalini, bali pia kutolea lawama kile anachokiamini msikilizaji au kumpa msikilizaji njia halisi ambayo msemaji anafikiria wakati wa mazungumzo.

Katika mazungumzo hayo kati ya Mzungu na wafanyakazi, Mzungu alitarajia kuwa wafanyakazi wangetafuta njia zao za kumpeleka mfanyakazi aliyeumia nyumbani, lakini wao walionelea kuwa njia iliyofaa zaidi ilikuwa ni kutumia *gari ya kampuni* iliyomilikiwa na kampuni ya bandarini.

Katika Kiswahili Sanifu, KN kinachodhihirisha utokeaji wa fokasi kati ya viambajengo vingine katika sentensi ndicho tu hupewa msisitizo. Kwa hivyo, kutambulisha fokasi kwenye KN huweza kuchukuliwa kama kinyume cha utambulishaji wa fokasi kwenye kiarifu.

Katika uchanganuzi huu, dhana ya tungo ambazo hutambulisha fokasi kwenye KN zimetumika kurejelea tungo za sentensi ambazo viambajengo vyake huwa na uamilifu wa KN katika kiwango cha kisemantiki. Tungo hizi hutumika kama sehemu ya fokasi katika kiwango cha muundo wa taarifa.

### 4.2.4 Fokasi Finyu

Van Valin na La Polla (1997:208) wanaeleza kuwa tungo ambazo zina fokasi finyu huwa zinatambulisha fokasi kwenye kiambajengo kimoja tu katika kishazi na huweza kuwa kiima, kitenzi, yambwa au KN kisicho wazi. Kwa mfano:

**66. Swali: Nilisikia kuwa kalamu yako iliibiwa.**

**Jibu: Mfuko wangu ndio ulioibiwa.**

Katika usemi wa **(66)**, kauli inayosema kuwa kuna kitu cha msikilizaji ambacho kiliibiwa ni sehemu ya uchukulio wa kipragmatiki. Dai ni kuwa, *ni mfuko wa msikilizaji ulioibiwa* nayo fokasi ni *mfuko*. Mawanda ya fokasi yako kwenye KN kizima, *mfuko wangu*. Hapa mawanda ya fokasi yamejikita kwenye KN na fokasi ni *mfuko* ambacho ni kiambajengo ambacho kiko kwenye mawanda ya fokasi. Viambajengo hivyo vingine vyote katika sentensi vinajulikana na huwa vinabeba taarifa inayojulikana na ndiyo mada ya sentensi huku *mfuko* ukiwa kiambajengo chenye taarifa mpya.

UNIVERSITY OF NAIROBI
EAST AFRICANA COLLECTION

Kwa upande mwingine, jibu ambalo lilitolewa lingetokana na swali:

**Ni kitu gani kati ya kalamu na mfuko kilichoibiwa?**

Kutokana na swali hili, tunapata kuwa taarifa mpya kwenye fokasi sio kiambajengo chenyewe lakini uwepo wa uhusiano kati ya kirejelewa na kauli yenye uchukulio kuwa '*kuna kitu cha msikilizaji kilichoibiwa*'. Katika utoaji wa taarifa mpya inayosema kuwa ni *mfuko wa msikilizaji ulioibiwa*, uhusiano huu ndio hukifanya kiambajengo kinachotambulisha fokasi kuwa arifu na sio hadhi ya kutanguliza kirejelewa upya au la.

Kwa mfano;

**67. "Mlipofika gatini wewe na askari wako mlikuta fujo yoyote?"**

**...............................**

**"Watu walikuwa wakifanya ghasiya" alijibu William.**

Kwa kufuata mfano huu tunaweza kutoa muhtasari wa jibu linalotolewa na William kama ifuatavyo;

| | |
|---|---|
| **Sentensi:** | **Watu walikuwa wakifanya ghasia.** |
| **Uchukulio:** | **Watu walikuwa wakifanya X.** |
| **Dai:** | **X= ghasiya** |
| **Fokasi:** | **ghasiya** |
| **Mawanda ya fokasi:** | **KN** |

Kutokana na usemi huu, kama swali lingekuwa tofauti na lilivyo, fokasi ingekuwa kwenye kiambajengo kingine mbali na *ghasiya*. Fokasi huweza kutambulishwa kwenye viambajengo vingine kama ifuatavyo:

**68.** ***Swali:*** ***Nani walikuwa wakifanya ghasiya?***

***Jibu:*** ***Watu walikuwa wakifanya ghasiya.***

***Swali:*** ***Watu walikuwa wakifanya nini?***

***Jibu:*** ***Watu walikuwa wakifanya ghasiya.***

***Swali:*** ***Watu walikuwa na nini?***

***Jibu:*** ***Watu walikuwa wakifanya ghasiya***

### 4.3. Fokasi katika Ukanushaji

Katika sehemu hii tutashughulikia ukanushaji wa kawaida unaotokea katika sentensi finyu na za kimsingi. Sentensi za aina hii huwa zenye vishazi vikuu na huwa na kiarifu kimoja chenye virai nomino na vielezi vumishi vichache iwezekanavyo. (Payne. 1985:198). Tutajikita katika jinsi fokasi huhama kutoka nafasi moja hadi nyingine katika sentensi wakati kauli fulani inapokanushwa.

Sifa moja ya ukanushaji wa kawaida ni welekeo wake unaojihusisha na elementi zenye kutambulisha fokasi katika sentensi. (Jackendoff. 1972 katika Payne. 1985:232). Katika Kiswahili Sanifu. kiambajengo ambacho kinakanushwa hupewa msisitizo zaidi kuliko viambajengo vingine. Kuna njia mbili za ukanushaji katika Kiswahili Sanifu: kwanza ni kwa kukanusha kitenzi kikuu ambacho huweza kubeba ukanushaji wa kiambajengo kingine katika sentensi. kama vile.

**69. a. Maria alichelewa kufika shuleni.**

**Maria <u>ha</u>kuchelewa kufika shuleni.**

Katika kitenzi *hakuchelewa*, tunapata kuwa kinaweza kuwa kinasimamia ukanushaji wa:

**b. Maria hakuchelewa, au**

**Maria hakuchelewa kufika, au**

**Maria hakuchelewa kufika shuleni.**

Pili ni kwa kutumia mbinu ya kisintaksia ya kuhamisha kushoto kiambajengo kinachokanushwa na kukitanguliza kwa kutumia kikanushi *Si*, kama vile:

**70. a. Maria alichelewa kufika shuleni.**

Katika ukanushaji tunapata kauli zifuatazo:

**b. Si Maria aliyechelewa kufika.shuleni, au**

**Si shuleni Maria alichelewa kufika, au**

**Si kuchelewa kufika shuleni kwa Maria, bali -------------------**

Wataalamu Van Valin na La Polla (1997:219) wanaeleza kuwa muundo wa fokasi huhusishwa katika fasiri ya ukanushaji. Tangu enzi za Russel (1905), wanasema kuwa imependekezwa kuwa katika tamko, sehemu inayodaiwa ndiyo tu ambayo hupitia ukanushaji na sehemu yenye uchukulio haikanushwi. Sehemu ya sentensi ambayo hufasiriwa kuwa imekanushwa kwa kawaida huwa kwenye mawanda ya ukanushaji, kama vile:

**71. "Mie sikwenda huko pwani kucheza ----------------" (Shafi 1979:21)**

Kutokana na kauli hii, fasiri ya ni kiambajengo kipi kinachokanushwa hubainishwa na muundo wa fokasi katika sentensi kama ilivyo kwenye kiimbo. Kwa mfano, tunaweza tukasema:

a. **MIE sikwenda huko pwani kucheza -------.** *(Mtu mwingine ndiye aliendа)*
b. **Mie SIKWENDA huko pwani kucheza ----.** *(nilifanya kitu kingine)*
c. **Mie sikwenda HUKO PWANI kucheza ------.** *(nilikwenda mahala pengine)*
d. **Mie sikwenda huko pwani KUCHEZA ----.** *(nilikwenda kufanya kitu kingine)*
e. **MIE SIKWENDA HUKO PWANI KUCHEZA ------.** *(sikutoka kamwe)*

Tukitazama kauli zilizopo hapo juu tunapata kuwa kauli **(a) - (d)** zimejikita kwenye fokasi finyu kwa kuwa ukanushaji upo tu kwenye kiambajengo kimoja. Nayo kauli ya **(e)** iko kwenye ukanushaji mpana kwa kuwa kishazi kizima kinapitia ukanushaji. Kiambajengo ambacho hutambulisha fokasi hufasiriwa kama kiko kwenye mawanda ya

ukanushaji na sehemu nyingine ya sentensi huwa ni yenye uchukulio. Kauli ya **(e)** ikiwa kwenye fokasi pana ni aina ya utungo wenye kutambulisha fokasi katika kiarifu na hivyo kirai kizima cha kiarifu kinapitia ukanushaji.

Katika vishazi ambavyo ni arifu yakinishi kaida za ukanushaji na zenye welekeo fulani hufuatwa kwa kuwa kila elementi ya hiari inayotajwa katika kishazi huwa fokasi ya taarifa inayodaiwa. (Givon 2001:230). Hali hii huwa tofauti pale ambapo tunapata kishazi kilichokanushwa na ambacho hukosa kiambajengo maalum, kama vile katika kauli:

**72. Kamau hakununua gari. (gari halikununuliwa)**

Kwa kuwa kauli hii haibebi kiambajengo cha hiari. kijalizo kizima ndicho kinachotambulisha fokasi na hivyo kupata fasiri tofauti kuwa Kamau alifanya kitu tofauti kabisa na ununuzi wa gari. Kwa hivyo, tukio la kununua gari halikutokea kamwe. Ikiwa kauli hii inaweza ikatamkwa bila kutumia mkazo linganuzi. KT chote hivyo basi kitakuwa kwenye mawanda ya ukanushaji.

Tunapopata kishazi chenye kiambajengo cha hiari tutapata mabadiliko tofauti na ilivyo hapo awali. Mawanda ya dai lililokanushwa litakuwa finyu ili kutojumlisha viambajengo vingine vyote isipokuwa tu kile cha hiari. Kwa mfano:

**73. a. Askari hakumuua mhalifu kusudi.** *(ilikuwa ni ajali)*

**b. Askari hakumuua mhalifu Jumamosi.** *(alimuua siku nyingine).*

**c. Askari hakumuua mhalifu vichochoroni.** *(lakini kwingine).*

**d. Askari hakumuua mhalifu kwa bunduki.** *(lakini kwa kisu).*

**e. Askari hakumuua mhalifu kwa hasira.** *(lakini kwa utaratibu).*

Kauli hizi **(73a) - (73e)** zinabeba viambajengo vya hiari ambavyo hukanushwa na huleta ulinganuzi na kitenzi cha kishazi hicho. Tunapata kuwa, Askari kwa kweli alimuua mhalifu lakini hakumuua kutokana na sababu zilizotolewa na viambajengo vya hiari, bali kutokana na sababu zingine tofauti. Kwa hivyo ukanushaji ni aina ya vitendo usemi ambavyo huleta kinyume cha hali ilivyo wakati wa tamko.

Tunapoangalia kwenye vishazi ambavyo hukosa viambajengo vya hiari, tunapata kuwa ulinganuzi wa ukanushaji huwa na mawanda mapana. Kwa kutumia kauli kama hizi tunapata kuwa kiambajengo chochote katika kishazi kinaweza kikakanushwa. Kwa mfano:

**74.** **a. Askari hakumuua mhalifu KUSUDI.** (*ilikuwa ni ajali)*

**b. ASKARI hakumuua mhalifu kusudi.** *(lakini mtu mwingine*)

**c. Askari HAKUMUUA mhalifu kusudi.** *(alimfanyia kitu kingine)*

**d. Askari hakumuua MHALIFU kusudi.** *(alimuua mtu au mnyama mwingine)*

Hali kadhalika, wakati ukanushaji unapotokea katika kishazi ambacho hakina kiambajengo cha hiari, tunapata kuwa kiambajengo chochote katika kishazi hicho huweza kutambulisha fokasi katika ukanushaji linganuzi, kama vile:

**75.** **a. ASKARI hakumuua mhalifu.** *(lakini mtu mwingine)*

**b. Askari HAKUMUUA mhalifu.** *(alimfanyia kitu kingine)*

**c. Askari hakumuua MHALIFU.** *(lakini mtu au mnyama mwingine)*

Kutokana na uchanganuzi huu tunapta kuwa kiambajengo ambacho hupitia ukanushaji ndicho huvuta au hutumika kutambulisha fokasi katika sentensi. Kiambajengo hiki ndicho hubeba taarifa moja na muhimu katika usemi na ndiyo sababu hukanushwa na

vingine kubakia katika hali yakinshi. Ikiwa taarifa mpya inabebwa na kishazi kizima, basi kauli yote yakinishi huweza ikakanushwa na kutumika kutambulisha fokasi.

## 4.4 Fokasi katika Tungo Za Maswali ya Majibu ya Ndiyo/La

Fokasi huweza kutambulishwa katika tungo za maswali yanayohitaji majibu ya ndiyo au la. (Givon, 2001:231). Ni njia moja ya kufinya mawanda ya majibu ya ndiyo au la na utokeaji wa fokasi linganuzi. Tunapopata vishazi vyenye Virai Nomino vya lazima, mawanda ya maswali yanayohitaji majibu ya ndiyo/la huwa yako wazi na huweza kuchukua KT kizima kikiwemo kiima, kwa mfano:

| | |
|---|---|
| **76. a. Kiongozi wa mashtaka:** | **"Kwa hivyo unaihakikishia mahakama kwamba mshtakiwa ndiye aliyeanzisha fujo hiyo?"** |
| **Bw. William:** | **"Ndiyo"** |
| **b. Rashidi:** | **"Ulipokuwa afisini kwako ulipata simu na uliyezungumza naye alikwambia gatini kuna fujo?"** |
| **William:** | **"Ndiyo"** **(Shafi, 1979:194)** |

Kutokana na maswali ya **(76a)** na **(76b)**, tunapata kuwa mawanda ya swali yanajumlisha sehemu nzima ya kishazi na ndiyo sababu Bw. William hana budi kutoa jibu la *ndiyo* kila wakati bila kutoa ufafanuzi wowote. Pia jibu laweza kuwa *la* kama vile:

**77. Swali: Askari alimuua mhalifu? (mhalifu aliuawa?)**
**Jibu: La.**

Pia, pale ambapo kiambajengo cha hiari kinapowekwa kwenye kishazi, fokasi ambayo hutambulishwa na maswali ya majibu ya ndiyo/la hutokea hata kama hakuna ulinganuzi wowote, kama vile:

**78. b. Swali: Juma alimkimbiza mbwa?**
**Jibu: Ndiyo/La**

**b. Swali: Mtoto alimlilia mamake?**
**Jibu: Ndiyo/La**

**c. Swali: Ulimpata Hamisi akivunja dirisha?**
**Jibu: Ndiyo/La**

Kutokana na mifano **(78a) – (78c)**, tunapata kuwa pale ambapo maswali yanayohitaji majibu ya ndiyo/la yanatumiwa katika kishazi chenye kiambajengo cha hiari, utambulishaji wa fokasi hutokea kwa njia mbili: kwanza katika kubana fokasi ya dai au swali ili lilenge kiambajengo cha hiari, na pili ni katika kuwekea mpaka fokasi linganuzi kwenye fokasi ya dai.

Aidha, tunapopata kishazi ambacho hakina kiambajengo cha hiari kinacholengwa katika swali, fokasi linganuzi hutokea kwenye kiambajengo chochote, kwa mfano:

**79. a. HASSANI alimchinja mbuzi? (au ni mtu mwingine?)**

**b. Hassani ALIMCHINJA mbuzi? (au alimpeleka malishoni?)**

**c. Hassani alimuua MBUZI? (au ni ng'ombe)**

Fokasi katika tungo za maswali ya majibu ya ndiyo/la huwa imetambulishwa kwenye kishazi kizima ambacho hubeba taarifa mpya. Swali ambalo huulizwa huwa halina

uchukulio wowote na ndiyo sababu jibu lake huwa ni ndiyo/la. Katika maswali ya aina hii dai na fokasi huwa zimelingana na mawanda ya fokasi huwa kwenye kishazi kinachobeba swali.

## 4.5. Fokasi Katika Tungo za Maswali ya Majibu Yanayohitaji Maelezo

Lambrecht (1994:282) anaeleza kuwa matumizi ya kiulizi kinachobeba taarifa hufaa ikiwa kauli inayotokana na swali huwa na uchukulio wa kipragmatiki kwenye diskosi. Katika Kiswahili Sanifu viulizi kama vile nani, nini, wapi, n.k. hutumika. Kwa mfano:

**80. Nani alizichoma karatasi?**

Kutokana na swali hili, msemaji anachukulia kuwa msikilizaji anafahamu karatasi zilichomwa na kuwa anajua kuna mtu aliyezichoma karatasi hizo. Uchukulio hapa ni kuwa, *kuna mtu aliyezichoma karatasi*. Uchukulio tunaoupata kwanza unatokana na KN, *nani?*, huku wa pili ukitokana na kishazi kizima, *nani alichoma karatasi?* Dai kutokana na swali hili ni kuwa msemaji ana matarajio kuwa msikilizaji atamwambia ni nani aliyezichoma karatasi. Fokasi katika tungo kama hizi huwa ni fokasi finyu.

Katika maswali yanayohitaji maelezo katika majibu, uchukulio wa msemaji ni kwamba msikilizaji huwa anaelewa kirejelewa au mrejelewa na kuwa atatoa jibu kamili. Hata hivyo, uchukulio sio umaanisho unaoletwa na tungo za kisarufi zenye maswali yanayobeba taarifa lakini kaida ambayo hutokea katika aina zote za maswali kwa jumla. Kwa mfano:

**81. "Lo! Nani wale?" Rashidi alimuuliza ------------ (Shafi, 1979:11)**

Kutokana na kauli hii, *nani wale?* ina uchukulio kuwa wanaozungumziwa ni watu ambao wanaweza kutambulikana. Kwa hivyo, swali hili lina uchukulio kuwa watu hao wana kitambulisho cha *X* na kuwa msemaji anadai kujua hao watu ni akina nani. Msemaji hapa akiwa ni Rashidi na msikilizaji ni kijana mwenzake. Kwa kuwa kiulizi *nani?* ndicho kinachozua majibu yanayodaiwa katika uchukulio wa kauli wazi, kile kiambajengo ambacho huwa kwenye mawanda ya fokasi ni kiulizi chenyewe. Kwa hivyo maswali yanayohitaji maelezo katika majibu huwa ni mfano wa tungo zenye muundo wa KN-fokasi, kama vile:

| **Nani** | **wale?** |
|---|---|
| **KN** | **fokasi** |

Kutokana na mifano tuliyotoa hapo juu, tunaweza tukatoa ufafanuzi zaidi na kusema kuwa msisitizo upo kwenye viambajengo vya mwisho, *karatasi* na *wale*. Ni wazi kuwa msisitizo huu sio wa kutambulisha fokasi bali ni wa kuingiza jambo jipya katika diskosi. Tunapata kuwa virejelewa vya virai nomino, *karatasi* na *wale*, hata kama vinarejelewa na msikilizaji, bado havijatambulishwa kwenye akili yake wakati swali linapoulizwa. Pia vinaweza kuwa bado havijatangulizwa katika diskosi kama vitu ambavyo vinaweza kuuliziwa swali.

Ikiwa virejelewa hivi, *karatasi* na *wale*, vilikuwa vimetangulizwa katika diskosi kama mada, basi maswali yangekuwa:

*a.* **Nani alizichoma?** *Au*

**b. Nani wale? (bila kuwekea kiulizi *nani* msisitizo)**

Kwa hivyo, virejelewa *karatasi* na *wale* hutambulisha mada katika kauli hizi kwa kuwa vinadhihirisha virejelewa ambavyo vinatumika kutoa jibu au taarifa mpya. Kulingana na miundo tofauti ya sentensi, sio kawaida kupata kiambajengo kinachotumika kutoa taarifa kikitokea mwishoni mwa sentensi. Katika Kiswahili Sanifu kauli za maswali hupangwa kwa kufuata mpangilio huu, kama vile:

**82. "Mbona juzi umetwambia uwongo?"**
**"Uwongo GANI?"** **(Shafi 1979:188)**

Kiambajengo cha kiulizi kimetokea mwishoni mwa sentensi na ndicho kinachobeba taarifa mpya na vilevile kutambulisha fokasi. Kinachoulizwa katika swali hili na Rashidi ni kuwa, msemaji anatarajiwa kutoa ufafanuzi kwa kutumia maelezo katika jibu lake. Kwa hivyo, kiambajengo *uwongo* ni mada ya kauli hiyo na ni kirejelewa ambacho tayari kimetajwa na kutokea katika diskosi. Pia tuna maswali kama:

**83. a. Utaondoka saa NGAPI?**
**b. Mlikula NINI?**
**c. Ulikuwa unatoka WAPI?**

Katika tungo hizi **(83a)** – **(84c)**, fokasi imehamishwa kulia na kutambulishwa kwenye viulizi *ngapi?, nini?* na *wapi?*

Givon (2001:237) anaeleza kuwa kuna uhusiano imara wa kisintaksia kati ya fokasi linganuzi na maswali yanayodai majibu ya maelezo. Kama ilivyo katika fokasi linganuzi, maswali haya yanahusu kauli au kishazi ambacho kinabeba uchukulio kikiwa kizima isipokuwa tu kwenye kiulizi ambacho hubeba au hutambulisha fokasi. Kiambjengo hiki vilevile ndicho hubeba taarifa mpya ambayo hutangulizwa katika diskosi. Kwa mfano:

**84. Amina aliuliza, "Nani mwenzangu?"**

**"Mie Faraji"** **(Shafi 1979:60)**

## 4.6 Kuhamisha Fokasi Kushoto

Fokasi huweza kuhamishwa kushoto katika tungo kwa kuzitanguliza huku tukitumia kauli *ni* au *si*. Viambajengo ambavyo huweza kuhamishwa kushoto ni pamoja na kiima, yambwa, vivumishi, viwakilishi au hata vielezi. Tungo za aina hii hutoa msisitizo kwa kutambulisha mada au fokasi. Pia huwa zinagawa kishazi na kuwa sehemu mbili, kila sehemu ikibeba kitenzi chake. (Quirk na Greenbaum, 1973). Kwa mfano:

**85. Si kazi yake tu iliyomfanya Faraji apendezwe na Rashidi; tabia yake vilevile ilikuwa nzuri.** **(Shafi, 1979:60)**

Sentensi ambazo huhamisha viambajengo fulani kushoto huanza kwa kiwakilishi *ni/si* kama ilivyo katika mfano wa **(85)**. Elementi ambayo inahamishwa kushoto hufuata kiwakilishi na ndiyo elementi ambayo hutambulisha fokasi. Kutokana na mfano wa **(85)**, tunaweza tukapata sentensi zifuatazo ambazo viambajengo vyake vingine vimehamishwa kushoto.

**86. Sentensi: Rashidi alimpendeza Faraji kwa tabia yake nzuri.**

**a. Fokasi kwenye kiima:**

*Ni Rashidi aliyempendeza Faraji kutokana na tabia yake nzuri.*

**b. Fokasi kwenye kitenzi:**

*Ni kupendezwa na Rashidi alivyohisi Faraji kwa sababu ya tabia yake nzuri.*

**c. Fokasi kwenye yambwa:**

*Ni Faraji aliyependezwa na tabia nzuri ya Rashidi.*

**d. Fokasi kwenye KH:**

*Ni kutokana na tabia yake nzuri, Faraji akapendezwa na Rashid.*

**e. Fokasi kwenye KN:**

*Ni tabia nzuri ya Rashidi iliyompendeza Faraji.*

Sentensi zenye kuhamisha viambajengo vingine kushoto kama katika **(86a) – (86e)** hutambulisha fokasi inayobeba taarifa mpya pale ambapo msisitizo unapokosa. Viambajengo vilivyotajwa huwa na athari ya fokasi linganuzi kuwa sio kiambajengo kingine katika tungo ambacho kinatambulisha fokasi isipokuwa kile ambacho kimehamishwa kushoto. Viambajengo vingine vyote huchukuliwa kama vyenye kubeba taarifa inayojulikana na ndivyo hutambulisha mada ya kishazi.

Tungo tulizotoa hapo juu pia huweza kuhamisha kushoto viambajengo vinavyotambulisha fokasi kwa kutumia kiwakilishi *si* kama vile:

**87. Si Hamisi, bali Rashidi aliyempendeza Faraji kutokana na tabia yake nzuri.**

Katika Kiswahili Sanifu, uhamishaji kushoto wa viambajengo vinavyotambulisha fokasi katika sentensi hutokea kwenye viambajengo vya kileksika kama tulivyopata katika uchanganuzi wetu. Pia hutokea kwenye virai kama vile katika KN na KH, kama ilivyo hapo juu. Kitenzi pia huweza kuhamishwa kushoto ikiwa KT kizima kinahamishwa kuliko kuhamisha kitenzi peke yake, kama vile;

| | | |
|---|---|---|
| **88.** | **Sentensi:** | **Mpishi alimmwagilia maji mtoto jana.** |
| | **T pekee;** | **Ni kummwagilia maji mtoto alivyomfanyia mpishi jana.** |
| | **KT:** | **Ni kummwagilia maji mtoto jana alivyofanya mpishi.** |

## 4.7. Hitimisho

Katika sura hii, tumeshughulikia baadhi ya tungo ambazo hutumika katika kutambulisha fokasi. Tumechanganua aina za fokasi: fokasi kwenye kiarifu, kweye agumenti, kwenye sentensi na fokasi finyu. Aina hizi nne za fokasi hulingana na majukumu ya kimsingi ya kuwasiliana: kutolea maelezo mada fulani, kutambulisha KN katika kauli, na kutanguliza kirejelewa kipya katika diskosi au kutoa ripoti kuhusu tukio fulani.

Aidha, tumeshughulikia na kuchanganua utambulishaji wa fokasi katika ukanushaji, katika tungo ambazo ni maswali yanayohitaji majibu ya ndiyo/la au maelezo. Katika tungo za aina hii tumebainisha utambulishaji wa fokasi kwenye viambajengo mbalimbali ambavyo hubeba taarifa mpya na ambayo inatajwa kwa mara ya kwanza katika diskosi.

Hatimaye, uchanganuzi wetu umehusu utambulishaji wa fokasi kwenye tungo ambazo huhamisha viambajengo vyake kushoto ili kutambulisha fokasi. Tumepata kuwa kila kiambajengo katika sentensi huweza kuhamishwa kushoto kikiwa na muundo wa kileksika au kikiwa kirai au kishazi kizima. Tungo za aina hii hutangulizwa kwa kutumia viwakilishi *ni/si* ambavyo hufuatwa na elementi inayotambulisha fokasi na ambayo hubeba taarifa mpya na muhimu.

Kwa jumla, tutasema kuwa fokasi katika Kiswahili Sanifu hutambulishwa katika KN, kiarifu na katika sentensi. Iwapo fokasi itachukua nafasi ya kwanza katika sentensi, kiambajengo ambacho hutambulisha fokasi hutangulizwa na *ni* katika sentensi yakinishi au *si* katika sentensi kanushi, kama tulivyoeleza awali.

Katika sura inayofuata tutajikita katika kuangalia na kuchanganua mahusiano yaliyopo kati ya mada na fokasi.

# SURA YA TANO

# UHUSIANO KATI YA MADA NA FOKASI

## 5.1 Utangulizi

Katika sura ya nne, tumejikita katika uchanganuzi wa tungo ambazo hutambulisha fokasi katika Kiswahili Sanifu. Tumeshughulikia aina mbalimbali za fokasi huku tukitolea maelezo yanayohusiana na utambulishaji wa fokasi katika KN, kiarifu, sentensi, na kuhusu fokasi finyu. Tumeshughulikia fokasi katika ukanushaji, jinsi inavyoweza kutambulishwa katika maswali yanayohitaji majibu ya 'ndiyo/la' na katika maswali yenye maelezo kwenye majibu. Aidha tumechanganua utambulishaji wa mada na fokasi katika tungo ambazo huhamisha viambajengo ambavyo huwekewa msisitizo kushoto au kulia katika sentensi. Tumetolea maelezo katika uchanganuzi wa data kutoka makala mbalimbali na pia data ambayo tumezalisha sisi wenyewe. Pia tutaangalia hali ambapo kiambajengo katika sentensi hutambulisha mada na fokasi kwa wakati mmoja.

Katika sura hii, tutaangalia jinsi mada na fokasi huhusiana katika muktadha wa utambuzi na uchochezi. Pia tutachanganua tungo ambazo zitatuongoza katika kupata uhusiano uliopo kati ya mada na fokasi huku tukijikita kwenye fokasi linganuzi na mada linganuzi. Haya yatatupa mwangaza katika kutambua nafasi ya mada na fokasi katika Kiswahili Sanifu.

## 5.2 Utambuzi, Uchochezi, na Vigezo vya Mada - Fokasi

Utambuzi ni dhana ambayo hutumiwa kurejelea hali ambayo msemaji huwa anatamani kutoa dai linalohusu kirejelewa fulani ambacho anachukulia kuwa hakijawakilishwa kwenye utambuzi wa msikilizaji na ambacho hakiwezi kurejelewa kwa kutumia vionyeshi. Kutokana na hali kama hii, msemaji hana budi kutoa kiwakilishi cha kirejelewa hicho kwa kutumia lugha na ambacho kitarejelewa tena katika diskosi itakayofuatia.

Uchochezi ni dhana ambayo hutumiwa kuelezea kuwa msikilizaji huwa anatarajiwa kuwa ana uchukulio wa kirejelewa chochote kitakachotajwa katika mazungumzo, na kuwa huwa ana utambuzi wa chochote anachokijua pindi tu kinapotajwa katika mazungumzo. Hata hivyo, hali ya kuwa mtu ana uelewa wa kitu fulani na kuwa anafikiria juu ya kitu fulani ni hali mbili tofauti za utambuzi. Ili mtu aweze kuwasilisha taarifa fulani huwa anahitaji uelewa wa taarifa hiyo na pia utambuzi wake. Lambrecht (1994:93) anatilia mkazo umuhimu wa kujitolea kwa msikilizaji na uwezo wake wa kuweka utambuzi kulingana na mahitaji yanayotolewa na miundo ya uchukulio ya msemaji.

Dhana za utambuzi na uchochezi huweza kudhihirishwa kama ifuatavyo:

**89. a. Nilisikia jambo la <u>kushangaza</u> jana usiku. Unamkumbuka <u>Hassani</u>, yule kijana aliyekuwa nasi <u>safarini</u>, ambaye ni <u>mgonjwa</u>? <u>Rafiki yake</u> aliaga dunia kutokana na <u>Ukimwi.</u>**

**b. Nimesikia jambo la <u>kushangaza</u>. Unamkumbuka <u>Hassani</u>, yule <u>kijana</u> aliyekuwa nasi <u>safarini</u>, ambaye ni <u>mgonjwa</u>? Nilikutana na <u>rafiki yake</u> jana akaniambia kuwa anaugua <u>Ukimwi</u>.**

Kutokana na mifano **(89a)** na **(89b)**, uchochezi wa hadhi ya kirejelewa, *rafiki yake*, una ulinganifu. Inaeleweka kuwa kirejelewa hiki hakijatajwa hapo mbeleni na kuwa kitafahamika kutokana na kirejelewa kingine katika muktadha. Lakini kuna tofauti ya kipragmatiki iliyopo katika virai nomino *rafiki yake* ambavyo si rahisi kutambua.

Katika **(89b)**, kirejelewa *rafiki yake* kinapewa umuhimu zaidi wa kipragmatiki kuliko katika **(89a)**. Umuhimu huu unahusiana na ukweli kuwa katika **(89b)**, KN *rafiki yake* kinaweza kikachukuliwa kama chenye umaarufu zaidi kiarudhi. Hadhi ya kirejelewa katika **(89a)** ni kuwa KN kina uamilifu wa kiima tofauti na ilivyo katika **(89b)** ambapo kinatokea kama KH kinachofuata kitenzi. Kisarufi, kirejelewa katika **(89a)** kinadokeza kuwa tayari kimetumika katika diskosi na hivyo basi kinatambulisha mada ya kauli hiyo. Lakini katika **(89b)**, tunadokezewa kuwa kirejelewa kinatolewa kwenye utambuzi wa msikilizaji kama kile ambacho hakijatumika katika diskosi iliyotangulia.

Tukiangalia katika kirai, *nilikutana na rafiki yake jana*, tunapata kuwa kinaweza kikachukuliwa kama kauli ya kuwasilisha taarifa fulani na ambayo jukumu lake ni kutanguliza kirejelewa cha KN kwenye diskosi kuliko kutoa taarifa kuhusu kiwakilishi cha kiima ni- katika kitenzi *<u>ni</u>likutana*.

Tofauti iliyopo kati ya **(89a)** na **(89b)** ni kuwa katika **(89a)**, tunapata kauli inayowasilisha ombi kwa msikilizaji ili awe kama alikuwa na utambuzi wa KN *rafiki yake* mbeleni, huku katika **(89b)** hakuna ombi ambalo linawasilishwa kwa kuwa kauli hii haibebi uchukulio wowote.

Hali kama hizi hudhihirisha kuwa vigezo vya utambuzi na uchochezi havitoi uamuzi kamili unaohusiana na muundo wa taarifa katika sentensi. Tunaweza tukasema kuwa muundo wa kisarufi wa sentensi pamoja na uwasilishaji wa virejelewa katika diskosi huwa na uhusiano na kuwa uhusiano huu hutegemea kipengele huru. Kipengele hiki huru hujumlisha muundo wa mada na muundo wa fokasi katika kauli ambapo kirejelewa huwa na uamilifu wa KN.

Tukizingatia vipengele hivi huru, tutasema kuwa kuna sababu ambazo hutofautisha kati ya *rafiki yake* katika **(89a)** na *rafiki yake* katika **(89b)**. Katika **(89a)** kirejelewa cha KN kinarejelea au kina uamilifu wa kipragmatiki wa kutambulisha mada huku katika **(89b)**, kirejelewa cha KN kikiwa na uamilifu wa kutambulisha fokasi katika kauli. Haya yanatubainishia uwepo wa mahusiano kati ya kutumika tena kwa kirejelewa, kiima na mada kwa upande mmoja na mahusiano kati ya kutanguliza kirejelewa upya, yambwa na fokasi kwa upande mwingine.

Katika Kiswahili Sanifu, tofauti kati ya mada na fokasi hudhihirika wazi katika hali ambapo kirejelewa kilichotolewa ili kitumike huweza kupewa utambulisho upya wa

kuwa na uamilifu wa mada au fokasi. Kiswahili Sanifu huweza kutambulisha virejelewa vyake huku vikisimbwa kwa kutumia viwakilishi kama vile:

**90. a. Swali: Mgonjwa amekula tayari?**

**Jibu: i. Mgonjwa alisema kuwa amekula <u>mara mbili.</u>**

**ii. Mgonjwa alisema kuwa wamemlisha <u>mara mbili.</u>**

Kutokana na majibu haya mawili, viambishi viwakilishi *a-* katika a*lisema* na *–m-* katika *wame*m*lisha,* vinamrejelea mgonjwa. Viambishi viwakilishi hivi vimetumika vikiwa na uhusiano wa mada ya kauli ambayo ni *mgonjwa.* Kiambajengo ambacho kinapokea au kinapewa msisitizo katika majibu **(i)** na **(ii)**, ni kielezi *mara mbili* ambacho kinatambulisha fokasi.

Tunaweza tukaonyesha uhusiano kati ya mada na fokasi kama ifuatavyo:

**b. Swali: Walimpiga nani?**

**Jibu: i. Ali alisema kuwa <u>a</u>likuwa <u>a</u>mepigwa.**

**ii. Ali alisema kuwa <u>wa</u>likuwa <u>wa</u>mempiga.**

Kutokana na mfano huu tunapata kuwa viambishi *a-* katika *alikuwa amepigwa,* na *–m-* katika *wamempiga,* ni vya mrejeo sabiki na kuwa vinatumika kurejelea kirejelewa *Ali* ambacho ndicho fokasi ya kauli hizi mbili. Tofauti na mfano **(90a)**, viambishi wakilishi hivi havijatumika kutambulisha mada bali kutambulisha fokasi ya kauli hizo.

Mifano tuliyotoa hapo juu inatudhihirishia kuwa mada na fokasi hutambulishwa katika sentensi kutegemea utambuzi na uchochezi wa virejelewa katika kauli. (Lambrecht, 1994:115). Pia mpangilio wa maneno katika sentensi hubainisha ni sehemu gani ya kishazi ambayo hutambulisha mada na ni gani hutambulisha fokasi.

Aidha, miundo ya sentensi ambazo hubeba kauli za maswali pia hudhihirisha uhusiano kati ya mada na fokasi. Kwa mfano, tukitazama mfano wa **(90a)**, tunapata kuwa swali hili linabeba uchukulio na inatokea kuwa ni rahisi kutambua viambajengo vinavyo-tambulisha mada au fokasi katika majibu yake. Ikiwa swali halibebi uchukulio, basi viambajengo ambavyo vinatumika upya katika majibu huwa vimetumika kutambulisha fokasi.

Tumepata kuwa kiambajengo katika sentensi huweza kutambulisha fokasi na mada kwa wakati mmoja kikitokea tu mwanzoni mwa diskosi. Msemaji hutanguliza mambo mapya katika diskosi na tunapata kuwa kiambajengo kinachopewa msisitizo huwa ndicho mada ya kauli hiyo na wakati huo huo hutambulihshwa kama fokasi.

## 5.3 Ulinganuzi

### 5.3.1 Fokasi Linganuzi

Dhana ya ulinganuzi kulingana na Halliday (1967:206) huelezwa kama kinyume cha kinachoarifiwa. Halliday anafafanua fokasi linganuzi kama inayohusiana na viwakilishi vinavyotangulizwa mara ya kwanza katika diskosi na yenye kubeba taarifa mpya X, kimuundo, kwa mfano:

**91. Ninaenda, wengine wakitaka watafuata.**

Kutokana na kauli hii kitenzi *naenda* kinabeba kiambishi kiwakilishi cha msemaji *{ni-}* ambacho kina ulinganuzi na watu wengine ambao wanatajwa katika kauli huku wakitambulishwa na viambishi wakilishi *{wa-}* katika vitenzi *wakitaka watafuata*.

Pia tunapata ulinganuzi wa fokasi katika virejelewa vinavyotumika mara ya kwanza kama nomino, kama vile:

**92. Swali: Kati ya Ali, Hassani na Abdi, nani mkubwa?**

**Jibu: Abdi ndiye mkubwa**

Kirejelewa *Abdi* katika jibu kinatumika katika ulinganuzi wa fokasi kati yake na virejelewa vingine katika swali, yaani *Ali* na *Hassani*. Kulingana na Halliday, tunapata kuwa virejelewa vinavyotangulizwa mara ya kwanza kama viwakilishi vya nomino huwa na ulinganuzi, lakini sio lazima virejelewa hivi viwe viwakilishi, huweza pia vikatokea kama KN, kama vile:

**93. "......... shahidi huyo anasema uwongo." (Shafi 1979:190)**

Kutokana na kauli hii, msomaji anaweza akabuni au akazua muktadha unaofaa. Inaeleweka kuwa katika mazungumzo ya msemaji, fokasi iko kwenye kiambajengo *shahidi huyo* na ambacho kinaweza kufasiriwa kwamba kina ulinganuzi na mashahidi wengine ambao walitarajiwa kutoa ushahidi wao mahakamani, hivi kwamba, *sio shahidi mwingine bali shahidi huyo anayesema uwongo.*

Kutokana na kauli hii, fokasi huweza kutambulishwa kama inayochukua nafasi tangulizi katika sentensi kama vile, *"...... shahidi huyo anasema uwongo"* au kama ambayo

inachukua nafasi ya mwisho katika sentensi kama vile, *"..... anasema uwongo shahidi huyo."*

Kutokana na mifano hii, tunapata kuwa kuna utambulishaji wa fokasi linganuzi. Vile vile tunaweza tukatofautisha fokasi linganuzi na fokasi kwenye KN. Kwa mfano:

**94. a. Abdi ndiye mkubwa.**

**b. Mkubwa wao ni <u>Abdi</u>.**

Katika **(94b)** tuna mfano wa fokasi linganuzi huku **(94a)** ikiwa na utambulishaji wa fokasi kwenye KN. Hata hivyo, huwa sio rahisi kutambua ni muundo gani wa sentensi ni linganuzi na ni upi usio linganuzi isipokuwa tu pale tunaporejelea muktadha wa mazungumzo katika diskosi.

Lambrecht (1994:289), anatofautiana na Halliday (1967) na kusema kuwa dhana ya ulinganuzi haiwezi ikatumika katika sentensi ambazo huwa na fokasi pana kwa kuwa mawanda ya fokasi hayajumlishi kirejelewa kimoja peke yake bali kirejelewa na taarifa yote inayohusiana na kirejelewa hicho, yaani, kiima- kiarifu. Kwa mfano:

**95. Swali: Kumetokea nini?**

**Jibu: Gari langu limeharibika.**

Mawanda ya fokasi yako kwenye sentensi nizima.

Lambrecht (1994:289), akimnukuu Chafe (1974) anaeleza sifa tatu ambazo ni muhimu katika ulinganuzi:

a. Lazima pawe na uelewa wa kimsingi wa hali fulani. (kama vile kati ya msemaji na msikilizaji kuwa mtu fulani alifanya kitu.)

b. Kuwe na wahusika wawili watakaotimiza jukumu la ulinganuzi.

c. Kuwe na dai kuwa wahusika hawa ndio wanaoshiriki.

Kulingana na Chafe, ulinganauzi hutokea tu ikiwa sifa hizi tatu zitafuatwa au kutimizwa. Kutokana na sifa za Chafe tunaweza tukatofautisha sentensi zifuatazo:

**96. a. Ulitaka nini?**

**Nilitaka chai tatu.**

**b. Ulitaka chai ngapi?**

**Nilitaka chai tatu.**

Katika **(96a)** msemaji anachukulia kuwa kuna vitu vingine ambavyo msikilizaji angetaka mbali na *chai tatu* na katika **(96b)**, hakuna ulinganuzi na pia uchukulio wowote kwa kuwa tayari katika swali msemaji anaelewa kuwa msikilizaji alitaka chai lakini hakuelewa ni chai ngapi. Hata hivyo sentensi ambazo hutamkwa zikiwa na uchukulio wa msemaji huweza kutofautishwa kutokana na sentensi ambazo si linganuzi na ambazo hazibebi uchukulio wowote.

Hata hivyo tunaweza tukasema kuwa uwekaji wa msisitizo kwenye kiambajengo ambacho kinatanguliza kirejelewa kwa mara ya kwanza hauwezi ukafafanuliwa kwa kutumia dhana ya ulinganuzi (Chafe (1974) na Halliday (1967)) bali kwa kuzingatia muundo wa fokasi. Dhana ya ulinganuzi haiwezi kufikiriwa tu kama kategoria ya sarufi bali kama wazo la ulinganuzi tunalopata tusikiapo kauli fulani zikitamkwa na kuzifasiri kulingana na muktadha wa mazungumzo.

Lambrecht (1994:290) anamnukuu Bolinger (1961:87) ambaye anatoa ufafanuzi wa dhana ya ulinganuzi kama;

> ***Katika semantiki, maana zote huwa na ulinganuzi. Kwa mfano tunaposema, "tukimbieni', ikiwa kauli imesemwa nje ya muktadha maalum tunapata kuwa haitakuwa na ulinganuzi wowote na kitu kama mbio bali ulinganuzi ambao upo ni kati ya kukimbia na kitu kingine ambacho watu hao wangekifanya. Jinsi tunavyofinya mawanda ya kitu kingine ambacho kingefanywa, ndivyo tunavyozidi kukaribia kupata ulinganuzi maalum wa kitu hicho.***
>
> **(Tafsiri yetu)**

Kutokana na ufafanuzi huu tunapata kuwa viwakilishi ambavyo husisitizwa katika sentensi huchukuliwa kama vyenye ulinganuzi kwa kuwa viwakilishi hivi huwa havipewi msisitizo katika diskosi. Viwakilishi hivi ambavyo havipewi msisitizo huwa na uamilifu wa kutambulisha mada na uwepo wake katika sentensi hufasiriwa kama njia muhimu ya kuwasiliana au kuwasilisha taarifa.

### 5.3.2. Mada Linganuzi

Kulingana na uchanganuzi wa fokasi linganuzi hapo awali, tumepata kuwa viambajengo katika sentensi hubeba virejelewa ambavyo hupewa mkazo na kutambulisha fokasi vilevile. Virejelewa hivyo hupewa mkazo na kutambulisha mada. Kwanza tutatofautisha kati ya fokasi linganuzi na mada linganuzi. Kwa mfano:

97. **Nilikutana na Maria na Juma jana. Mmoja ametuma salamu na mwingine amekasirika sana na wewe.**

Kutokana na kauli hii, viwakilishi vinavyopewa mkazo, *mmoja* na *mwingine*, vinatumika kusimba virejelewa viwili ambavyo vina ulinganuzi: *Maria* na *Juma*. Uamilifu wa aina hii wa mada linganuzi kama tulivyotaja hapo awali huwa tofauti na fokasi linganuzi. Kama tulivyotaja awali, mada haitambulishwi katika ukanushaji kwa kuwa ukanushaji hunasibishwa na utambulishaji wa fokasi. Mada huwa nje ya mawanda ya ukanushaji.

Tofauti iliyopo kati ya mada linganuzi na fokasi linganuzi ni rahisi kutambua kwa kuwa inadhihirika kiarudhi na pia kimofosintaksia, kama vile:

**98. <u>Ni</u>naenda wengine <u>wa</u>naweza <u>wa</u>kafuata ikiwa <u>wa</u>nataka.**

Kutokana na kauli hii, kiambishi kiwakilishi {*wa-*} ambacho kinapewa msikiko kinafafanua ulinganuzi wa mada kwa kuwa ni kiambishi kitangulizi ambacho kimetumika kurejelea watu wengine ambao walikuwa pamoja na msemaji wakati wa mazungumzo. Lakini kiambishi kiwakilishi {n*i-*} katika ni*naenda* kinatambulisha fokasi kwa kuwa kinarejelea msemaji ambaye hajatokea hapo awali katika diskosi.

Tunaweza pia tukapata uhusiano zaidi kati ya mada linganuzi na fokasi linganuzi kwa kufuata mfano huu:

**99. Njeri: Kamau, wewe <u>utafua nguo</u>, na mimi <u>nipike</u>.**

**Kamau: Hapana, <u>mimi</u> nitapika, na <u>wewe</u> ufanye <u>kitu kingine</u>.**

Kulingana na matamshi ya *Njeri* tunapata kuwa ni yenye muundo wa mada – kiarifu. Viwakilishi *mimi* na *wewe* vinadhihirisha mada linganuzi. Lakini katika matamshi ya *Kamau*, tunapata ulinganuzi wa fokasi kati ya kile *Maria* atafanya na kile *Kamau*

Kutokana na kauli hii, viwakilishi vinavyopewa mkazo, *mmoja* na *mwingine*, vinatumika kusimba virejelewa viwili ambavyo vina ulinganuzi: *Maria* na *Juma*. Uamilifu wa aina hii wa mada linganuzi kama tulivyotaja hapo awali huwa tofauti na fokasi linganuzi. Kama tulivyotaja awali, mada haitambulishwi katika ukanushaji kwa kuwa ukanushaji hunasibishwa na utambulishaji wa fokasi. Mada huwa nje ya mawanda ya ukanushaji.

Tofauti iliyopo kati ya mada linganuzi na fokasi linganuzi ni rahisi kutambua kwa kuwa inadhihirika kiarudhi na pia kimofosintaksia, kama vile:

**98. Ninaenda wengine wanaweza wakafuata ikiwa wanataka.**

Kutokana na kauli hii, kiambishi kiwakilishi {*wa-*} ambacho kinapewa msikiko kinafafanua ulinganuzi wa mada kwa kuwa ni kiambishi kitangulizi ambacho kimetumika kurejelea watu wengine ambao walikuwa pamoja na msemaji wakati wa mazungumzo. Lakini kiambishi kiwakilishi {*ni-*} katika ni*naenda* kinatambulisha fokasi kwa kuwa kinarejelea msemaji ambaye hajatokea hapo awali katika diskosi.

Tunaweza pia tukapata uhusiano zaidi kati ya mada linganuzi na fokasi linganuzi kwa kufuata mfano huu:

**99. Njeri: Kamau, wewe utafua nguo, na mimi nipike.**

**Kamau: Hapana, mimi nitapika, na wewe ufanye kitu kingine.**

Kulingana na matamshi ya *Njeri* tunapata kuwa ni yenye muundo wa mada – kiarifu. Viwakilishi *mimi* na *wewe* vinadhihirisha mada linganuzi. Lakini katika matamshi ya *Kamau*, tunapata ulinganuzi wa fokasi kati ya kile *Maria* atafanya na kile *Kamau*

atakachokifanya. Kuwa kauli wazi ya X *'atapika'* inabeba uchukulio wa kipragmatiki. Tukiangalia kishazi cha pili katika matamshi ya *Kamau*, *'.... Na wewe ufanye kitu kingine'* tunapata muundo wa mada – kiarifu pale kiambajengo *na wewe* kina uamilifu wa mada linganuzi.

Hali kadhalika, uhusiano zaidi unajitokeza katika kauli hii:

**100. <u>Pesa hizo</u> alizilipa <u>jana.</u>**

Kulingana na sentensi hii, KN *pesa hizo* huchukuliwa kuwa na uamilifu wa kutambulisha mada, lakini kimetumika kutambulisha fokasi linganuzi ambayo imehamishwa kushoto au kutangulizwa mwanzoni mwa sentensi. Kwa upande mwingine, KN *pesa zako*, huweza kutambulisha mada linganuzi huku kikiwa kimetumika hapo awali katika diskosi. Kawaida kauli hizi huchukuliwa kuwa zenye kutambulisha mada linganuzi:

**a. <u>Pesa hizo</u> alizilipa jana.**

**b. <u>Nyumba zote</u> tulizikamilisha jana.**

Virai nomino vinavyotangulia katika kauli hizi mbili vinachukuliwa kuwa vyenye ulinganuzi hata kama vina uamilifu tofauti, wa kutambulisha mada au fokasi.

## 5.4 Hitimisho

Katika sura hii, tumeshughulikia maswala mbalimbali miongoni mwa mengine ambayo yanatumika katika kubainisha uhusiano kati ya mada na fokasi. Tumepata kuwa mbali na utambuzi na uchochezi, kuna vigezo vingine vya mada na fokasi ambavyo hubainisha ni

viambajengo gani hutambulisha mada au fokasi. Moja kati ya vigezo hivi ni mpangilio wa maneno katika sentensi ambao kama tulivyosema awali huwa huru kwa kiasi katika Kiswahili Sanifu.

Vile vile, tumeshughulikia dhana ya ulinganuzi katika mada na katika fokasi. Tumetolea maelezo yanayohusiana na ulinganuzi kati ya mada na fokasi ili kudhihirisha uhusiano kati yazo.

Katika sura ya sita, tutajikita katika kuhitimisha utafiti huu huku tukitoa kwa muhtasari matokeo ya uchanganuzi wetu. Aidha, tutatoa mapendekezo yatakayochochea tafiti zaidi katika uwanja huu.

# SURA YA SITA

# HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 6.1 Utangulizi

Sura hii itashughulikia mambo mawili muhimu; hitimisho la utafiti na kutoa mapendekezo. Katika hitimisho tutaelezea matokeo ya utafiti huu huku tukionyesha kufanikiwa kwa malengo yetu ya utafiti pamoja na nadharia tete. Katika mapendekezo tutaelezea kwa kina maeneo ambayo tungetaka yashughulikiwe katika tafiti zijazo kuhusiana na uwanja huu wa utafiti.

## 6.2 Hitimisho

Katika utafiti huu tumeshughulikia maswala mbalimbali yanayohusiana na utambulishaji wa mada na fokasi katika Kiswahili Sanifu. Madhumuni ya utafiti huu yalikuwa ni kuchunguza utambulishaji wa mada na fokasi katika Kiswahili Sanifu, kutathmini ikiwa mada na fokasi hutambulishwa katika kirai, kishazi au kileksika, kubainisha uhusiano kati ya mada na fokasi na mwisho kutathmini kufanikiwa kwa mtazamo wa muundo wa taarifa katika utafiti huu.

Uchanganuzi wa data umeshughulikia utambulishaji wa mada na fokasi katika sentensi ambazo ziko katika muktadha wa diskosi. Uamilifu wa mada katika sentensi ni kutaja kirejelewa ambacho hutambulisha mada kwenye diskosi au kuelezea uhusiano wa kisemantiki kati ya kirejelewa cha mada na kiarifu. Sarufi hutenganisha majukumu haya

mawili ya mada kwa kuwa pale kirejelewa kinapotajwa katika diskosi, tunapata kuwa mada husimbwa kwa kutumia virai nomino vya kileksika. Na pale uhusiano wa kisemantiki unapoelezwa kati ya kirejelewa na kiarifu mada husimbwa kwa kutumia viwakilishi. Viwakilishi hutambulishwa kisarufi kama vyenye uamilifu wa mada.

Katika uchanganuzi wa data tumepata kuwa uhusiano kati ya mada na kauli huchukuliwa kipragmatiki kama kurudisha kirejelewa tena katika diskosi wakati tamko linapotolewa, hivi kwamba ili kitu fulani kitumike kama mada, lazima kipewe uchukulio kuwa kitarejelewa mara kwa mara katika kauli au diskosi. Tofauti na ilivyo kwenye elementi yoyote ya fokasi, uhusiano kati ya fokasi na kauli huwa kinyume na ule wa mada kwa kuwa elementi ya fokasi huwa imetangulizwa katika diskosi kwa mara ya kwanza. Haiwezi ikawa imetumika au imejitokeza katika diskosi iliyotangulia. Elementi ya fokasi huwa haina urejelezi kama ilivyo katika mada hivi kwamba wakati tamko linapotolewa, kiambajengo kinachotambulisha fokasi huwa kinatolewa kwa mara ya kwanza na huwa hakibebi uchukulio wowote.

Tumeshughulikia tungo ambazo hutambulisha mada katika Kiswahili Sanifu. Kama katika tungo ambazo hutambulisha fokasi, tungo hizi pia huenda kinyume na mpangilio wa maneno ambao huwa huru kwa kiasi katika Kiswahili Sanifu. Mada linganuzi ambayo haijatokea katika nafasi ya kwanza katika sentensi huweza kutangulizwa na kuchukua nafasi ya kwanza katika kishazi hicho. Hili huenda sawia na muundo bia wa kuwa mada huchukua nafasi ya kiima katika sentensi.

Katika uchanganuzi huu, pia tumeshughulikia uhamishaji wa mada kushoto. Tumepata kuwa ikiwa kirejelewa fulani kimetumika katika diskosi na kikakosa kutumika kwa muda, kirejelewa hicho huweza kikatumika tena kinaporudishwa katika diskosi. Kirejelewa kinaporudishwa katika muktadha, huwa kinatangulizwa katika kauli ambayo inakiwasilisha. Virejelewa ambavyo huhamishwa kushoto ni vile ambavyo vimetumika katika diskosi na baadaye panakuwa na haja ya kuvitumia upya.

Uhamisho wa mada kulia ni kigezo kingine ambacho tumeshughulikia katika uchanganuzi wa data. Kinyume na madai ya wanaisimu wa Shule ya Prague ambao hudai kuwa mada huchukua nafasi ya kiima katika kishazi, tunapata kuwa mada huweza ikachukua nafasi ya mwisho katika kishazi. Hali hii ni dhahiri katika Kiswahili Sanifu hasa katika muktadha wa mazungumzo. Hili husaidia katika kubeba taarifa inayowasilishwa na kauli fulani na ambayo inahusu kirejelewa cha mada, hadi mwishoni mwa sentensi. Hii ni njia mojawapo ya kujenga au kubeba taharuki kwa upande wa msomaji au msikilizaji ili atake kujua ni kitu gani ambacho kinarejelewa katika taarifa.

Matokeo zaidi katika utambulishaji wa mada ni kuwa mada huweza kutambulishwa kama yambwa tendwa au yambwa tendewa. Katika Kiswahili Sanifu, kiambajengo ambacho hutambulisha mada kati ya yambwa tendwa na yambwa tendewa ndicho hutangulia katika sentensi huku kikifuata kitenzi. Vigezo hivi huwa kwenye mawanda ya KT na kile ambacho hufuata kitenzi ndicho hutambulisha mada ya kauli hiyo. Yambwa tendwa na yambwa tendewa huweza zikabadilishana nafasi katika sentensi kutegemea ni kiambajengo kipi kitakachotambulisha mada katika sentensi hiyo. Kwa hivyo, mada

katika Kiswahili Sanifu hutambulishwa katika kiwango cha kirai, kishazi na kileksika kwa kuitanguliza katika sentesni, kuihamisha kushoto au kulia na kwa kuihamisha yambwa tendwa au tendewa.

Kigezo kingine ambacho tumeshughulikia katika uchanganuzi wetu na ambacho ni muhimu katika muundo wa taarifa katika sentensi ni kile cha fokasi. Tumepata kuwa muundo wa fokasi katika sentensi ni ile kaida ya uhusiano kati ya muundo wa sentensi na fasiri ya fokasi katika kauli inayoitambulisha. Tumechanganua aina mbalimbali za fokasi kulingana na mawanda ya semantiki ya fokasi katika kauli na kulingana na mawanda ya kisarufi yanayofafanua fokasi katika sentensi. Katika uchanganuzi wa fokasi katika sentensi, tumepata kuwa uamilifu wake katika mawasiliano au katika kutoa taarifa ni kuarifu hali ya mada iliyotolewa katika sentensi. Muundo wa sentensi katika Kiswahili Sanifu kwa mujibu wa fokasi kwenye kiarifu, hufuata muundo wa sentensi unaochukuliwa kama wa kimsingi wa kiima- kiarifu. Kiima kikitambulisha mada huku kiarifu kikitambulisha fokasi.

Katika utambulishaji wa fokasi kwenye KN tumepata kuwa uamilifu wake ni wa kutambulisha KN kwenye kauli iliyotolewa. Mawanda ya fokasi hujikita kwenye KN ambacho hutangulizwa katika diskosi kwa mara ya kwanza na ndicho tu miongoni mwa viambajengo vingine kinachopewa msisitizo. Tumebainisha kuwa utambulishaji wa fokasi kwenye kiarifu huchukuliwa kuwa kinyume cha utambulishaji wa fokasi kwenye KN.

Muundo wa taarifa huweza kujitokeza katika fokasi finyu. Aina hii ya fokasi huwa na mawanda ambayo hujikita kwenye kiambajengo kimoja tu katika sentensi. Fokasi huweza kutambulishwa kwenye kiima, yambwa tendwa au tendewa au kwenye kategoria nyingine yoyote ya kisintaksia kama vile nomino, kitenzi, kiwakilishi, kielezi, kivumishi, n.k. Uchanganuzi tulioufanya umetudhihirishia kuwa fokasi huweza kutambulishwa katika kategoria hizi za maneno katika Kiswahili Sanifu.

Kinyume na fokasi finyu kuna fokasi pana ambayo hutambulishwa katika sentensi au kishazi kizima huku ikiwacha nje kategoria yoyote yenye utambulishaji wa mada. Uamilifu wake huwa ni kutanguliza kirejelewa kipya katika diskosi au kutoa ripoti kuhusu tukio fulani. Fokasi huwa imetambulishwa kwenye muundo mzima wa sentensi wa kiima – kiarifu na kama tulivyotaja awali, mawanda ya fokasi huwa kwenye sentensi. Tumebaini kuwa kishazi ambacho hutambulisha fokasi huwa hakibebi uchukulio wowote wa kipragmatiki.

Hata hivyo, sentensi katika Kiswahili Sanifu huweza ikadhihirisha majukumu yote ya utambulishaji wa fokasi yaani katika kiarifu, katika KN na katika sentensi. Kutokana na majukumu haya tunapata migao miwili ya fokasi: fokasi finyu na fokasi pana.

Tukizingatia umuhimu wa nadharia ya muundo wa taarifa tunapata kuwa imefanikisha harakati za uchanganuzi wa data unaohusiana na tungo zinazotambulisha mada na fokasi. Pia tumepata kuwa kategoria ambazo husimba tofauti za muundo wa taarifa huwa zenye

miundo ya umaanisho na huwa na ulinganifu wa maagizo kutoka kwa msemaji hadi kwa msikilizaji ya kufasiri kauli fulani kama yenye kubeba muundo wa taarifa maalum.

Kulingana na muundo wa taarifa, uamilifu wa sarufi ni kutoa ufafanuzi wa kauli ambazo umbo lake ni la kipragmatiki. Uamilifu wa diskosi hivyo basi ni wa kiasili katika mfumo maalum wa sentensi. Sentensi hazipewi uhai bila kutilia maanani muundo wa taarifa unaowasilishwa kwenye sentensi hiyo. Hata hivyo hakuna ulinganifu wa moja kwa moja kati ya kategoria ya sintaksia na kategoria ya muundo wa taarifa. Fasiri ya muundo wa taarifa katika sentensi huamuliwa na muungano wa sifa za viambajengo tofauti za kiisimu katika sentensi. Hivi ni kumaanisha kuwa uhusiano kati ya umbo la sentensi na uamilifu wake katika diskosi hutawaliwa au huongozwa na kanuni za kisarufi.

Mtazamo huu unawiana na kauli kuwa vijenzi vya lugha hupangwa pamoja kwa kufuata mfumo maalum vikizingatia sintaksia kama msingi wake na muundo wa taarifa kama sehemu badala. Ukweli wa muundo wa taarifa ni kuwa tunapotazama mpangilio wa sarufi ambapo vijenzi vya maana hutokea (mofolojia, sintaksia, arudhi na msamiati) tunapata kuwa huwa vina mwingiliano sana, na kila kimoja huhusiana na kingine. Hivyo basi hatuwezi tukatenganisha sarufi na diskosi.

Muundo wa taarifa haushugulikii tofauti kati ya sentensi zenye kufuata kanuni za kisarufi na ambazo hazifuati kanuni za kisarufi. Hii ndiyo sababu katika uchanganuzi wa data tumeweza kuchanganua kauli mbalimbali katika utambulishaji wa mada na fokasi. Kauli hizi zinakiuka muundo au mpangilio wa maneno katika sentensi unaochukuliwa kuwa wa

kimsingi wa kiima- kiarifu ili kutambua utokeaji wa muundo wa taarifa katika kauli mahususi. Tumeshughulikia mada na fokasi zikichukua nafasi mbalimbali katika sentensi kama vile kiima, kiarifu, sentensi au kama kiambajengo kimojawapo katika kishazi au sentensi.

Kama tulivyotaja awali, muundo wa taarifa umetuongoza katika uchanganuzi wa data. Pia umetuongoza katika kujibu swali katika sarufi zalishi la ni kwa nini sarufi hutoa njia tofautitofauti za kuelezea kauli moja, yaani, taarifa moja huweza kuelezewa kwa kutumia kauli mbalimbali. Uchanganuzi wa muundo wa taarifa umetuwezesha kuelewa sarufi kama mfumo wa ikolojia, au jinsi viumbe huhusiana au huingiliana na mazingira wanamoishi ili kufasiri taarifa kimuktadha.

Katika uchanganuzi wa data, tumetumia riwaya ya *Kuli* ya Adam Shafi (1979) kama msingi wa data yetu. Tumeteua kauli mbalimbali na miundo tofauti ya sentensi ambayo imekidhi mahitajii yetu. Mbali na riwaya hii, tumepata data kutoka makala mbalimbali yaliyochapishwa na pia kuzalisha data yetu wenyewe. Data hii imefanikisha uchanganuzi wetu wa kubainisha vipengele ambavyo hutambulisha mada na fokasi katika Kiswahili Sanifu.

Uchanganuzi wetu katika utambulishaji wa mada na fokasi katika Kiswahili Sanifu umeegemea katika kiwango cha sentensi ambazo zimejikita katika muktadha wa diskosi.

## 6.3 Mapendekezo

Utafiti huu umejikita katika uchanganuzi wa data katika muktadha wa kiusemi ili kubainisha utambulishaji wa mada na fokasi katika sentensi. Tunapendekeza utafiti zaidi wa mada na fokasi katika Kiswahili Sanifu katika kiwango cha kimofosintaksia.

Aidha utafiti huu umeongozwa na nadharia ya muundo wa taarifa. Hata hivyo, utafiti wa kina unaweza ukafanywa kwa kutumia nadharia nyingine tofauti kama vile nadharia ya uminimalisti ili kuchunguza vigezo vya kimofosintaksia ambavyo hutambulisha mada na fokasi katika Kiswahili Sanifu.

Kwa kuwa tumeshughulikia uchanganuzi wa data katika kiwango cha kisintaksia, tunapendekeza utafiti zaidi ufanywe ambao utashughulikia muundo wa taarifa ambao husimbwa katika mofimu, katika tungo changamani za kimofosintaksia au katika tungo za kiarudhi.

Matokeo ya utafiti wetu yanaweza kutumika darasani na walimu katika kufunzia stadi za uandishi wa kujiendeleza kama vile insha na hadithi fupi.

# MAREJELEO


Abdulla, M.S., (1968). Kisima cha Giningi. Nairobi: Evans Brothers Kenya Limited.

Aissen, J.L., (1992), "Topic and Focus in Mayan", Language Vol.68 NO1 pp 43-80. University of C alifonia: Linguistic Society of America.

Ashton, E. O., (1947). Swahili grammar (including Intonation). Second Edition. London: Longman.

Augustine, M., (2004). Topic and Focus in Swahili. Graduate Institute of Applied Linguistics: (Hakijachapishwa).

Bresnan, J na S. Mchombo (1987). Topic, Pronoun and Agreement in Chichewa. Language Vol 63, No 4 pp 741 – 782. Linguistic Society of America.

Brown, G. na G.Yule, (1983), Discourse Analysis. U.S.A: Cambridge University Press.

Carlos, G., (2008). 'Types of Focus in English', in Lee, C. et al, Cross Linguistic Perspectives on Meaning and Intonation. Pp 83-100. Springer Journals.

Chomsky, N., (1980), Rules and Reprsentations. New York. Columbia University Pres.

Cobuild, C., (1990). English Grammar. The University of Birmingham: Collins Publishers.

Cruttenden, A., (1986). Intonation. Cambridge: Cambridge University Press.

Crystal, D., (1980). A Dictionary of Linguistics and Phonetics (5th Edition). Oxford: Blackwell Publishing.

Danes, F. (1966). 'A Three-level Approach to Syntax.' In F. Danes et.al. (eds) TravauxLinguistic de Prague Vol 1 pp 225 – 240. University of Alabama.

Foley, A. W., (1996). 'Information Structure'. In Brown.K & J. Miller. Concise Encyclopedia of Syntactic Theories. Cambridge: Cambridge University Press.

Givon, T., (2001). Syntax: An Introduction. Amsterdam/ Philadelphia: John Benjamin Publishing Company.

Halliday, M.A. K., (1967). 'Notes on Transitivity and Theme in English': Part 2: Journal of Linguistics 3, pp 199-244.

Hofmann, R., (1993). Realms of Meaning: An Introduction to Semantics. London: Longman

Jackendoff, R., (1972). Semantic Interpretation in Generative Grammar. Cambridge: Mass.MIT Press.

Kanerva, J. M, (1990). 'Focusing on Phonological Phrases in Chichewa'. In Sharon, I., na Z.Draga, *The Phonology – Syntax Connection*, Chicago: The University of Chicago Press.

Lambrecht, K., (1994). Information Structure and Sentence Form: a theory of topic, focus and the mental representations of discourse referents, Cambridge: Cambridge University Press.

Lyons, J, (1968). Introduction to Theoretical Linguistics. Cambridge: Cambridge University Press.

Maw, J., na John Kelly, (1975), Intonation in Swahili, London: School of Oriental and African Studies.

Maw, J., (1976), "Focus and the Morphology of the Swahili Verb", Bulletin of the School of Oriental and African Studies. University of London, Vol.39, NO.2, pp 389-402 UK: Cambridge University Press.

Mchombo, S. A., (1980), Dative and Passive in Chichewa: an argument for surface grammar. xxxxxxxxxxxxxxxxxxxxxxxxxxxxxxxxx.

Mgullu, R.S, (1999), Mtalaa wa Isimu, Fonetiki, Fonolojia na Mofolojia ya Kiswahili. Nairobi. Longhorn Publishers.

Muller – Gotama, F., (1996), Topic and Focus in Sundanese. Anthropological Linguistics, Vol 38, NO 1, pp 117-132, New York: The Trustees of Indiana University.

Payne, J. R., (1985), "Negation". In Shopen, T., Language Typology and Syntactic Description, Vol. 1, Clause Structure, U.S.A: Cambridge University Press.

Quirk, R., na S. Greenbaum, (1973), A University Grammar of English, New Delhi: Tan Prints (1) Pvt. Ltd

Saeed, J.I., (1997), Semantics, Blackwell: Blackwell Publishing

Shafi, A., (1997), Kuli, Nairobi: Longhorn Publishers.

Sornicola, R., (1996), 'Topic, Focus and Word Order', in Brown, K., & J. Miller, Concise Encyclopedia of Syntactic Theories, Cambridge: Cambridge University Press

TUKI (2000), English-Swahili Dictionary (2nd Edition), Dar es Salaam: Institute of Kiswahili Research.

--------- (1981). Kamusi ya Kiswahili Sanifu. Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.

-------- (2001). Kamusi ya Kiswahili- Kiingereza. Swahili-English Dictionary. Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Van Valin. R. D., na R. J. La Polla. (1997). Syntax. Structure. Meaning and Function. U.K: Cambridge University Press.

Vitale. A. J., (1981). Swahili Syntax. Dordrecht. Holland. Cinnamison: N. J. Foris Publishers.

Wamitila. K.W., (2002). Bina – Adamu!. Nairobi: Phoenix Publishers.